Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# MAJADILIANO YA BUNGE

## BUNGE LA TANZANIA

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Saba – Tarehe 19 Juni, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge tungekuwa na maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini taarifa nilizozipata hadi tunachapisha *Order Paper* ni kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu asingekuwepo.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 38 fasili ya 5 Waziri Mkuu anapokuwa hayupo ama tukijua kwamba pengine hatakuwepo basi hatupangi maswali.

Lakini la pili ni kwamba wiki ijayo Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa ndiyo anawasilisha hotuba yake. Kwa hiyo, atashiriki katika kuzungumzia mambo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge mtamwuliza.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu atoe hoja ya kutengua Kanuni ile kwa ajili ya Alhamisi ijayo ili katika wiki ile ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu anashughulikia hotuba yake kusiwe na Maswali kwa Waziri Mkuu.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu,

kwa kuzingatia Kanuni ya 90 kutengua Kanuni ya Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu siku ya Alhamisi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki Hoja ya kutengua Kanuni ya Maswali kwa Waziri Mkuu siku ya Alhamisi ijayo ya tarehe 26 Juni, 2008)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge walioafiki wameshinda kwa hiyo, Alhamisi ijayo hatutakuwa na kipindi cha Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita mwuliza swali la kwanza, napenda nitambue kazi nzuri sana iliyofanywa na Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Job Ndugai katika hii siku moja na nusu nilipokuwa na shughuli ofisini. Wamekaa vizuri, wamefanyakazi nzuri sana. Nawashukuru sana. Swali la kwanza kwa siku ya leo linaulizwa na Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami, linaelekezwa ofisi ya Waziri Mkuu.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 57

### Dodoma Makao Makuu ya Nchi

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa Dodoma ni Makao Makuu ya nchi lakini haina hadhi ya kuwa Makao Makuu ya nchi:-

(a) Je, kuna viwanja vingapi vilivyotengwa kwa ajili ya Ofisi za Wizara vikitajwa namba zake na maeneo vilipo?

(b) Je, Serikali inakusudia kuhamia Dodoma mwaka gani au karne gani?

(c) Je, kuendelea kujenga majengo mapya kwenye Ofisi za Wizara na Idara zake Jijini Dar es Salaam si kiini macho cha kuiita Dodoma Makao Makuu ya nchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda nijibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mpango wa ujenzi wa Ofisi za Serikali Dodoma haukuzingatia kila Wizara kutengewa kiwanja chake bali eneo la kutosha la hekta 53 lilitengwa katika mpango kabambe wa Mji wa Dodoma kwa ajili ya kujenga maofisi ya Serikali na huduma nyingine muhimu. Eneo hili linalojulikana kimipango miji kama *National Capital Centre* lipo kando ya eneo la Mlimani, kusini mwa barabara inayojengwa sasa kwenda Chuo Kikuu cha Dodoma na limesanifiwa kimipango. Usanifu huo wa miundombinu ya eneo hili ulikamilika mwaka 1986. Kinachosubiriwa sasa ni kujengwa kwa miundombinu hiyo na usanifu wa majengo ya Ofisi za Wizara mbalimbali. Kazi ya kuufanya Mji wa Dodoma kuwa na hadhi ya Makao Makuu ya nchi inahitaji rasilimali nyingi na pia muda mrefu na siyo jambo la mara moja.

(b) Azma ya Serikali ya kuhamia Dodoma bado ipo pale pale. Uhamiaji utakwenda kwa haraka pale tu miundombinu na huduma nyingine muhimu zitakapokuwa zimewekwa kama vile nyumba za kuishi wafanyakazi na maofisi.

(c) Kutokana na kuongezeka kwa shughuli za Wizara zinazokwenda sambamba na kuongezeka kwa wafanyakazi, Wizara au idara zinalazimika kupanua maeneo ya ofisi zao kwa kujenga majengo mapya kwenye maeneo yao ili kuboresha mazingira ya utendaji kazi. Ujenzi wa majengo mapya Jijini Dar es Salaam wala si kikwazo cha Wizara hizo kuhamia Dodoma maana hata zikihamia Dodoma majengo hayo yanaweza kukodishwa kwa watu wengine maana Dar es Salaam itandelea kuwa Jiji la kibiashara. Wizara zinaweza pia kubakisha baadhi ya ofisi zao kwa shughuli zitakazopaswa kuendeshwa Jijini Dar es Salaam.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa kuna sheria ya kuendeleza Dodoma, *The Dodoma Special Investment Act* ambayo haitekelezeki kwa vile wawekezaji wanakwama kuja Dodoma kuwekeza. Je, Serikali inawasaidiaje *CDA* ili ipate wawekezaji kwa vile *CDA* tayari ina mpango mzuri sana wa kuleta Maendeleo hapa Dodoma?

(b)Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti na mpya wa kuhakikisha *CDA* inapewa fedha ya kutosha ili kupanua hiyo miundombinu ambayo Mheshimiwa Waziri amesema na mpango wake madhubuti wa Serikali wa kuhakikisha inahamia Dodoma hata kama ni wa muda mrefu kuliko ilivyo leo kuwa ni maneno tu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, maswali yake kama ifuatavyo:-

Ile sheria inayotoa nafuu kwa wawekezaji wa Dodoma bado iko na ina mvuto ni kwa vile tu ni kwa muda mrefu wawekezaji hawakuitumia sheria hiyo lakini kwa sasa nataka kumhakikishia Mbunge na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwamba sasa hivi kuna wawekezaji wengi tu ambao wanajenga hapa Dodoma.

*CDA* kwa muda mrefu haikuwa inapata ruzuku kutoka Serikalini kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti yetu. Lakini kuanzia mwaka jana na mwaka ujao wa fedha *CDA* huwa tumeitengea fedha za Maendeleo na tuna hakika kwamba itaendeleza miundombinu kujiandaa kwa ajili ya uhamiaji. Pia kwa upande wa rasilimali watu tunajitahidi sana kuwapata watumishi hasa watalaam wanaohitajika kwa ajili ya kuendeleza Mji Mkuu. (*Makofi*)

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika jibu la msingi Mheshimiwa Waziri amesema kwamba uendelezaji wa Makao Makuu ni pamoja na kuboresha miundombinu na yeye akataja nyumba tu peke yake na kwa kuwa barabara pia ni muhimu katika kuendeleza ama kuboresha Mji Mkuu wa Dodoma. Je, haoni kwamba kuna haja ya kujenga barabara za lami kutoka kila upande wa nchi ikiwepo Kusini na Kaskazini kwa maana ya kujenga barabara ya Iringa – Dodoma – Minjungu ili kuweza kuhamasisha wawekezaji? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, swali lake kama ifuatavyo:-

Nakubaliana naye kabisa kwamba miundombinu kama barabara ni muhimu sana katika kuharakisha uhamiaji wa Serikali kwenye Mji Mkuu Dodoma. Kwa upande wa Mji wenyewe fedha ambazo tunazitenga kwa mfano mwaka ujao wa fedha shilingi bilioni 2.8 ni kwa ajili ya barabara katika maeneo mapya ya Mji huu kama vile Kisasa, Chadulu na yale maeneo ya zamani ambayo barabara yake ilikuwa imeshasanifiwa kama vile Nkuhungu.

Mheshimiwa Mbunge, bila shaka atakumbuka kwamba Serikali iko mbioni sasa hivi mkandarasi ameshapatikana kwa kile kipande cha barabara kati ya Minjungu na Babati na kuna uwezekano mkubwa pia fedha zikapatikana kwa barabara ya Babati – Dodoma na ya Dodoma hadi Iringa. (*Makofi*)

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swali la msingi lilikuwa linauliza Serikali inakusudia kuhamia mwaka gani au karne gani. Mheshimiwa Waziri atakuwa hajamtendea haki mwuliza swali kwa kueleza maelezo badala ya kujibu swali, tunaomba tujue ni mwaka gani au ni karne gani? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Said Arfi, swali lake kama ifuatavyo:-

Serikali kama nilivyosema hapo awali inakusudia kuhamisha Makao Makuu Dodoma, lakini kutegemeana na hali halisi ya kifedha. Kwa uzoefu wa wenzetu, yaani waliowahi kujenga Makao Mkuu Mapya iliwachukua muda mrefu. Mfano Mzuri ni Australia. Kwa bahati mimi niliwahi kusoma kwa miaka miwili kule Australia na wiki chache zilizopita nilienda tena Canberra. Wenzetu hao waliamua kuhamia Canberra kutoka mwaka wa 1901.

Lakini ukumbi wa kudumu wa Wabunge ulikamilika mwaka 1988 miaka 87 baadaye. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya kuhamia Dodoma iko pale pale, isipokuwa tatizo ni fedha. Tukipata fedha basi zoezi la kuhamia Dodoma litakamilika. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, inaelekea mnapapenda sana Dodoma , mpaka mnapatetea kiasi hicho. (*Kicheko*)

Na. 58

**Tatizo la Maji – Mlowo**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais, kwenye kampeni zake za uchaguzi mwaka 2005 aliahidi kulipatia ufumbuzi tatizo la maji katika Mji wa Mlowo wilayani Mbozi na kwa kuwa kipindi cha miaka 5 ya uongozi wake karibu kinamalizika na maji ya visima yanayochimbwa Mlowo yanaonekana kuwa kidogo:-

(a) Je, utekelezaji wa ahadi hiyo umefikia wapi?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuuchukua mradi wa maji wa *Lukululu Group* (Mbozi Mashariki) uliokuwa ufadhiliwe na *JICA* lakini haukuendelea na ambao ungewapatia maji vijiji kumi na moja (11) pamoja na Mji wa Mlowo na hivyo kumaliza kabisa tatizo la maji kwenye mji huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki ,lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inalifahamu tatizo la Mji Mdogo wa Mlowo katika Wilaya ya Mbozi, kuhusu uhaba mkubwa wa maji.

Kwa kutambua hilo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, inaendelea na jitihada za kuboresha upatikanaji wa maji katika mji huo. Katika mpango wa muda mrefu, Serikali kupitia Halmashauri imepima na kuchimba visima viwili. Kisima kimoja kina uwezo wa kutoa maji kiasi cha mita za ujazo 2.85 kwa saa.

Kisima kingine bado hakijakamilika kwa sababu vifaa vya wakala wa uchimbaji wa visima *DDCA* viliharibika tarehe 30 Machi, 2008 wakati kazi ikiwa inaendelea. Vifaa hivyo tayari vimetengenezwa na kazi inatarajiwa kuanza tarehe 21 Juni, 2008 na kukamilika tarehe 28 Juni, 2008. Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, imetumia shilingi milioni 9.6 kwa kazi hizo zilizotangulia.

(b) Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mrefu wa kuupatia maji mji mdogo wa Mlowo unahusu kupata maji ya mtiririko kutoka katika vyanzo vya maji vilivyo katika Vijiji vya Iyule na Lukululu. Awali, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) lilionyesha nia ya kutekeleza mradi unaojulikana kama *Iyule Group*. Kwa bahati mbaya hadi sasa KKKT hawajapata wafadhili wa kujenga mradi huo kutokana na ukubwa wa mradi na gharama zake.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Lukululu bado haujapata wafadhili. Mwaka 2003, Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*) lilituma mtalaam wake kwenda Mbozi kuchunguza hali ya upatikanaji wa maji katika Wilaya hiyo. Mradi wa Mlowo ulikuwa mmoja kati ya miradi iliyopendekezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi. Miradi mingine iliyopendekezwa pamoja na Mlowo ni Iyula na Iguma.

Mheshimiwa Spika, mwezi Mei 2008, Wizara yangu imepokea maombi ya Halmashauri ya kutekeleza mradi wa Lukululu. Wizara yangu sasa imeamua kuufanyia mradi wa Lukululu upembezi yakinifu na usanifu katika mwaka wa 2008/2009, ikiwa ni matayarisho muhimu ya utekelezaji wake.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Lakini nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa amekiri kwamba kuna tatizo la msingi la maji katika Wilaya ya Mbozi na kwa kuwa sasa Serikali imekubali kuufanyia upembezi yakinifu mradi wa *Lukululu Group*. Je, si itakuwa pia vema kama Serikali itakuwa tayari kuufanyia upembezi yakinifu mradi wa *Iyule Group* ili vile vijiji ambavyo vingefaidika ambavyo viko takribani 7 (saba) na vyenyewe viweze kufaidika?

(b) Kwa kuwa Serikali kupitia miradi ya *quick wing* inatarajia kuvipatia vijiji vingi nchini maji je, kwa Wilaya Mbozi, Wizara ina mkakati gani pia wa kuvipatia vijiji vingi zaidi maji na hasa ukizingatia kwamba tunalima sana kahawa na kwa maana hii upatikanaji wa maji ungetusaidia sana katika kusafirisha kahawa yetu tunayozalisha? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Zambi kama ifuatavyo:-

Nakubaliana naye kabisa kwamba kwa kuwa Lukululu na *Iyule Group* iko katika eneo moja basi itakuwa busara kufanya upembuzi yakinifu katika miradi yote hiyo miwili. (*Makofi*)

La pili, kuhusu utaratibu wa *quick wing* ningependa kwanza nimpongeze Mheshimiwa Zambi kwamba katika utaratibu wa mwaka uliopita Wilaya ya Mbozi ndiyo ilikuwa Wilaya ya kwanza kwa kutekeleza miradi ile na kutoa taarifa na hivyo ikawa inaongoza. Kwa hiyo, tutakapokuwa tumepata fedha za *quick wing* kama zitapatikana basi Wilaya ya Mbozi ina nafasi ya kwanza kabisa katika Halmashauri zote za Miji Midogo 132. Lakini hiyo ni kutegemea na fedha hizo kama zitakuwa zimepatikana.

Kuhusu zao la kahawa ningesema mradi huu unaweza ukaibuliwa kwa sababu kule hakuna maji ya mtiririko. Kwa hiyo, naomba nimshauri Mheshimiwa Zambi kupitia Halmashauri waibue mradi wa kujenga Bwawa ambao utawasaidia kuwa na maji badala ya kutegemea maji ya visima. (*Makofi*)

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika jimbo la Mtera kuna vijiji viwili ambavyo vimepata matatizo ya kimsingi kama yale ya Mbozi kwamba katika tetemeko lililotokea mwaka juzi vijiji viwili vilikuwa na visima na visima vyake vikaharibika kabisa, kijiji cha Nambaku na Kijiji cha Suli na Wizara iliahidi kwamba vijiji hivi vingepatiwa maji kwanza. Mara ya kwanza waliahidi wangetoa wao wenyewe baadaye tukaambiwa *quick wing* na kwamba sasa *quick wing* imekwishafanya lakini hivyo vijiji mpaka leo na kwa kweli vina shida ya maji sana kutokana na uharibifu ambao ulitokea kwa matukio ya Mwenyezi Mungu na si kwa kupenda. Je, Waziri anaweza kunihakikishia kwamba vijiji hivyo sasa vitaingia kwenye *quick wing* na wananchi wataanza kupata maji mapema iwezekanavyo?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Samuel Malecela Mbunge wa Mtera baada ya majibu mazuri ya swali la msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri na najibu kama ifuatavyo:-

Naomba kumhakikishia kwamba hili la uchimbaji wa visima vipya au kutafuta maji katika maeneo hayo liko katika uwezo wetu na tutafuta fedha katika *quick wings* au kwa njia yoyote ile tutakayoweza. Namhakikishia kwamba mimi mwenyewe nikipata nafasi katika hizi siku tutakazokuwa hapa Bungeni nitakuwa tayari kutembelea maeneo hayo kujionea mwenyewe. Ahsante. (*Makofi*)

Na. 59

**Ukosefu wa Madaktari Bingwa kwenye Kitengo cha Neurology – Hospitali ya Bugando**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Hospitali ya Rufaa ya Bugando inahudumia wagonjwa wengi kutoka kwenye hospitali za Wilaya na Mkoa wa Mwanza, Kigoma, Shinyanga, Mara na

Kagera; na kwa kuwa, mara kwa mara kumekuwa na upungufu wa Madaktari Bingwa hususan kwenye kitengo cha *Neurology* ambapo kwa sasa yupo Daktari mmoja tu:-

(a) Je, Serikali inayo taarifa kwamba, wapo wagonjwa wanaopewa rufaa kwenda kwenye kitengo hicho ambao hukaa muda mrefu sana bila kupata matibabu?

(b) Je, Serikali inafahamu kwamba, kutokana na kukosekana kwa huduma kwenye kitengo hicho ndugu wa wenye wagonjwa wao huwahamisha wagonjwa wao na kuwapeleka kwenye hospitali binafsi na kwingineko?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'wale, pamoja na marekebisho lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Bugando ni Hospitali ya Rufaa kwa Kanda ya Ziwa iliyopo Mjini Mwanza. Kama zilivyo hospitali nyingine za Rufaa na Mikoa Hospitali ya Rufaa ya Bugando inakabiliwa na upungufu wa madaktari bingwa husasan wa '*Superspeciality*' kwa sasa Hospitali ya Bugando ina jumla ya madaktari bingwa 23 ambao nitampatia Mheshimiwa Mbunge. Aidha, hospitali haina Daktari Bingwa wa magonjwa ya mishipa *(neurologist)* kama alivyodai Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Bugando inapokea wagonjwa wengi na wa matatizo mbalimbali yakiwemo ya mishipa kutoka ndani na nje ya Mkoa wa Mwanza. Kwa kuwa hospitali haina Daktari Bingwa wa magonjwa ya mishipa; wagonjwa wa mishipa wanaotibiwa katika hospitali hiyo ni wale ambao hali zao si mbaya sana.

Aidha, kwa kuzingatia ukweli kwamba madaktari katika hospitali hiyo ni wachache, baadhi ya wagonjwa wakiwemo wagonjwa wa mishipa ambao kitaalam hali zao si mbaya sana hulazimika kusubiri ili wale wanaohitaji huduma ya haraka waweze kuhudumiwa. Hata hivyo, kutokana na asili ya magonjwa mengi ya mishipa na hatua ya ugonjwa wenyewe wagonjwa hulazimika kukaa hospitali muda mrefu hata pale Madaktari Bingwa wanapokuwa wengi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa katika kipindi cha kusubiri huduma baadhi ya ndugu wa wagonjwa huwahamisha wagonjwa wao kwenda kutibiwa katika hospitali zingine za rufaa kama vile *KCMC*, Muhimbili na hospitali nyingine za binafsi.

Mheshimiwa Spika, hili si jambo baya kwa wananchi kwenda kutafuta huduma mahali ambapo wanaamini wanaweza kuipata kwa kiwango kinachostahili. Serikali inashirikiana na hospitali binafsi katika kutoa huduma bora na kumpa nafasi mwananchi kuchagua huduma aipendayo (*Free Market System*).

Hata hivyo, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu, kuwa kuanzia mwakani hospitali ya Bugando itakuwa na daktari bingwa wa

magonjwa ya mishipa baada ya daktari aliyepelekwa masomoni Ujerumani atakapokuwa amerejea hapa nchini. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kuna upungufu wa madaktari bingwa na kwa kuwa upungufu huu unasababisha mazingira kwa baadhi ya wauguzi wasio waaminifu wasio na maadili mema kufanya vitendo vya rushwa na kwa kuwa katika utaratibu wa kawaida wa Wizara kuna Bodi za afya kuanzia zahanati, vituo vya afya, hospitali za Wilaya na Mkoa ambazo husikiliza matatizo ya wagonjwa au wasaidizi wao.

Je, Serikali inaweza ikawaambia wananchi katika hospitali ya Bugando kuna Bodi ya Afya ambayo inaweza ikasikiliza matatizo ya wagonjwa ambao iko wazi kabisa kwa kila mtu hata wale wa Busolwa, Nyang'wale au wale wa kutoka Bukoba waweze kupeleka matatizo yao kwa wazi kabisa pale Bugando wanapopata matatizo? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa Hospitali ya Rufaa ya Bugando inamilikiwa na Kanisa la Katoliki na kwa kuwa Kanisa la Katoliki lina uwezo kabisa kupata madaktari kokote duniani hasa kwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo ni Askofu Balina Askofu mahiri kabisa.

Je, Serikali haiwezi ikashirikiana na Bodi au uongozi wa Hospitali au Kanisa la Katoliki, kupata madaktari bingwa kutoka Ujerumani, China, Israel na kwingineko duniani ili kumaliza tatizo hilo? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu kwa kifupi, maswali ya nyongeza yalikuwa marefu sana.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Musalika, baada ya majibu mazuri ya Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

Hospitali ya Buganda kama zilivyo hospitali zingine zinazo Bodi za Afya ambapo pamoja na mambo mengine ni kusikiliza na kutatua matatizo ambayo wateja wetu wanafikisha pale.

Aidha, kuna masanduku ya maoni ambayo unaweza ukaweka. Wananchi wengine wanaogopa wakionekana kwenda kushtaki kwa wakubwa basi wanaona kwamba

waganga watawajua kwamba ni wao. Lakini tunayo masunduku ambayo unaweza ukaweka maoni yako halafu hatua zikachukuliwa.

Swali la pili la kushirikiana na Bodi na Kanisa, tunashirikiana nao kwa karibu sana. Nitoe taarifa tu kwamba mwezi uliopita niliongoza ujumbe ambao Askofu Balina tulikuwa naye katika nchi ya *Italy* na tulisaini mkataba ambapo tutajengewa hospitali ya kansa pale Bugando na vile vile *Vatican* watatusaidia kujenga hospitali ya watoto pale Bugando. Kwa hiyo, tunashirikiana nao kwa karibu sana. Ahsante. (*Makofi*)

Na. 60

**Ahadi ya Rais kupeleka Vifaa vya Hospitali ya Bukombe**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali wakati ikijibu swali Na. 20 kwenye Mkutano wa Bunge wa Kumi na Moja ilisema kuwa itapeleka vifaa vya hospitali kama *X-Ray* kwenye baadhi ya hospitali; na kwa kuwa Bukombe haikutajwa miongoni mwa hospitali hizo:-

(a) Je, ahadi ya Mheshimiwa Rais alipokuwa anafungua hospitali ya Wilaya ya Bukombe kwamba Serikali itapeleka mashine ya *X-Ray* na *Ultra Sound* imefikiwa wapi, au imesahaulika?

(b) Kama haijasahaulika. Je, ni lini vifaa hivyo vitapelekwa Bukombe?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mbunge wa Bukombe, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni uamuzi wa Serikali kuzipatia hospitali zote za rufaa, hospitali maalum na Hospitali za Wilaya vifaa vifuatavyo:- Mashine za *X-Ray*, *Ultra Sound*, vifaa vya upasuaji na kurekebisha mifumo ya maji na umeme.

Hadi sasa Serikali yetu kwa kushirikiana na Serikali ya Uholanzi chini ya Mradi wa *ORET* wa awamu ya kwanza ilikwishazipatia hospitali zote za Serikali isipokuwa hospitali za Wilaya mpya vifaa tajwa hapo juu.

Aidha, chini ya mradi wa *ORET* wa awamu ya pili Serikali imekwisha kamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuzipatia hospitali za Wilaya mpya nchini mashine za *X-Ray, Ultra Sound*, vifaa vya upasuaji , mifumo ya umeme na maji. Hospitali hizo ni pamoja na hospitali ya Wilaya ya Bukombe.

Mheshimiwa Spika, naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais ya kupeleka mashine ya *X-Ray* na *Ultrasound* katika Hospitali ya Wilaya ya Bukombe bado inakumbukwa na inafanyiwa kazi. Wakati tukisubiri utekelezaji wa mradi *ORATE* awamu ya pili, tutaangalia uwezekano wa kutumia fedha zilizobaki katika utekelezaji wa mradi wa *ORATE* awamu ya kwanza ili kununua vifaa tiba kwa ajili ya hospitali zenye mahitaji makubwa zaidi ikiwemo hospitali ya Wilaya ya Bukombe. Namwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Bukombe kuendelea kuvuta subira wakati suala hili linashughulikiwa kwa uzito unaostahili.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa majibu ambayo wametoa kwa kweli Mheshimiwa Rais alipoenda pale kuzindua mwaka 2007 aliahidi Januari, 2008 mashine hizo zingefika pale na kwa kuwa Serikali inaendelea kusisitiza basi niombe wahakikishe kwamba wanawasaidia wananchi hao. Baada ya shukrani hizo napenda kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mashine hizi zinaambatana sana na uwepo wa wataalam katika maeneo hayo. Je, Serikali inatuhakikishiaje pia kutuongezea wataalam wa afya katika Wilaya ya Bukombe?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama tulivyoahidi kwamba tutawapatia Bukombe mashine za *Ex-Ray* na maana hiyo kwamba wanahitaji wataalam. Napenda kuwashauri tu kwamba wakati wanasubiri hizi mashine ziende, ningewashauri Halmashauri ya Bukombe sasa iweke katika Bajeti yao mahitaji ya watumishi ambao wanawahitaji ili waweze kupata kibali Utumishi ili wakati watakapokuwa na mashine zinaenda tayari wawe wameshaajiri watumishi hawa kule kwenye Halmashauri yao.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Wilaya ya Iramba katika Hospitali ya Kiomboi tunayo hiyo mashine ya *X-Ray*, lakini tuna tatizo moja la mtaalam. Hili tatizo ni la muda mrefu na pamoja na kufuata taratibu ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri amezisema. Lakini bado mpaka sasa hatujapata mtaalam. Je Wizara inasemaje kuhusiana na tatizo hilo huko Kiomboi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, suala la wataalam kama nilivyozungumza katika jibu langu la msingi ni kwamba kuna uhaba wa watumishi. Lakini pale wanapokuwa wanapatikana huwa ni wachache.

Lakini pale tunapowapangia kwenda maeneo husika mara nyingi huwa wale wafanyakazi hawaripoti. Suala hili siyo tatizo kwamba ni Wizara ambayo haipeleki kule watalam ila ni kwamba wale watu wanaopangiwa kule hawawezi, huwa wanakataa kwenda.

Nitakachoweza kushauri kwa Mheshimiwa Mbunge ni kwamba kama ataweza kwenda ku-*lob* na kuweza kumpata huyu mtaalam, akituletea tu jina lake hata kesho sisi tutampangia kazi atakwenda kule Iramba. Kwa sababu tatizo linalotupata sisi tutapeleka watumishi lakini watumishi wenyewe hawataki kwenda kukaa kule, kwa sababu wanakosa zile motisha, wanakosa nyumba, na vitu vingine ambavyo wanaweza wakazipata huku mjini.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa matatizo wanayopata wenzetu hawa waliotangulia kuuliza maswali yanatupa sisi katika Jimbo letu la Kilwa Kaskazini kule Kipatimo na kwa kuwa Naibu Waziri ulisema kwamba uliahidi kwamba utatusaidia katika kutupa *X-Ray* na bahati mzuri kwa mbinu zetu wenyewe tumepata ile *X-Ray*. Sasa je, wataalam tutapata lini? Na *Ultrasound* ambayo ni muhimu katika magonjwa ya wananchi wetu itapatikana lini? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mpanda pamoja na wananchi wa Kilwa Kaskazini kwa kuweza kupata *X-Ray* ambayo itaongeza ufanisi wa huduma kwa wananchi wa kule Kilwa Kipatimu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema ni kwamba Serikali imeshapanga sasa kuweza kuwapatia zile Wilaya ambazo hazina vifaa hivi ikiwemo *Ultrasound*. Napenda nirudie tena sehemu ambazo hazina *Ultrasound*, basi tutawapatia *Ultrasound*, pamoja na *X-Ray* kama nilivyosema hapo mwanzo. Lakini suala la watumishi kama nilivyozungumza ni kwamba sisi bado tunajitahidi kuweza kupata hawa wataalam. Katika mpango wetu tutahakikisha kwamba wataalam wengi wanafuzu ili waweze kwenda katika maeneo ambayo hawana watalaam. Hivyo tutakapokuwa tumewapata naamini kabisa tutakuwa tunawapelekea hasa ukizingatia kwamba *X-Ray* wanazo pamoja na zile Wilaya ambazo zina vifaa hivi lakini hazina wataalam.

Na. 61

**Ujenzi wa miundombinu machimboni**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa ujenzi wa miundombinu ni hatua ya muhimu ya kuanza uchimbaji wa chuma na makaa ya mawe Wilayani Ludewa:-

(a) Je, ni lini barabara za kwenda na kutoka Liganga na Mchuchuma zitaanza kujengwa?

(b) Je, ni lini viwanja vya ndege pale Liganga na Masasi vitafufuliwa kwa shughuli za machimbo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maeneo ya Liganga na Mchuchuma katika Wilaya ya Ludewa, Mkoani Iringa, kwa sasa yanahudumiwa na barabara za Njombe-Itoni; Itoni-Mkiwu- Manda (km 221) ambazo ni barabara kuu na Mkiwu-Madaba (km.80) ambayo ni barabara ya Mkoa. Barabara hizi zote zinahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini *TANROADS,* Mkoa wa Iringa.

Kati ya mwaka 2000 hadi 2005, barabara hizo zilifanyiwa matengenezo makubwa kupitia mradi wa RUSIRM uliokuwa unafadhiliwa kwa pamoja na Nchi za Jumuiya ya Ulaya na Serikali ya Tanzania.

Hali ya barabara hizo ni nzuri na zinapitika wakati wote. Serikali imeendelea kuzifanyia matengenezo ya kawaida kila mwaka kwa kadri fedha zinavyoopatikana kuhakikisha kuwa zinapitika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu ya barabara za kwenda na kutoka Liganga na Mchuchuma ni moja ya vipengele muhimu vinavyojumuishwa katika mradi wa Uchimbaji wa Chuma na Makaa ya Mawe kwa mwekezaji yeyote atakayejitokeza.

(b) Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zilizopo zinaonyesha kwamba kiwanja cha ndege cha Liganga na kile cha Masasi kilichopo Mchuchuma si viwanja vya ndege vinavyohudumiwa na Mamlaka ya Viwanja vya ndege hapa nchini. Hata hivyo, Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itakuwa tayari kutoa ushauri wa kiufundi na kitaalamu pale ambapo atapatikana mwekezaji binafsi, kampuni au taasisi yoyote itakayokuwa tayari kuvifufua viwanja hivi kwa shughuli za machimbo au shughuli yoyote ya kiuchumi au kijamii.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Awali kwa vile tutakuwa wengi tumesoma kwenye magazeti kwamba watu wa *NDC* wamekuwa wakitangaza kwamba huenda kukaanza

kujengwa kiwanda cha kuzalisha sponji kule Liganga na kwa kuwa nina vi-*note* hapa kimoja ni cha mwaka 2006 cha aliyekuwa Waziri wa *Planning and Economy,* Mheshimiwa Dr. Juma Ngosongwa akisema kwamba barabara hiyo ya kwenda Liganga imeshaamuliwa na Serikali kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami, ninavyo hapa. Sasa je, uamuzi huo ulioamuliwa ni upi sasa kama bado mnategemea mwekezaji aje ndiyo ashughulikie barabara hizo?

Swali la pili, kwa vile barabara ya kutoka Itoni – Njombe kwenda Manda ni *trunk road* ni barabara kubwa sana na masika haifiki kule Manda. Ni *trunk road* gani hiyo ambayo isiyothaminiwa na Serikali kana kwamba kule hakuna umuhimu wa kupeleka *trunk road* mpaka Manda ibakie hivyo hivyo milele na milele licha ya umuhimu wa madini yaliyoko kule? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kuhusiana na uamuzi kwamba barabara ya kwenda kwenye haya machimbo ilishaamuliwa kwamba iwekwe kwa kiwango cha lami. Mimi nilisema hapa katika jibu la msingi kwamba na jinsi ninavyofahamu hata katika matangazo haya yanayotolewa na *NDC* kwamba *component* mojawapo ya mwekezaji yoyote anayejitokeza katika kuendeleza mradi wa machimbo haya, *component* mojawapo ni ujenzi wa barabara. Sasa kama mwekezaji atakapokuwa amejitokeza nadhani sharti moja la msingi ni kwamba lazima barabara iwe ya lami ili iweze ikapitika kwa urahisi. Kwa hiyo, bado tunaendelea kusisitiza kwamba barabara ya kwenda kwenye machimbo haya kusema kweli itakuwa imebebwa na mwekezaji yoyote ambaye atajitokeza katika kuendeleza mradi huu.

Lakini swali la pili Mheshimiwa Spika, juu ya barabara ya *trunk road* hii inayokwenda mpaka Manda, nimesema hapa katika majibu ya msingi ya kwamba Serikali inatenga fedha mara kwa mara kwa kadri inavyowezekana kuhakikisha kwamba barabara inapitika wakati wote. Sasa nataka tu nitoe ahadi hapa ya kwamba barabara hii itaendelea kuangaliwa kwa kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana na sisi tusingependa kuiacha barabara hii iwe *trunk road* kwa jina tu badala yake iendelee kuwasaidia wananchi wa Ludewa.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kabisa kwamba barabara ya kutoka Madaba, pia ni barabara nyingine muhimu sana inayoungana Madaba-Mahanje mpaka kwenye machimbo hayo ya chuma.

Kwa kuwa amesema na kukiri kwamba katika *component* zote zitakazowekwa kwenye mradi ule wa makaa ya mawe ni pamoja kuweka lami kwenye barabara hizo zinazoingia kwenye machimbo. Sasa swali langu je, Serikali itaendelea kuonyesha katika hiyo mipango yake kwamba hata kile kipande cha kutokea Madaba kuelekea Mahanje mpaka kwenye yale machimbo nacho kitawekewa msisitizo wa kuwekwa lami ili kuongeza nguvu ya barabara hizo kuingia na kutoka kwenye machimbo hayo ya makaa ya mawe?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, labda niweke wazi zaidi kwamba nilipokuwa najibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwalyosi hapa niliendelea kusisitiza suala ya kwamba *component* ya mradi ule wa Mchuchuma na Liganga unahitaji ujenzi wa barabara. Sasa iwe ni kwa lami au kwa njia nyingine yoyote lakini kuhakikisha kwamba barabara hiyo inafikika kwa uhakika. Kwa hiyo, nisingependa ieleweke moja kwa moja kwamba barabara hiyo lazima iwe ni ya lami.

Lakini baada ya kujibu hilo sasa niseme tu kwamba kipande hicho alichokieleza Mheshimiwa Mbunge kama kinakwenda kwenye hayo machimbo kwa vyovyote vile kama itakuwa imeamuliwa kwamba machimbo hayo sasa yamepata mwekezaji nayo itaangaliwa kwa upana wake ili iweze kuwa na uhakika wa kufikika huko japokuwa siyo lazima iwe ya lami.

Na. 62

**Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Songwe**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeonyesha dhamira ya kuendeleza ujenzi wa uwanja wa ndege wa Songwe – Mbeya ili uanze kutumika ifikapo Agosti, 2008:-

(a) Je, Serikali imefikia hatua zipi za ukamilishaji wa azma hiyo?

(b) Je, ni nini hasa mpango mkakati wa kuumalizia ujenzi wa uwanja huo muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwaigula Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Songwe, Mbeya, awali ulilenga kukidhi matumizi ya ndege zenye ukubwa unaolingana na *Fokker 50* ambazo ni ndege za ukubwa wa kati zenye uwezo wa kubeba abiria 50 kwa wakati mmoja. Wakati huo, kiwanja hicho kililenga kuhudumia Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, pamoja na Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, kasi ya mabadiliko ya maendeleo ya kiuchumi na mahusiano ya kikanda hasa ushirikiano baina ya nchi wanachama wa Ukanda wa Mtwara, *(Mtwara Development Corridor)* unaojumuisha nchi za Tanzania, Malawi, Msumbiji na Zambia,

yalisababisha Serikali kuamua kufanya mabadiliko ya matumizi ya uwanja ili uweze kuhudumia ndege kubwa zaidi.

Hivyo ukubwa wa kiwanja uliongezwa maradufu ili kiweze kuhudumia ndege kubwa zinazolingana na ukubwa wa *Boeing 737,* ambazo ni ndege zenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 100.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya yalilazimu kufanyika kwa marejeo ya usanifu ili uende sambamba na mahitaji mapya. *(Makofi)*

Kazi hii ya marejeo ya usanifu ilichukua muda kukamilika, ingawa haikusababisha kukwama kabisa ka shughuli za ujenzi, kwani wakati maamuzi ya mabadiliko yakichukuliwa na kutekelezwa, tayari makandarasi wa ujenzi wa mradi katika awamu ya pili walikuwa wamekwisha anza kazi.

Kutokana na mabadiliko ya ukubwa wa kiwanja, miundombinu yote ilibadilika na kuwa mikubwa sambamba na huduma inayotarajiwa kutolewa na hivyo kulazimika kuongeza na kusogeza mbele muda wa kumalizika kwa ujenzi ambao awali ulikuwa umepangwa ukamilike mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, katika awamu mbili za awali, kazi zilizokwisha fanyika ni pamoja na kuhamisha wananchi waliokuwa wamejenga katika eneo la kiwanja na kuwalipa fidia, kupata hati ya kumiliki eneo la kiwanja, ujenzi wa jengo la abiria, jengo la huduma za zimamoto, jengo la kuongozea ndege *(Control Tower),* jengo la kituo cha umeme *(Power House),* matanki ya kuhifadhia maji, matanki ya maji taka, ujenzi wa barabara ya kutua na kurukia ndege *(runway);* njia ya kutokea na kuingilia kwenye maegezo *(taxiway),* maegesho ya ndege *(apron)* pamoja na barabara ya kuingia kiwanjani *(access road)* kutoka barabara kuu itokayo Mbeya kwenda Tunduma.

Mheshimiwa Spika, awamu ya tatu ya utekelezaji ambayo kimsingi inalenga kumalizia ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Songwe kwa kuweka lami katika barabara ya kutua na kuondokea ndege pamoja na miundombinu mingine inatarajiwa kuanza kutekelezwa mwezi Julai 2008 na kukamilika baada ya kipindi cha miezi kumi na minane (18). Kwa sasa taratibu za kusaini Mikataba na Mkandarasi zimekamilika.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa ameeleza kwamba kutokana na mabadiliko mapya sasa katika uwanja huo na kwa kuwa tuliomba kwamba jengo la abiria liangaliwe upya, lisanifiwe upya, nilitaka kujua.

Je, katika mpango huu sasa mpango mpya jengo lile la abiria litapewa uzito unaotakiwa kwa sababu lile lililokuwepo mwanzo lilikuwa ni dogo na lilikuwa limesanifiwa kwa ajili ya abiria 50. Je, hilo limezingatiwa katika utaratibu huu mpya?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya uamzi ule wa kuongeza ukubwa wa kiwanja pamoja na huduma mbalimbali maradufu, kwa vyovyote vile hata hili jengo analolizungumzia Mheshimiwa Mbunge litatiliwa maanani na kuzingatiwa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuniona leo. Kwa kuwa katika ajali ambazo zimejitokeza hivi karibuni katika nchi ya Tanzania ufuatiliaji wangu unaonyesha kwamba Mbeya kumekuwa kukitokea ajali mara kwa mara. Mimi najiridhisha kuwa yawezekana ni kwa sababu ya ukosefu wa kiwanja kizuri kwa matumizi hayo, pamoja na kunyima pia fursa kwa mikoa iliyoko Kusini kwa kuwa kiwanja hicho ndicho kinahitajika kwa ajili ya ku-*link* liwanja vya Kusini. Je, Serikali haioni kwamba inahatarisha maisha ya watu walioko katika Mikoa hiyo na pamoja na wengine ambao wanakuwa wanaenda Mbeya katika shughuli mbalimbali?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka niseme kwamba ajali ni ajali kwa hiyo inapotokea ajali sasa kama imekuwa mfululizo katika eneo moja kwa kweli lazima tuchukulie tu kwamba ni ajali. Lakini kimsingi tukubaliane kwamba huduma ya kiwanja cha ndege kule Mbeya inahitajika. Sasa ndiyo maana Serikali sasa hivi imeamua kukijenga kiwanja hiki kwa ukubwa unaostahili. Lakini hiyo haimahanishi kwamba kukosekana kwa kiwanja kule ndiyo kumesababisha ajali. Hizi ajali zinaweza kutokea tu wakati wowote na mahali popote hata kama kuna kiwanja ambacho kinakidhi. Kwa hiyo, tusiyachanganye majambo haya mawili ya ajali pamoja na ukosekanaji wa huduma za viwanja. Lakini kwa sasa hivi Serikali tunachukua hizo za kuimarisha huduma za kiwanja cha ndege kule Mbeya.

Na. 63

**Fedha za Msaada toka Marekani kwa Shughuli za Maendeleo**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Marekani kupitia Rais George W. Bush imekubali kuisaidia nchi yetu kwa kuipatia fedha kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo chini ya mpango wa *Millennium Challenge Corporation (MCC):-*

(a) Je, fedha hizo zimegawanywa kwa kuzingatia misingi ipi kwa miradi iliyopendekezwa?

(b) Je, ni kiasi gani kimetolewa kwa kila mradi na kwa masharti yapi?

(c) Je, *TANROAD* itahusika vipi na miradi hiyo ya barabara ili uratibu wa kazi uoane na mipango ya nchi kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Seneta Paul Kimiti, Mbunge wa Jimbo la Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, misingi iliyozingatiwa katika kuipatia fedha miradi iliyopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kukamilika kwa upembuzi yakinifu kwa miradi husika *(feasibility study).*

(ii) Urejeshaji wa rasilimali kwa kiwango cha kuridhisha *(Economic rate of return).*

(iii) Uchangiaji wa kuridhisha katika kupunguza umaskini kama ilivyoainishwa katika MKUKUTA na kukuza uchumi.

(iv) Miongoni mwa vipaumbele vya Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Marekani imekubali kusaidia kutekeleza miradi ya Maendeleo yenye thamani ya dola za kimarekani 698 milioni. Utekelezaji huo ni kwa kipindi cha miaka mitano.

Hata hivyo, kwa wakati huu sitaweza kutaja fedha zilizotengwa kwa kila mradi, kwa sababu zabuni za ujenzi bado hazijatangazwa. Kutangaza kiwango kilichowekwa kwa kila mradi kutaondoa dhana nzima ya ushindani. Mheshimiwa Spika, sharti kubwa katika utekelezaji wa mradi iliyochaguliwa chini ya msaada huu ni uwazi na uwajibikaji.

(c) Mheshimiwa Spika, chini ya utaratibu uliowekwa pamoja na kuzingatia uzoefu katika sekta ya barabara, *TANROAD* imepewa jukumu la kusimamia ujenzi wa barabara zote zilizo chini ya msaada huu.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali madogo mawili. La kwanza, kwa kuwa tumehakikishiwa kuwa sasa fedha zimepatikana kwa kujenga barabara, mojawapo ikiwa ya Tunduma-Sumbawanga.

Kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa kipindi kirefu wamesota. Je, Waziri atakubaliana nami ya kwamba kipaumbele cha kwanza cha kupata makandarasi mmoja aanzie Sumbawanga, mmoja aanze Laela, mwingine Tunduma mwingine Ndalambo ili kasi ya ujenzi wa barabara hiyo iende sambamba na wenzetu katika maeneo mengine? La kwanza hilo.

La pili, Mheshimiwa Spika, nimemwomba Waziri anisaidie, kati ya fedha ya *MCC* karibuni bilioni 4 zimetengwa kwa ajili ya wenzetu upande wa Zanzibar na

Zanzibar kama sehemu ya Muungano ina *also* maeneo ya Pemba. Kwa kuwa wananchi wa Pemba wamekuwa kila wakati wakilalamika ya kwamba hawapewi haki yao. Je, Serikali inasema nini? Je, imetoa kidogo kwa Pemba kwa fedha hizo walizopewa za *MCC? (Makofi)*

**SPIKA:** Haya ndiyo maswali ya ki-Seneta, hayaangalii upande mmoja tu wa nchi. Yanaangalia nchi nzima ya Tanzania.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)**: Mheshimiwa Spika, kwanza kwa kuwa taratibu zote zimekwisha kamilika za hii miradi ambayo itapatiwa fedha kutoka *MCC.* Miradi mingi itatangazwa zabuni zake kwa pamoja na namwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba hivyo ambavyo anavyoona yeye ndivyo ambavyo Serikali itakavyofanya. *(Makofi)*

Lakini la pili amezungumzia suala la miradi ya Pemba. Nataka niseme tu kwamba Pemba ni kama sehemu nyingine yoyote ya Tanzania. Maendeleo yapo lakini kuna sekta ambazo zinahitaji msukumo wa ziada ikiwa ni sekta mojawapo hapo ni sekta ya barabara. Serikali kupitia *MCC* itajenga barabara tano za Pemba. *(Makofi)*

Na. 64

**Utekelezaji wa Bajeti ya Nchi**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa, muda wa utekeelezaji wa Bajeti ya nchi hauendani na majira na hali ya hewa, hali inayosababisha kuwa na muda mfupi sana wa kutumia fedha za Bajeti ya Serikali na hivyo fedha nyingi kurudishwa bila kutumika au miundombinu kuharibiwa na mvua kipindi cha masika:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa mwezi Juni, Julai na Agosti ungekuwa ni muda mzuri wa utekelezaji wa mipango ya ujenzi wa barabara badala ya kuwa muda wa kupitisha fedha za Bajeti?

(b) Kwa kuwa baada ya kupitisha Bajeti takribani miezi mitatu hupitia bila utekelezaji na kwa kuwa, fedha huwa hazijapatikana.

Je, Serikali itakubaliana nami kuwa Bajeti yetu hutekelezwa kikamilifu kwa miezi saba tu tena wakati wa masika ambao haufai kwa ujenzi wa majengo, barabara na madaraja na hivyo fedha zetu nyingi kupotea bure mara tu baada ya kutumika kwa barabara kuharibiwa na mvua?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mbunge wa Jimbo la Kalambo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mipango ya Bajeti ya Serikali ni dhana pana, ambayo inakwenda zaidi ya ujenzi. Utekelezaji huzingatia mwaka wa fedha, ambao kwa mujibu wa sheria za fedha za umma ni mzunguko unaoanzia mwezi Julai hadi Juni. *(Makofi)*

Aidha, utaratibu wa Bajeti unalitaka kila Fungu na Mtekelezaji kuandaa Mpango wa Utekelezaji *(Action Plan)*, Mpango wa Mtiririko wa Fedha *(Cash Flow Plan)*, na Mpango wa Ununuzi *(Procurement Plan)* ambayo huzingatia vipaumbele, kipindi cha utekelezaji na uzoefu.

Mheshimiwa Spika, kama mtekelezaji ataufuata utaratibu mzima wa Bajeti na kwa umakini na kwa kuzingatia kwamba shughuli za Serikali huendeshwa kwa utaratibu wa mwendelezo *(continuity)*, hakuna uwezekano wa fedha za Serikali kupotea kwa sababu ya muda wa utekelezaji wa Bajeti.

Hata hivyo, ni vyema tukafahamu kuwa ujenzi wa miradi ni sehemu tu ya mpango mzima wa utekelezaji wa Bajeti. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini mimi kwa kipindi cha miaka saba ambayo nimekuwa Bungeni ninayo *experience* ambayo inaonyesha katika Wilaya yangu kila Bajeti inapopitishwa fedha zinaanza kupatikana toka mwezi wa tisa na mwezi wa kumi.

Ukianzia toka kipindi kile ambacho Bajeti inasomwa mwezi wa sita ni kama miezi minne au mitano hivi ambayo unakuta shughuli haziendi. Je, urasimu huu haoni kwamba ni kero kwa wananchi katika majimbo yetu na katika Wilaya zetu? *(Makofi)*

Pili, hivi Serikali inashindwa nini kutengeneza mpango maalum mara makadirio ya mapato na matumizi ya serikali yanaposomwa na kupitishwa?

Basi mipango ya kupata fedha za miradi kama ya ujenzi wa barabara, ujenzi wa majumba kama mashule na vitu vingine vya Serikali, fedha zipatikane mara moja. Je, Serikali itatekeleza lini mpango huu wa kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana mapema?

Mheshimiwa Spika, Serikali haipendelei na wala haipendi kuona urasimu unaendelea. Na siku zote tunapenda kuhakikisha kwamba fedha zinakwenda sambamba na mpango uliopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Nataka nirudie kusema kwamba kama utazingatiwa mpango mzima wa utekelezaji wa miradi urasimu hautatokea.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano mwaka 2007 mwezi Juni, ambao Mheshimiwa mbunge alikuwa anazungumzia katika kipindi cha Bajeti tunachokisoma. Mwezi Juni mwaka 2007 Serikali ilitoa 8,000,000,000/= kwaajili ya utengenezaji wa barabara. Mwezi Julai mwaka 2007, Serikali ilitoa bilioni 8.8 kwa ajili ya ujenzi wa barabara, Mwezi Ogasti 2007, Serikali ilitoa bilioni 11.6 kwa ajili ya barabara. Ni kipindi hiki ambacho tunasoma Bajeti. Lakini hawa ambao wamepata pesa wametengeneza *action plan* wameiwasilisha Serikalini kwa utekelezaji kwamba tunahitaji fedha hizi na wale ambao hawakutengeneza *action plan* watakaa. Sasa Serikali ifanye nini? Lazima tutengeneze *action plan,* tutengeneze mahitaji ya fedha ili tuweze kujua kwamba katika kipindi hiki mradi huu unahitaji hiki mradi huu unahitaji hiki. Nitaomba sana, wale ambao wana mamlaka ya kusimamia na kutekeleza miradi wafanye hili ili tuweze kushirikiana katika utoaji mzima wa fedha. *(Makofi).*

**SPIKA:** Ingawa muda wa maswali umefika, lakini tuna maswali mawili mafupi ya Wizara ya Elimu ningeona ni vizuri yaweze kujibiwa leo ili tusiyaahirishe. Kwa hiyo nitatumia dakika chache. Sasa amwita muuliza swali linalofuata la Wizara ya Elimu, Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Viti Maalum.

Na. 65

**Mihula ya Shule za Sekondari**

**MHE. MARGRETH A. MKANGA** aliuliza**:-**

Kwa kuwa, mihula ya shule za sekondari zenye kidato cha kwanza hadi cha Sita inapishana, hali inayosababisha walimu wa shule hizo kushindwa kwenda likizo ipasavyo:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuunganisha mihula hiyo?

(b) Je, Serikali itakubaliana na mimi kuwa, kitendo cha mwalimu kutopata likizo ya kutosha kinaweza kuathiri utendaji wa kazi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Agnes Mkanga, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mihula ya Shule za Sekondari zenye kidato cha kwanza hadi cha sita inapishana. Serikali inaona umuhimu wa kuunganisha mihula ili kuhakikisha walimu wanapata likizo zao stahili.

Hata hivyo Serikali ililazimika kubadili mihula ili kuwapunguzia wanafunzi muda mrefu wa kusubiri matokeo ya mitihani ya kidato cha nne na kidato cha sita, ambao ulikuwa ni miezi 7 kwa kidato cha nne na miezi 15 kwa kidato cha sita. Muda huo ulipotea bure na kusababisha baadhi ya vijana kujiingiza kwenye vitendo visivyofaa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kubadili mihula umefanikiwa kwa shule zenye kidato cha kwanza hadi cha nne na zile za kidato cha tano hadi cha sita tu. Hata hivyo mpishano wa mihula umeathiri shule zenye kidato cha kwanza hadi cha sita ambapo shule hulazimika kutofungwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na hoja ya kuwa mwalimu anastahili kupata likizo kwa mujibu wa sheria na taratibu. Ili kupunguza athari za mpishano wa mihula, Wakuu wa Shule zenye kidato cha kwanza hadi cha sita wamekuwa wakijiwekea taratibu zao ambazo zinawapa fursa walimu wa shule hizo kupata likizo. Hata hivyo tatizo hilo litamalizika baada ya shule zote za bweni kuwa za kidato cha tano na sita tu.

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza ambayo ni mawili.

Kwa kuwa, Serikali imekiri kwamba mpangilio huu wa mpishano wa mihula umeathiri kidogo uwezekano wa likizo stahili kwa walimu wanaohusika. Sasa je, kwa siku hizo ambazo hawakuweza kwenda likizo kikamilifu serikali itaweza kuruhusu kufidiwa walimu hawa ili wawe na likizo ndefu?

La pili, kwa vile, Serikali imeeleza kwamba baada ya shule zote za bweni ndio kutakuwa na mpangilio huu kidogo kuweza kusaidia je, ni lini shule zote hizo za bweni zitakuwa na *A – level* kusudi walimu hawa wapate ahuweni na haki ya kuwa na stahili sahihi kabisa ya kupata likizo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Margreth Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, likizo hizo kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi ni kwamba walimu wamepewa utaratibu wao wenyewe wa kujipangia nani aende mwezi gani ili kwa utaratibu wote waweze kupata stahili zao. Kwa hiyo, Serikali haina mahala pakusema itawafidia. Na walimu ambao kwa sababu zao wenyewe kutokana na kuipenda kazi yao wamejitolea, wanazo namna ndani ya shule zao wanavyoweza kufidiana.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Utaratibu wa shule zote za bweni kuwa katika kidato cha tano na sita, utatekelezeka itakapofika mwaka 2011, asante.

Na. 66

**Mipango ya Kuongeza Idadi ya Walimu**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa, mipango ya *MMES* na *MMEM* inahitaji idadi kubwa ya walimu katika shule za sekondari na za msingi, na kwa kuwa, Serikali imejitahidi kuwa na mipango ya muda mrefu na mifupi ya kujaza nafasi zilizo wazi lakini bado upatikanaji wa walimu wa kutosha limebakia kuwa kitendawili hasa katika Mikoa ya pembezoni kama Mtwara na Lindi:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza hali halisi ilivyo katika Mkoa wa Mtwara kuhusu upatikanaji wa walimu ikielezea nafasi zilizopo na mpango halisi wa kushughulikia hali hiyo kwa shule za msingi na sekondari?

(b) Je, ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya walimu waliokataa kuripoti kwenye vituo vya Mtwara ili iwe fundisho kwa wengine?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa walimu ambao wameripoti Mtwara wakiwa wameshawekwa kwenye *payroll* ya Wizara baada ya muda mfupi wanapewa uhamisho kwenda nje ya mkoa kwa msaada wa maafisa toka Makao Makuu ya Wizara na Mikoani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi, maswali yake (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hali halisi ya upatikanaji wa Walimu wa Shule za sekondari ilivyo Mkoa wa Mtwara ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya walimu kwa shule za sekondari ni 1,565 waliopo na walimu 6,707 kwa shule za msingi. Walimu waliopo vituoni hadi tarehe 30/04/2008 ni 876 na walimu wa shule za msingi ni 4,677, hivyo upungufu wa walimu wa shule za sekondari uliopo mkoani Mtwara ni walimu 689 na upungufu katika shule za msingi ni walimu 1,530.

(a) Ili kukabiliana na upungufu huo, Wizara itaendelea kuajiri na kuwapanga walimu mkoani Mtwara katika utaratibu wa kawaida ambapo wahitimu wa Elimu ya Ualimu huajiriwa. Napenda kutoa taarifa kuwa mwaka 2008, Julai jumla ya walimu 12,692 watahitimu katika vyuo vya ualimu na Vyuo Vikuu hapa nchini.

(b) Wizara yangu haiwezi kumchukulia hatua mwalimu ambaye hajaripoti kwa kuwa anakuwa bado hajaingia mkataba na Serikali, hivyo si rahisi kumtambua alipo.

(c) Uhamisho wa walimu wa sekondari kwenda nje ya mkoa hufanywa na makao makuu ya wizara kwa kuzingatia ikama ya walimu na taratibu zilizopo. Aidha, miongoni mwa sababu zinazoweza kufanya mwalimu apewe uhamisho ni pamoja na sababu za kiafya. Mfano mwalimu anapotakiwa kuwa karibu na hospitali ya rufaa, sababu za kijamii mfano wanandoa mke au mume anapoomba kumfuata mwenza wake.

Aidha, uhamisho hufanywa baada ya mkuu wa shule husika kuithibitishia wizara uhalali wa maombi ya mwalimu huyo.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana na sehemu (a) ya majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini katika sehemu (b) na (c) ndio kwa maoni yangu naona kuna udhaifu katika majibu haya na tusipoangalia yanaweza kupelekea walimu kupata kiburi na kuunda mikakati tu mbalimbali ya kutokufika katika maeneo haya waliyopangiwa na mimi ningeomba haya yashughulikiwe kiwizara ili kuwe na msimamo mpya.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba je, Naibu Waziri yuko tayari kumwagiza Afisa Elimu wa Mkoa wa Mtwara kufanya zoezi la kuorodhesha walimu wapya wote walioko kwenye *pay role* na ambao wametoroka Mtwara kwenda sehemu nyingine ili tuweze kuwachukulia hatua za kinidhanmu, kwasababu hawa ndio wanaoongeza ujinga katika Mkoa wangu kwa kutoripoti. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mrope, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

(a) Tunapokea ushauri waketutaufanyia kazi.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda nimthibitishie kwamba orodha hii iliyopatikana imetoka katika Ofisi ya Afisa Elimu wa Mkoa wa Mtwara. Ni yeye ndiye ambaye amepokea walimu waliopangiwa katika Mkoa wa Mtwara. Kwa bahati mbaya sana naomba nimshawishi na niwashawishi Wabunge wote kwa ujumla tuboreshe mazingira na tuwe karibu kabisa na walimu hawa kuwapokea. Naomba nikiri kwamba hili ni tatizo, utaweza kumwadhibu mwalimu pale utakapokuwa naye pale ambapo hayupo kabisa hajaripoti utamwadhibu wapi? Na ninaomba niseme ni hiyari yake kwenda kufanya kazi pale au kuacha kabisa akaingia kwenye sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, nakuomba tuboreshe miundombinu, tuweke vivutio katika maeneo na tuige mfano wa wenzetu wa mkoa wa Rukwa, wameweka vivutio na kwamba suala la walimu kwa mkoa wa Rukwa sasa hivi litakuwa ni historia. Ahsante *(Makofi).*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu, kifungu gani? Kanuni, Kanuni ipi?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, natumia Kanuni ya 68 lakini inahusu Kanuni ya 39(2) na Kanuni ya 46(1). Kanuni ya 39 ipo ukurasa wa 24 na Kanuni ya 46 ipo ukurasa wa 28. Sijui kama niendelee?

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Kanuni. Kwahiyo, nilikuwa nafuatilia utekelezaji wa Kanuni zetu mpya nimeona kanuni ya 39 inakiukwa. Baadhi ya maswali yanakuwa marefu mno, kwahiyo majibu yanakuwa marefu matokeo yake yanapunguza nafasi ya kuweza kuuliza maswali na kujibu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 46(1), hii inahusu sharti la mwuliza swali kupewa majibu mapema kabla swali lake halijajibiwa ili aweze kupanga swali la kuuliza. Kwa mfano nimefanya utafiti, nimekuta mwuliza swali la kwanza leo Mheshimiwa Nyami, majibu yake aliyapata saa 3.55. Sasa hii nadhani ni ukiukaji wa kanuni. Nashuru Mheshim iwa Spika.*(Makofi).*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa *Senator* William Shellukindo. Hawa ma-*senator* ni muhimu sana kuwa nao. Ulichofanya ni kutukumbusha tu, sisi sote kuhusu Kanuni hizo mbili na kwa kuwa inatuhusu sisi sote. *(Makofi/Kicheko).*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo yafuatayo, kwanza ni wageni:-

Ninafurahi sana kwamba katika ukumbi huu leo yupo Mwakilishi wa Taifa rafiki la Sweden, ambalo ni moja ya washiriki katika Maendeleo yetu kwa hali ya juu. *Mr. Ambassador, it says very special pleasure to welcome you to Dodoma and particularly to this chamber. We know Sweden's contribution to our development since independence and even before independence. And it is a special pleasure to welcome you, thank you Sir. (Makofi).*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Haroub Masoud, nao ni wafuatao nitaomba wasimame watakapotajwa. Ndugu Hassan Shaaban, Ndugu Mwinyi Juma, wale pale. Ndugu Ally Ramadhan, Ndugu Mussa Ame, Ndugu Bonifas Ezekiel na Ndugu Thomas Buluda. Hawa wote ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Kati Unguja. Karibuni sana. Mgeni wa Mheshimiwa Sigfrid Ng'itu, Ndugu Kaspari Muya, Mwenyekiti wa *CCM* Wilaya ya Ruangwa. Yule pale, karibu sana Mwenyekiti, ahsante sana na pole kwa safari ndefu. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Lindi, ni Ndugu Abdallah Mussa Chiwawe, Mwenyekiti wa Wazazi, Mkoa wa Lindi, yule pale, karibu sana. Ndugu Benezeti, hii ni Mbawawa Mbawala? Basi imeandikwa Mbawawa, Katibnu wa Wazazi Mkoani Lindi, karibu sana *(Makofi).*

Wapo pia wanafunzi 57 pamoja na walimu wao kutoka Kata ya Zanka, Wilaya ya Bahi. Ni wale pale, karibuni sana na naona na walimu, ahsante sana. Tunawatakia mema katika kazi zenu. Nadhani upande wa kushoto nawaona vijana wangu wa sekondari ya Ilboru, naomba musimame pamoja na walimu, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, mimi ni mmoja wa walezi wa shule hiyo ndiyo maana nafurahi sana kuwaona vijana wangu wa Ilboru, karibuni sana. Tutapata nafasi ya kupiga picha ya pamoja saa 7.15. Mheshimiwa naibu Waziri, Dr. David Matayo David, akiwa pia ndiye Mbunge wa Same Magharibi na pia Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, anao wageni wake wawili ambao ni Ndugu August Lyana Kesi, Mwenyekiti wa *CCM* Wilaya ya Same na namtambulisha pia ni Meneja wake wa kampeni.

Eeh, basi huko Same Magharibi itakuwa ni vigumu sana watu kugombea kwa sababu Mwenyekiti tayari ndio Meneja wa kampeni, ahsante sana. Wabunge wenzangu wa Majimbo, huu ni mfano mzuri unamteka Mwenyekiti, halafu mambo yanakunyookea. Ameambatana na Katibu wa Jumuiya ya Wazazi wa Mkoa wa Kilimanjaro ambaye hakumtaja jina, yule pale. Ahsante mama *(Makofi/Kicheko).*

Vikao, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, ameniomba nitangaze kuwepo kwa kikao kifupi cha Kamati hiyo ya Katiba Sheria na Utawala, leo saa 5.00 asubuhi ukumbi namba 219, jengo la Utawala, Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, saa 5.00 asubuhi hii, ukumbi Namba 219.

Mheshimiwa Alhaji Mohamed Misanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, ameniomba nitangaze kuwepo kwa kikao cha Kamati ya Miundombinu,

leo tarehe 19 Juni, saa 7.00 mchana. Kikao hicho kitafanyika ukumbi namba 428, Kamati ya Miundombinu, saa 7.00 mchana ukumbi 428.

Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, ameniomba nitangaze kwamba leo mchana saa 7.00 kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo ya *PAC*, Kamati ya Hesabu za Serikali, saa 7.00 mchana Ukumbi Namba 231. Kwahiyo, *PAC* saa 7.00 Ukumbi Namba 231.

Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, ameniomba nitangaze kwamba leo saa 5.00 asubuhi katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo kwa ajili ya kukamilisha muhtasari wa kazi za Kamati kwa kipindi kilichopita. Wajumbe wote wa *POAC*, yaani Hesabu za Mashirika ya Umma, mnaombwa kuhudhuria bila kukosa ili kuikamilisha taarifa hiyo muhimu.

Mheshimiwa William Shellukindo kwa kofia yake nyingine kama Mratibu wa *Bunge Range Club*, yaani Wapiga Shabaha wa Bunge, ameniomba nitangaze kwamba wanachama wote wa *Bunge Range Club*, kutakuwa na zoezi la kulenga shabaha Jumapili hii inayokuja, tarehe 22 Juni, 2008 katika Kambi ya Makutupora Jeshi la Kujenga Taifa kuanzia saa 4.00 asubuhi.

Wabunge wote na watumishi ambao ni wanachama wa *Bunge Range Club* zoezi la kulenga shabaha Jumapili tarehe 22 Juni, 2008 saa 4.00 asubuhi *JKT* Makutupora. Wanachama wote wanaombwa wakatie sahihi kwenye orodha iliyoko kwenye *receiption* ya ukumbi wa Bunge *(Makofi).*

Hayo ndio matangazo ya leo, namwita Katibu kwa hatua inayofuata.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo, enhe, Mheshimiwa Hamad Rashid.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68(7). Kanuni ya 96 inasema kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha za Serikali. Kanuni ya 96(1) inasema: Waziri atapeleka kwa Katibu Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Serikali ya mwaka wa fedha unaohusika na nakala ya

Makadirio hayo itapelekwa na kumfikia kila Mbunge angalau siku 21 kabla ya mkutano ambao utashughulikia Makadirio hayo. Kwenye Kamati ya Fedha, vitabu vilivyokuja vilikuwa ni vitatu, kwenye Bunge lako Tukufu Waziri katika hotuba yake aliweka mezani vitabu vyote vinne. Bunge lako mpaka leo halijapata kitabu cha Namba ya Kwanza, yaani cha *Revenue,* kinyume na Kanuni hii ambayo nimeisoma. Kwa maana hiyo Bunge lako halitokuwa limetekeleza kikamilifu, kwanza matakwa ya Katiba. Lakini pia matakwa ya Kanuni hii ambayo ninaisoma hivi sasa. Tunaomba mwongozo wako hasa tukizingatia kwamba hata jana Waziri baada ya kukiri kwamba kuna mapungufu ya kitakwimu alikiri kwamba ataleta *addendum* asubuhi hii ya leo ili angalau Wabunge wawe wamepata na hadi sasa Wabunge wako hatujapata na Kanuni hii imevunjwa katika kipindi hicho. Tunaomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Mwongozo wangu nitautoa baada ya kushauriana na Serikali. Kwa hiyo, sasa tunaendelea. Aah, Mheshimiwa John Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, pia katika jambo hili la hesabu utaratibu wetu baada ya Mheshimiwa Waziri kutujibu.

**SPIKA:** Kanuni ipi Mheshimiwa Cheyo?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68(7). Mwongozo wa Spika, niendelee?

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa John Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa utaratibu wetu baada ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kutoa majibu kwa Bunge hakuna nafasi tena ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri katika utaratibu wetu, mara moja kama hivi kesho tutakwenda kupiga kura kama tunakubali au hatukubali.

Sasa mimi nilipokuwa nachangia nilimweleza Mheshimiwa Waziri kwamba, hata kwenye mizania yake takwimu zake haziendi sawasawa, kwamba huwezi kusema umepokea trilioni 2.489 kutoka kwa wafadhili halafu kwenye mizania ambayo ipo ukurasa wa 48 ukaweka trilioni 1.551 na isitoshe huwezi kutumia fedha zote ulizopata kwa mapato ya ndani halafu ukatumia karibu zote isipokuwa trilioni mbili halafu ukaweka kwamba utaweka fedha za ndani bilioni 936. Sasa hatuna utaratibu ambapo kama akinijibu nimeridhika au nisiridhike hakuna utaratibu katika Bunge hili wa kumwuliza Mheshimiwa Waziri ku-*clarify* juu ya hili. Na mimi nami napaswa kupiga kura kama nakubali au nakataa. Kwa hiyo, naomba nifafanuliwe tutafanyaje?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa John Cheyo, mimi nina hakika kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi ameyasikia hayo, yatafanyiwa marekebisho kama Miswada mingine kabla ya kupiga kura. Ahsante sana. Tunaendelea.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 96 ni katika suala hilo hilo mwendelezo wa suala la Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Kwa mujibu wa Kanuni zetu na zilivyoandikwa, tunapokaa kama Kamati ya Matumizi tunapitisha vitabu vya matumizi. Kwenye Kanuni haionyeshi mapato na Bajeti ni mapato na matumizi na mpaka sasa tunapozungumza Bunge lako limekuwa likijadili nusu ya Bajeti kwa maana ya matumizi kwa sababu hakuna hata vitabu vya mapato. Hakuna hata Mbunge mmoja kama alivyosema Kiongozi wa Upinzani Bungeni, mwenye vitabu vya mapato. Naomba utakapokuwa unatoa mwongozo wako baada ya kushauriana na Serikali uweze kutufahamisha Wabunge ni wakati gani tutapitisha mapato ya Serikali kwa sababu miaka yote tumekuwa tukipitisha matumizi tu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Basi naona umejibu mwenyewe kwa sababu nilikwishaahidi kushauriana na Serikali na nitatoa mwongozo unaolingana na ufafanuzi baada ya kushauriana na upande wa Serikali.

Katibu, endelea na *Order Paper* kwa shughuli inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2007 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2008/2009

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, orodha yangu ina wachangiaji 18 bado kuna nafasi ya watatu wanne hivi. Kwahiyo, msisikie tabu kama umepata wazo la kuchangia kwa Wizara hii ya Fedha na Uchumi, basi tunapenda tuendelee leo hadi jioni. Kwahiyo, nitawataja watano wa mwanzo ili waweze kukaa sawa. Tutaanza na Mheshimiwa Elizabeth Batenga, atafuataiwa na Mheshimiwa Clemence Lyamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kelango Malecela halafu Mheshimiwa Fred Mpendazoe na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya. Kwa mpangilio huo kwa asubuhi hii.

Namwita sasa Mheshimiwa Elizabeth Batenga na wakati huo huo Mheshimiwa Clemence Lyamba, ajiandae.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii asubuhi hii ya leo kuwa mzungumzaji wa kwanza ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Bajeti iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kukiri kosa na kueleza ukweli ulivyo ni kitendo cha uungwana lakini pia ni kitendo cha ujasiri. Kwahiyo, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa maelezo aliyoyatoa jana jioni.

Lakini pia naomba nimpe pole sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwamba watendaji wake hapa hawakuonyesha umahiri wala hawakuonyesha umakini katika kazi zao. Kwa sababu mpaka sasa hivi tungekuwa tumekwishapata marekebisho kama alivyoeleza hapo jana.

Ninaliomba Bunge lako Tukufu, lilione hili na lione kwamba watendaji wetu wa serikali hawatusaidii. Na hawatusaidii, na mimi ningesema kwamba hawakitakii mema Chama cha Mapinduzi katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, ninaomba na mimi nichangie katika Hotuba hii ya Bajeti kwa kuuangalia Mkoa wa Kagera. Mkoa wa Kagera ni kiungo cha nchi yetu, kwa nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa sababu unapakana na Uganda, Rwanda na Burundi, lakini hata Kenya kwa kutumia Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa ninafikiri kwamba, Mkoa wa Kagera ungekuwa miongoni mwa mikoa ambayo ingefaidi fursa ambazo zimo katika huu ushirikiano wa Afrika Mashariki, lakini ninapoangalia sioni ni jinsi gani, Serikali imeandaa mipango mizuri ya kuwahakikishia Wananchi wa Kagera kwamba, wanaweza wakafaidi hizi fursa. Badala yake, ninachokiona, mkoa wetu umekuwa ni soko la nchi hizo jirani na pia imekuwa badala ya miundombinu ambayo tulitarajia itaandaliwa na Serikali, sisi tunaona tunazidi kurudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa wa Kagera kukosa Uwanja wa Ndege wa uhakika, mimi sioni kama Serikali inautakia mema Mkoa huu ili uweze kufaidi hizi fursa ambazo tunafikiri tungezipata au tungenufaika na hii Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wenzangu wengi wamezungumzia kuhusu huu Uwanja wa Ndege, lakini kama hautaangaliwa ina maana kwamba, Mkoa wa Kagera unazidi kurudi nyuma, kwa sababu sidhani hata kama hao Watendaji wa Serikali wataweza kufuatilia shughuli za maendeleo zinazotendeka katika mkoa ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sioni ni Waziri gani atakayekubali kusafiri kwa gari kutoka Dar es Salaam kwenda Kagera, sioni ni mtendaji gani wa Serikali atakayekubali kwenda na ndege mpaka Mwanza, akifika Mwanza apande MV Victoria ambayo nayo inaenda kwa mwendo kwa kusua sua! Kwa hiyo, nilikuwa ninaiomba sana Serikali iliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, isingekuwa vyema nikaacha kutoa pongezi na shukrani kwa Mheshimiwa Rais, kwa kumteua Mheshimiwa Kamala kuwa Waziri wa Afrika

Mashariki, akiwa ni mwana-Kagera. Kwa hiyo, tulitarajia kwamba, basi kila njia ifanyike mtusaidie ili huyu mtoto wa Kagera, aliyepewa dhamana hiyo na watu wa Kagera waweze kunufaika katika Jumuiya hii ya Afrika Mashiriki. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba nitaje mambo ambayo yangeweza kutusaidia kuziona hizi faida au fursa nzuri tunazotarajia katika Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeshasema Uwanja wa Ndege wa Bukoba, lakini pia ningeweza kusema barabara ya kutoka Kyaka kufika Kayanga. Barabara hii ni muhimu sana itoke Kayanga iende mpaka Lusumo au maarufu sana Kwabenako; itakuwa imeuunganisha Mkoa wa Kagera na nchi za Rwanda na Burundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna barabara ya Usagara – Chato – Kyamyorwa, inaendelea kutengenezwa na tunashukuru sana, lakini kuna kipande cha barabara kutoka Bwanga kwenda Biharamulo, ambacho hakionekani kabisa kana kwamba hakipo. Ninashauri kama hakipo, basi kiwepo katika mipango ili kiweze kutengenezwa na kuifanya Barabara ya Mwanza ifike mpaka Biharamulo na hapo itakapokuwa imetengenezwa barabara ya Kagoma mpaka Lusahunga basi itakuwa imeuunga mkoa wetu na unaweza ukafikika kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nilifikiri kingetusaidia ni *EPZ*, ambayo ipo katika mpango wa kujengwa Mkoani Kagera ili na sisi tuweze kupata bidhaa za kuuza nje. Hapo awali nilisema kwamba, mkoa wetu umekuwa ni soko la bidhaa za nchi jirani. Mkoa wa Kagea, mfuko wa *cement* ya Tanga au Twiga tunaununua kwa Sh.25,000; sasa cement tunayoletewa kutoka Uganda pamoja na kwamba haina ubora unaotosha, tunaweza angalau kuinunua kwa Sh. 20,000. Kwa hiyo, wenzetu wametajirika sana maana tunakimbilia hiyo ambayo angalau ina bei nafuu. Mimi nilikuwa ninadhani kwamba na sisi tuwe na bidhaa za viwanda, ambazo tunaweza kuwauzia wenzetu. Ninaiomba Serikali iharakishe mpango wa kujenga *EPZ*, ambayo imepangwa kujengwa Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaomba kuzungumzia umeme katika Wilaya za Ngara na Biharamulo. Ngara na Biharamulo ni Wilaya kongwe tangu enzi za ukoloni na ushahidi ni majengo ya Kijerumani, ambayo yapo Biharamulo, lakini utashangaa hizi zimekuwa ni karibu Wilaya za mwisho kupatiwa umeme. Umeme waliopewa ni wa jenereta chakavu, ambazo ziling'olewa kutoka Babati na nyingine zilitoka Kondoa. Sasa hivi umeme huo ni wa matatizo, watu wanakaa mwezi mzima au wiki mbili mfululizo bila kupata umeme. Kwa hiyo, umeme huo hautusaidii kwa sababu lengo lilikuwa umeme uchochee maendeleo, sasa umeme wa jenereta hauwezi ukachochea maendeleo. Tangu umeme huo ulipowekwa miaka sita iliyopita, haujaenda hata zaidi ya kilomita mbili katika Miji ya Kabanga, Rusumo, Rulenge, Muganza, Buserere na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya yote yanastaili kupata umeme, lakini kama jenereta zenyewe haziwezi kuzalisha umeme wa kutosheleza hata sehemu ndogo, maana inavyoelekea *DCs* ndio wamewekewa ule umeme, kwa sababu hauendi mbali; miaka sita yote haujaweza kusambazwa katika maeneo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa ninaomba kwa sababu nchi yetu ni kubwa, watu wote wanastaili kupata huduma zinazostaili, basi Serikali iwe na mpango wa kugawa rasilimali hizi za Taifa kwa uwiano ulio mzuri, isionekane kwamba, baadhi ya watu wanastahili kupata umeme wa majenereta chakavu yaliyong'olewa sehemu nyingine au isionekane kwamba sehemu nyingine hawapati maji; kwa mfano, Mradi wa Maji wa *Ngara Hides*, tunashangaa umekufa hivi hivi wala hauonyesha utafufuliwa au utakuwaje na hizo mashine zenyewe haziwezi hata kusukuma maji ili watu waweze kupata maji kama kusudio la Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa ninaomba sana, kama ni mikopo ichukuliwe, watu waweze kupewa huduma ambayo itawasaidia, wasipewe vitu tu kama mapambo halafu mseme Ngara kuna umeme wakati huo umeme wala hauwafaidishi watu, hauwezi kuendesha viwanda vidogo vidogo na hauwezi kufanya shughuli zao kwa jinsi ambavyo walitarajia uwasaidie.

Mheshimiwa Spika, ninaomba hayo ili na sisi tuweze kujisikia kwamba tupo ndani ya Tanzania, maana mtu ukiwa Ngara kule wakati mwingine unaweza kusahau kama upo Tanzania kwa sababu kule ni pembeni sana, tunapakana na nchi nyingine za jirani.

Mheshimiwa Spika, naomba Uwanja wa Ndege wa Kagera utengenezwe, kwani ndicho kilio cha wananchi wa Mkoa wa Kagera. Naomba vilevile tupatiwe meli iliyo imara ili watu waweze kusafiri bila wasiwasi na waweze kufanya shughuli zao za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia tena kukushukuru sana na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu mdogo kwenye hoja iliyo mbele yetu kuhusiana na Bajeti ya 2008/2009. Kwanza kabisa, natoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, pamoja na Naibu Mawaziri na timu yao yote ya Wataalam. Pia bila kusahau, natoa pongezi nyingi kwa uongozi mzima wa *TRA* na wasaidizi wao wote, kwa kazi nzuri ya ukusanyaji wa mapato; tunaomba waongeze bidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ninaiita bajeti poa, kwa sababu ukilinganisha na bajeti nyingi zilizopita na hasa kwa kuzingatia ugumu wa hali ya uchumi Duniani na nchini kwetu, tulitegemea ingetuletea makali yasiyotegemewa, lakini kwa namna ilivyoandaliwa ni bajeti poa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi zote Duniani, zinalalamikia Serikali zao zipunguze makali ya maisha ya wananchi, kwa sababu kuna matatizo mtambuka ya upandaji wa bei

za mafuta na uhaba wa chakula. Tanzania siyo kisiwa na sisi tunakumbwa na matatizo hayo hayo, kwa hiyo ni wajibu wa Watanzania wote na hasa sisi Wabunge, tulikubali hilo kwamba, tuna changamoto ya kutoa elimu tosha kwa wananchi kwa ujumla, juu ya hali inayotukumba sisi kama sehemu ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, ninachosema wakati mgumu kama huu ni wakati wa Wabunge wote, kushikamana kwa upendo na uungwana, kuishauri Serikali namna ya kupunguza makali ya maisha ya Watanzania. Sote tunapaswa kuwa makini, kwa sababu huu wakati ni mgumu, si wakati wa kushutumiana au kubezana na zaidi siyo wakati wa kutoa kauli zinazoweza kuleta hisia za kuwachonganisha wapiga kura wetu na Wabunge. Kubwa zaidi, siyo wakati wa kutoa kauli ambazo zinaweza kuwachonganisha wananchi na Serikali yao. Kama Wabunge tulivyoungana wakati wa kujadili sakata la *Richmond* na Muswada wa Umeme, ndivyo tunapaswa tushikamane katika kuboresha bajeti hii ili tuweze kuwavusha salama Watanzania katika kipindi hiki kigumu kinachoitikisa Dunia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba tangu mwanzo nitamke rasmi kwamba, ninaiunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, pamoja na kutengewa asilimia 6.4 ya bajeti, ninaiomba Serikali ichukue hatua za haraka na makusudi, kuyafutia hatimiliki mashamba yote makubwa ambayo yametelekezwa au hayatumiki ipaswa na …

**SPIKA:** Mheshimiwa Lyamba, naomba kama unasoma hotuba yako, Kanuni haziruhusu hilo. Umeinama muda wote, nimejaribu kukuangalia naona umeinama tu, Kanuni zinatakaza kusoma hotuba; unaweza kuwa *notes* halafu unaongea, endelea.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, nitaangalia *notes* halafu nitaeleza.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninasema ninaomba Serikali ichukue hatua za haraka na za makusudi ili kutaifisha au kufuata hatimiliki za mashamba yaliyotelekezwa ili yaweze kugawiwa kwa wanavijiji wanaoyazunguka maeneo hayo. Mashamba haya yatawasaidia kukuza kilimo katika kipindi hiki kigumu cha uhaba wa chakula.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mikumi na la Kilosa, kuna maeneo makubwa ya mashamba ambayo yalikuwa ya mkonge na ambayo yametelekezwa nayo yanaangukia katika ombi hili. Mashamba haya yatawasaidia sana wakulima na wanavijiji katika maeneo hayo, kuweza kuzalisha chakula katika hali hii ngumu ya hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, linaloambatana na hilo ni suala la miundombinu. Katika Wilaya ya Kilosa na Mikumi, kuna maeneo ambayo ni maarufu katika uzalishaji wa chakula kwa wingi maeneo kama Malolo, Lumuma, Kilangari, Zombo, Ulaya na Muhenda lakini tatizo ni barabara. Ninaamini katika nchi yetu pia kuna maeneo mengine katika vijiji, ambako kuna uzalishaji mkubwa wa chakula. Ninaiomba Serikali, ichukue hatua za makusudi za kuagiza *TANROAD* wafanye ukarabati katika barabara muhimu

katika maeneo yanayozalisha chakula. Hii itasaidia kuunganisha maeneo hayo na barabara za mkoa kwa kurahisisha usafirishaji wa chakula katika maeneo yenye chakula kingi kupeleka katika maeneo ambayo yana chakula haba. Vilevile itasaidia kukabiliana na hali ngumu ya chakula hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Mikumi barabara zinazohusika katika mfumo huo ni barabara ya kutoka Mikumi – Kisanga, barabara ya kutoka Changarawe – Kilangari na barabara ya kutoka Kilosa – Lumuma. Maeneo haya yanazalisha chakula kwa wingi sana, kama barabara zingeimarishwa pamoja na madaraja sehemu ya Zombo na Ulaya, ingeleta faida kubwa ya kupunguza tatizo la chakula nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa wakulima wadogo hautakuwa kama masoko hayajaandaliwa. Kwa hiyo, iwapo Serikali itaendelea tu kukaa kungojea wafanyabiashara binafsi wajiamulie wenyewe kwenda vijijini na kujenga maghala au kuanzisha vituo vya kununua na kuuza mazao, tutakuwa kidogo hatujaongeza *speed* ya kuwakomboa wanavijiji au wakulima kwa kuuza mazao yao. Kwa hiyo, ninaishawishi Serikali, itumie kila mbinu kuwahamasisha wafanyabiashara binafsi kwa kuwapa motisha maalum, waweze kufungua vituo katika vijiji vya kununua, kuhifadhi na kuuza mazao ili iwe *centre* na soko maalum ambalo lipo moja kwa moja mbele ya wakulima wanaozalisha vyakula katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Waziri wa Fedha ametoa msamaha wa kodi za *VAT* kwenye Sekta za Kimataifa katika biashara za huduma. Ninampongeza kwa hilo, lakini nimepigwa simanzi na kusononeshwa sana kuona kwamba, hakulitazama suala la huduma zinazotolewa kwa wakulima wa miwa katika fani ya ukataji, upakiaji na usafirishaji wa miwa. Wakulima wa miwa kama alivyoeleza jana kwa kirefu jirani yangu, Mheshimiwa Ligalama, mimi sitaenda *into details.* Ninataka kusema tu kwamba, kwa sababu suala hili lilishawasilishwa katika *Tax Reform Committee* kupitia wadau wote wanaohusika, pamoja na Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo na *TRA*, imebainika wazi kwamba, kwa kweli si haki kuendelea kuwakata au kuwatoza *VAT* wakulima wa miwa katika huduma hizo nilizozitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2005/06 ndipo kodi hizi zilianza, wakati ule kulikuwa na msukumo wa *TRA* kuongeza makusanyo ya kodi. Kwa hiyo, nafikiri walifanya bila kuangalia vizuri kwamba, kwa kufanya hivyo, mkulima wa miwa analipa kodi mara mbili *(Double Taxation)*, kwa sababu kwanza *VAT* ni *registered*, lakini pili, hana namna ya ku-*claim* hii kodi kwa vile hawa wakulima ni wadogo wadogo. Kwa maana hiyo, wakilipa kodi hiyo kwa huduma ya miwa yao kwa kukata, kupakia na kusomba, watakaponunua sukari napo katika bei ile kuna *VAT*, kwa hiyo, kuna *double taxation* ambayo inawakuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wa wakulima karibu ni asilimia 50 ya miwa inayozalishwa na kutoa sukari kwa wakulima hawa ambao wanajitoa. Kwa hiyo, ni *only fair* kwa sababu *Tax Reform Committee* nayo nimeifuatilia sana, wameshakubali na kuona kwamba, kuna *basis* ya kufuta kodi hii. Kwa hakika, ilikuwa *fair* kuwarudishia au kuwafutia wakulima kodi hii ili kuwapunguzia hasara ambayo sasa hivi wanaipata.

Kilichojitokeza, wakulima wameanza kuacha kulima miwa, wameanza kuing'oa na kupanda mpunga na mahindi.  Jambo hili likiendelea, litaishia katika kupunguza uzalishaji wa sukari kwa kiasi kikubwa na tutaagiza sukari kutoka nje kwa bei za kutisha. Ninapendekeza Serikali itazame kwa makini na kuifuta kodi hiyo.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Waziri wa Fedha, kupendekeza kuondoa ushuru wa asilimia kumi kwenye mafuta ghafi ya kula; ninaungana mkono na Wabunge waliotangulia, kupinga pendekezo hili, kwa sababu litaleta vurugu katika soko la mauzo ya mafuta ya kula, kwa mbegu zinazozalishwa nchini na litaleta tu vurugu na kuhujumu soko la mafuta.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri kwa kuongeza au kupanua wigo wa malipo ya mishahara mpaka Sh.100,000 kwa wafanyakazi pasipo kutozwa kodi. Napenda kuiuliza Serikali; inawafikiriaje wastaafu wa miaka mingi, ambao kwa miaka 30 na zaidi wamekuwa wakishuhudia mishahara inapandishwa kulingana na kupanda kwa gharama za maisha, wakati wenzao wamekaa tu katika mishahara ile ile ya zamani ya Sh.21,000 na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, kupitia bajeti hii, ninaomba Serikali iwe na ubinadamu, ifikirie kuwaongezea angalau hata nusu ya *minimum wage* ile wafikie Sh.50,000. Ilani ya Uchaguzi, ukurasa wa 127 unawatambua wastaafu ambao wengi ni wazee waliotoa mchango mkubwa katika uzalishaji rasilimali katika Taifa letu.  Ukurasa wa 128, unawaita wastaafu kama ni rasilimali, lakini rasilimali hii ukiangalia Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam utashangaa, wamevaa nguo nyingine zimechanika, zina viraka, viatu kimoja kinatazama kulia na kingine kushoto, wengine kandambili na kadhalika!  Hii kwa kweli haileti heshima kwetu na kwa sababu tuliahidi katika Ilani ya Uchaguzi kwenye Ibara 500(b), ninaomba ninukuu inatamka kwamba: "Serikali itaweka utaratibu kwa wastaafu kulipwa kima cha chini kwa malipo ya pensheni, yanayozingatia mabadiliko ya kiuchumi na hali ya maisha."

Mheshimiwa Spika, hakuna kipindi kigumu cha mabadiliko ya uchumi na hali ya maisha kilichokuwepo kuliko kilichopo hivi sasa.  Ninaiomba Serikali, chonde chonde iwaangalie na kuwafikiria wastaafu. *Time is running out,* tuna muda mfupi uliobaki; tuwaongezee malipo hawa ili watusaidie kwa sala zao tuvuke 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la uchimbaji madini na kodi zake, nilitaka tu kuunga mkono wasemaji waliotangulia kwamba, tumekuwa *too lenient*, uungwana wetu na ustaarabu ndio unaotufanya tutoe misamaha mikubwa ya kodi kwa wenye migodi ya madini.  Sasa hivi lazima tugangamale kuhakikisha kwamba, tunakataa kutoa misamaha holela kwa ajili ya manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *D by D*, nilikuwa ninafikiri ni wakati umefika, tuwathamini Madiwani kwa kiasi kikubwa, kwa kuwalipa posho zinazokidhi majukumu ambayo wanayafanya.  Vilevile Viongozi wa Serikali za Vijiji hata kama ni kwa kuwalipa posho ndogo, baada ya kila miezi mitatu, iwaonyeshe kwamba, Serikali ina-

*appreciate* kazi kubwa wanayoifanya vijijini. Hawa ndio kiungo kikubwa kati ya wananchi na sisi, kwa hiyo, tuwafikirie kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, meno aliyopewa Mkaguzi Mkuu Kitaifa, yateremshwe pia wapewe Wakagazi wa Ndani. Serikali itafute namna ili Wakaguzi wa Ndani waogopwe kama ilivyokuwa zamani. Waogopwe na watendaji ambao wapo tayari kuvurunda au kuchezea mali za umma.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, wajasiriamali waliofaidi fedha za mikopo ya JK tangu zilipoanza ni wafanyabiashara wa katikati, lakini wajasiriamali waliojilenga kwenye kilimo, hawakupewa fedha za kutosha kwa kuogopa kwamba, watakuwa hawana uwezo wa kulipa. Ninaiomba Serikali itoe mwongozo kwamba, katika fedha za JK, kuwe na asilimia fulani iliyotengwa maalum kwa ajili ya wajasiriamali wanaojihusisha na shughuli za kilimo ili kuwa na *fair share* katika mchango wao kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninarudia kusema ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ANNA K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba nianze mapema kusema ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Mawaziri wote watatu na kwa sababu ninajua wote ni wasikivu na wanaopokea ushauri, watakuwa wanapokea ushauri ambao Wabunge tutautoa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wengi wamesema mengi ambayo ningependa kuyasema lakini ninaomba nijikite mahali pamoja tu. Kwamba, Serikali ninafikiri inaelewa vyema kwamba, ili Taifa lisonge mbele ni lazima mapato ya ndani ndio tuyasimamie zaidi. Mapato ya ndani yanapokuwa ni kidogo, tukitegemea mapato ya nje tunakuwa hatuna uhakika na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwenye mapato ya ndani ndio mahali ambapo nina matatizo na Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. Mapato ya ndani hatuyakamui vizuri; kuna *sources* kubwa za mapato ya ndani, ambazo tukizisimamia vizuri, tutakuwa na uhakika wa kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, ninaomba uniruhusu kabla sijaanza kuzungumza, nimnukuu mwanafalsafa mmoja wa Kigiriki, aliyekuwa anaitwa Socrates. Wengi mnaosoma vitabu mnafahamu. Siku moja alienda sokoni kwenye mkutano wa hadhara huko Ugiriki akahutubia lakini alisema neno kubwa sana. Kwa ruhusa yako, ninaomba nimnukuu, alisema hivi; ninaomba nitumie lugha aliyoitumia halafu nitatafsiri kidogo: *"Faithfulness to a cause is the most important thing in life, all great people have been considered great because they died for the causes."* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Socrates alimaanisha kwamba, watu wengi Duniani huwa wapo tayari kufa kwa ajili ya kile wanachokiamini, ambacho ni ukweli na haki.

Ninaomba niongelee ulinzi wa fedha za Watanzania, hiki ni chanzo kikubwa sana cha mapato ya ndani lakini ninaiomba Serikali ikubaliane na mimi kwamba, katika ulinzi wa fedha za Watanzania, kwa kipindi kirefu Serikali iliachia mwanya. Serikali iliachia mwanya katika kulinda fedha za Watanzania. Fedha za Watanzania ni fedha za Wananchi wa Same, ni fedha za Wananchi wa Igunga, Urambo na Kigoma Mjini. *(Makofi)*

Naomba mniangalie ninakokwenda, watu waliingiaje wakachukua fedha za *EPA* kama kweli Serikali inalinda fedha za wananchi? Hii ni *source* kubwa sana; ni pesa za mapato ya ndani ni kwamba, ulinzi ulikuwa finyu kwa muda mrefu. Iwapo tutaendelea kutokulinda fedha za ndani za wananchi kiasi hiki, kila siku tutakuwa tuna bajeti ya sungura mdogo, kwa sababu fedha nyingi zitakuwa mikononi mwa wenzetu wachache. Nilitaka kuanza kuzungumzia hapo kwenye *EPA.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi hatutaki wale Wabunge ambao tunalitetea Taifa, tuzungumze sana kwa sababu hapa Rais amesimama kidete amesema, pesa ni lazima zirudi na nina imani kwa Mtanzania yeyote anayejua maana ya Rais, atazirudisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze bila ya kuogopa kitisho cha mtu yeyote kwamba, fedha za *EPA* zisiporudishwa, hapa mahali patakuwa padogo, hapatatosha kwa sababu Wabunge wote ambao tuna nia nzuri na Serikali ya CCM, hatutakubali mapato ya ndani ya nchi yetu yawe madogo kwa sababu ya mianya kama hii. Ulinzi wa fedha za Watanzania unakuwa mdogo.

Mheshimiwa Spika, mimi sitakubali kuikana hata siku moja falsafa ya Socrates, kwa sababu na mimi nipo kama yeye. Siku ile alipohutubia pale kwenye mkutano, aliambiwa kana hiyo kauli yako; Socrates akasema sitaikana. Akaambiwa tunakupa adhabu ya kunywa sumu ufe, akanyoosha mkono akapewa sumu akanywa akafa, kuliko akane; akane nini kauli yake anayoiamini! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme sitakana kauli yangu ninayoiamini kwamba, lazima Serikali isimamie mapato ya wananchi na pesa za *EPA* zirudi ama sivyo, wananchi huko nje nyamazeni, Wabunge tutapambana na zitarudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye pesa nyingine ambazo zinachezewa, ili mjue mapato ya ndani yapo lakini yapo mikononi mwa watu wachache. Kuna bilioni 216 tangu miaka ya 1992, kwa wale ambao mnafuatilia mambo ya nchi, zilitolewa mikopo kwa ajili ya *import support.*

Nitaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajumuisha, atuambie kama bilioni 216 zimesharudi, ambazo zilitolewa zaidi ya miaka 16 zimekopwa na wenzetu wananchi wachache. Sasa ni zaidi ya miaka 16 zipo mikononi mwa watu wachache, lakini leo hii tunasema mapato ya ndani ni madogo. Mapato ya ndani jamani siyo madogo, yapo mikononi mwa wenzetu wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilisoma vyombo vya habari, Serikali ikawapa hawa watu miezi mitatu tangu Aprili wazirudishe, mwisho ni Julai. *Okay!* Tuwape hata Julai. Waziri atueleze hivi ikifika Julai hawajazirejesha bilioni 216 za Wananchi wa Same Mashariki na Kigoma Mjini; Serikali itachukua hatua gani?

Waheshimiwa Wabunge, iwapo mtakaa kimya mkiogopa vitisho, mkiacha kutetea wananchi wenu, hamuitendei haki nchi hii. Acha tusimame imara na Mbunge ambaye hatawatetea wananchi wake, ina maana hawapendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba hiki kieleweke; bilioni 216 hizi wakati Waziri ana-*wind up* atuambie zimerudi ngapi? Kama hazitarudi patakuwa padogo tena hapa. (*Makofi*)

Madhara ya tabia kama ya kuacha kundi dogo la Watanzania likamate pesa za nchi lenyewe, halafu kundi kubwa liachwe linateseka; wananchi wakufa, wanawake wanazalia barabarani madhani, makubwa yapo mawili: La kwanza, Taifa linakosa mapato ya ndani, lakini kubwa kuliko yote, Waheshimiwa Wabunge mpaangalie hapo ni kwamba, sura ya namna hii inamomonyoa imani ya Taifa kidogo kidogo, bila ya sisi wenyewe kugundua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niingie kwenye jambo lingine ambalo halina ulinzi mzuri nalo ni ulinzi wa rasilimali za nchi hii. Mapato ya ndani tunang’ang’ania mno *TRA* hapana, kuna vyanzo vikubwa ambavyo vimekosa ulinzi; eneo la Madini haina ulinzi mzuri, Mbuga zetu za Wanyama kwenye utalii hakuko sawa!

Mheshimiwa Spika, nakwambia Rais akisema leo aunde Tume ifanye kazi vizuri, hakuko sawa kwenye utalii; mapato mengi na pesa zetu nyingi zimelala huko. Mimi naomba nimuunge mkono Mheshimiwa Lazaro Nyalandu alivyozungumza, pesa nyingi zimelala huko.

Jamani naomba kuuliza hivi usiporingia rasilimali ya nchi yako utaringia nini? Leo hii kuna mfumko wa bei dunia nzima, naomba Watanzania waelewe kwamba, mfumko wa bei hauko Tanzania tu hapana; Dunia nzima kuna mfumko wa bei. Nimetoka Amerika na Waamerika nao sasa wanalia na mfumko wa bei. Nimepita Uingereza na Waingereza wanalia mfumko wa bei ni sababu moja kubwa; mwenzetu amejali na kuringia rasilimali yake, yaani Mwarabu amekwenda akakataa na mafuta yake, akapanga bei anayotaka yeye kwa ajili ya mapato yake ya ndani.

Sasa sisi tunawaaachia watu kwenye *Tanzanite* wanavyotaka na kwenye almasi zetu wanavyotaka, sidhani kama tuna ulinzi wa uhakika, tunapoteza pesa nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, kuna mifano mingine nikitoa kwa kweli inachekesha. Hebu angalieni nchi kama Kenya; *let us be fair,* hivi Kenya ina nini cha zaidi kutuzidi sisi Tanzania? Lakini Kenya mapato ya ndani bajeti ya 90% anajitegemea na sisi tukubaliane

jamani; sisi tuna rasilimali nyingi kuzidi Kenya. Kwa hiyo, kuna mahali kuna kasoro. Jamani Wabunge sisi ndiyo wa kurekebisha matatizo ya nchi hii, naomba tuungane, tusiogope vitisho bali tusimame imara; tukisimama imara Mungu atasimama na sisi tutashinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukienda Botswana, *can you imagine;* Botswana wana almasi wameilinda vizuri kwelikweli. Wana ng'ombe na wana makaa, lakini leo hii aibu sisi Tanzania hatuwezi kuisogelea Botswana. Nenda Libya kuna gesi wameiwekea sheria kali, sasa hivi Libya hatuwezi kuisogelea lakini sisi jamani Tanzania tuna matatizo gani? Hii tabia ya kuwaachia watu wachache utajiri wa nchi hii waukumbe na Watanzania wafe kwa sababu ya kutokuwa makini, mimi naomba niseme sitakana kile ninachokiamini kuwa nii ukweli na haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nieleweke ninafanya hivi kwa ajili ya Taifa langu na kwa ajili ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Nitaitetea na ninaomba nizungumze bila woga kwamba, tutapambana pesa zetu zitarudi ziingie kwenye bajeti, isipokuwa tunaomba pesa za *EPA* na zile bilioni 216 kurudi kwake sisi Wabunge tuthibitishe, hatutaki kuambiwa kwenye karatasi. Sababu inaeleweka, tunaweza tukaambiwa kwenye karatasi kumbe pesa hazikurudi, kwa hiyo, tutakuwa hatujafanya kazi tuliyotumwa na wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, iwapo hatutasimama imara, tutakuwa Taifa lisiloheshimika. Ukiona Taifa linawaachia kikundi kidogo kihodhi pesa za Watanzania na Wabunge mpo, mmechaguliwa na wananchi mnakuja mnakaa kimya; *it is wrong* ni bora msije. Tusimame imara tusiogope vitisho wala tusimwogope mtu yeyote yule, bali tuisimamie Serikali yetu ya CCM. Ugomvi wangu ni kwa wale wanaoichafua Serikali ya CCM, kwa kuhodhi pesa za Watanzania isivyo halali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana na bahati njema Spika huyu mliye naye haogopi vitisho. Tunaendelea na Mheshimiwa Fred Mpendazoe Tungu, atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Stellah M. Manyanya. *(Makofi)*

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana, kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Ninaomba nimpongeze, kwa ujasiri alioufanya siku ya jana kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Ninaomba nimnukuu Sir Churchil, kwa suala la ujasiri alilolifanya Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo. Sir Churchil alisema hivi: "Ujasiri ndiyo sifa kubwa kwa binadamu, kwa sababu ndiyo unaohakikisha uwepo wa sifa nyingi."

Nampongeza sana Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, kwa ujasiri wake wa jana na ninaamini kwamba, sifa nyingine zitakuwepo kwa Mheshimiwa Mkulo kutokana na ujasiri alioufanya kama Sir Churchil alivyosema.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nichangie katika suala la namna tunavyotumia fedha zetu baada ya kupitisha bajeti. Kwanza kabisa, naomba nizungumzie Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya Mwaka 2006/07, upande wa Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2006/07, kiasi cha fedha zaidi ya shilingi bilioni saba zilizotolewa na Serikali Kuu, zitumike kwenye Halmashauri zetu hazikutumika. Hii inamaanisha kwamba, Miradi ya Maendeleo ambayo ilikuwa imepangwa itumie hizo fedha haikutekelezwa, kwa sababu zile fedha hazikutumika katika Halmashauri hizo.

Nitazungumzia sababu mbili zilizotajwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sababu ya kwanza, ameeleza ni upungufu wa wataalamu kwenye Halmashauri na sababu ya pili amezungumzia udhaifu katika kuibua miradi.

Nia ya Serikali ya kupeleka fedha nyingi kwenye Halmashauri ni nzuri, lakini tunaona kuna matatizo; shilingi bilioni saba hazikutumika na miradi haikutekelezwa, tatizo ni wataalamu wachache.

Nitoe mfano wa Halmashauri ya Kishapu, ina upungufu wa wataalamu 344. Huu ni upungufu mkubwa na ni moja ya mfano kwamba miradi ya kule haitekelezwi na inawezekana ndio sababu ya Wilaya yetu kuwa nyuma kimaendeleo.

Sababu ya pili iliyozungumzwa ni matatizo ya kuibua miradi kwenye Halmashauri zetu. Nikitoa mfano wa Wilaya ya Kishapu ni tatizo la kuandaa mikutano ya hadhara, kwa ajili ya kuibua miradi katika Halmashauri. Uibuaji ni mgumu, kwa sababu kwa mfano katika Wilaya ya Kishapu kuna vijiji vyenye kaya 1,000, kuna vijiji vyenye kaya 800 na kuna vijiji vyenye kaya 500 na 600. Kwa kawaida, kijiji kinatakiwa kiwe na kaya 100 au 200; sasa kama kuna kijiji chenye kaya 1,000, 800 au 600; uibuaji unakuwa ni mgumu. Mtendaji wa Kijiji ataweza kutembelea kaya 1,000 kuhamasisha ili miradi iweze kuibuliwa?

Matokeo yake, fedha zinazopelekwa hazitumiki kama Ripoti ya Mkaguzi Mkuu ilivyoonyesha kwamba, kuna shilingi bilioni saba hazikutumika. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, itoe kipaumbele kupeleka watalaamu kwenye Halmashauri ambazo zina upungufu mkubwa kama Wilaya yetu ya Kishapu. Vilevile iharakishe ugawaji wa vijiji ambavyo ni vikubwa mno, kama vijiji vya Wilaya yetu ya Kishapu na kuna Kata vilevile katika Wilaya yetu ambazo ni kubwa sana, tunaomba basi Serikali iharakishe ugawaji wa Vijiji na Kata ambazo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tatizo la kuibua miradi, kama alivyoeleza Mheshimiwa Lyamba, linasababishwa na Wenyeviti wa Vitongoji, pamoja na Wenyeviti wa Vijiji kuwa hawana posho na ndiyo msingi wa uibuaji miradi na ndiyo tunawategemea wawahamasishe watu waende kwenye mikutano ya hadhara, waweze kukubaliana ni miradi gani ya kupaumbele katika vijiji hivyo. Wenyeviti wa Vitongoji hawana posho, Wenyeviti wa Vijiji hawana posho na vilevile Madiwani wetu ambao

wanasimamia Kata na kuhamasisha Kata, wanakuwa hawana posho za kutosha na mazingira yao ya kazi ni magumu. Naomba sana Serikali iliangalie hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili, Ripoti ya Mkaguzi imeonyesha katika mwaka 2006/07, Miradi ya Maendeleo yenye zaidi ya shilingi bilioni 60 ilichelewa kukamilishwa katika Halmashauri zetu. Miradi hiyo ni mingi na malengo ya Serikali yoyote hapa duniani ni kuhakikisha kwamba, wananchi wake wananufaika haraka na Miradi ya Maendeleo. Kuchelewa kutekelezwa kwa miradi hiyo, kunawavunja moyo wananchi.

Nitazungumzia sababu mbili zilizoelezwa na Mkaguzi. Ya kwanza ni kutopatikana kwa michango kutoka kwa wananchi na ya pili ni ucheleweshaji wa kutoa fedha kutoka kwa wafadhili au wahisani.

Nianze na hili la michango kutoka kwa wananchi; kumekuwa na tatizo sana, lakini tatizo kubwa ni ubovu wa utaratibu wa kupata michango kutoka kwa wananchi. Vilevile wananchi hawasomewi mapato na matumizi. Nilikuwa naomba sana, hili limezungumzwa wakati uliopita, ningeomba Serikali itueleze leo wakati Waziri anakamilisha hoja hii; wamechukua hatua gani kwa Watendaji wa Kata na Vijiji, ambao wameshindwa kusoma matumizi na mapato ya fedha za wananchi waliochangia maendeleo, kwa sababu kutokana na hiyo ndiyo wananchi wanakuwa na matatizo ya kuchangia? *(Makofi)*

Nizungumzie suala la Watendaji wa Kata na Vijiji kutokuwa na mpango wa kazi; wakiamka leo wanakwenda kukusanya michango. Hawana utaratibu kabisa. Ninachoomba, kuwepo na utaratibu na Serikali itoe Waraka kuhusu utaratibu mzuri wa michango, kwa sababu Watendaji wa Kata na Vijiji kutokuwa na mipango, ndiyo maana wamekuwa wakinyanyasa wananchi. Tumeshuhudia Wilaya ya Solwa; mama amekwenda kujifungua akiwa amewekwa rumande kwa sababu ya michango. Kwa hiyo, ninaomba sana kuwepo na utaratibu na Serikali itoe Waraka wa namna michango itakavyofanyika katika Halmashauri zetu na imechukua hatua gani kwa Watendaji hao ambao wamekuwa na ubadhirifu mkubwa wa michango.

Suala la wafadhili kuchelewa kutoa fedha ni suala linalokera wananchi na mimi nilikuwa naona Serikali ichukue hatua ya kuhakikisha tunajitegemea zaidi kuliko ile 34%. Nchi zinazoonekana kutoa ahadi na zisitoe hizo fedha; naona siyo nchi wahisani au nchi wafadhili. Hizi ni nchi hasi kwa maendeleo yetu, yaani zinavuruga maendeleo ya nchi kama alivyokiri Waziri wa Fedha kwamba, misaada kutoka kwa Wafadhili haitabiliki.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie tena Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali katika upande wa Serikali Kuu. Mtakubaliana nami na mtakubaliana na Watanzania wengi kwamba, nchi yetu ya Tanzania siyo maskini, japokuwa Watanzania wengi ni maskini. Pamoja na utajiri mkubwa tulionao, bado bajeti yetu inategemea watu kutoka nje kwa 34%. Ripoti inazungumza kwamba, pamoja na maduhuli kuongezeka kutoka trilioni 2.9 mpaka trilion 4.2 mwaka 2006/07, inaonekana kwamba, bado

mchango wake katika uchumi haukuonekana, kwa sababu fedha nyingi zilichukuliwa na wachache kama alivyoeleza Mheshimiwa Anne K. Malecela. Maoni ya Watanzania wengi tunaowawakilisha ni kwamba, Serikali ichukue hatua madhubuti juu ya ubadhirifu uliotokea. *(Makofi)*

Ubadhirifu uliotokea umeleta hasara na aibu kwa nchi yetu. Wananchi wetu wengi wanafuatilia suala hili kwa makini na Serikali inatakiwa ichukue hatua madhubuti. Nitasoma mwanafalsafa mmoja alivyosema na ninaomba ninukuu: "Unafahamu ni kitu gani kimenishangaza kuliko vyote maishani; ni kushindwa kwa matumizi ya nguvu kukupatia kitu chochote cha maana endelevu maishani, nimetambua kwamba mwisho wa yote hata husalimu amri kwa ukweli."

Serikali itueleze bayana, inachukua hatua gani kuhusu suala la ufisadi kwa fedha za *EPA?* Vilevile Waziri anapo-*wind up* atueleze fedha za *EPA* zinazorudishwa ni nani anayezirudisha?

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Tume ya Mwakyembe nayo tunaomba yatolewe.

Naomba ninukuu tena suala lifuatalo: "Unaweza kuwadanganya watu wachache wakati wote, lakini huwezi kuwadanganya watu wote wakati wote." *(Makofi)*

Lazima Serikali iwe bayana katika suala la ufisadi, litailetea tatizo Taifa letu, hali hii siyo nzuri.

Mwisho, naomba nizungumzie yafuatayo: Katika Ripoti hiyo inaonyesha vilevile kwamba, hakukuwa na usimamizi wa deni la Taifa na kwamba kulikuwa na uhafifu katika kusimamia deni la Taifa. Hii ina maana gani? Ukiangalia deni la Taifa ni 10% na ndivyo ile asilimia ya maduhuli iliongezeka kutoka 2.9 trilioni mpaka 4.2 trilioni ; zilizoongezeka ni trilioni 1.3, ambayo ni 10% ya Pato la Taifa. Fedha hizi ndizo zilizopotea kwa ubadhirifu wa aina mbalimbali. Ukiangalia 10% ya pato la deni la Taifa zilizopotea, utaona kutosimamia Deni la Taifa kikamilifu ni kitu ambacho kinaonekana kilipangwa. *(Makofi)*

Kitabu cha Waziri kinaonyesha kwamba, asilimia kumi ya ni Deni la Taifa zilizopotea ni kutokana na ubadhirifu wa aina mbalimbali. Naomba Serikali iwe makini katika suala hilo; kama tunataka nchi yetu isalimike, tunataka majibu ya kina na ya uwazi, kwa sababu ni kweli pesa zimepotea, zimerudishwa na ni ukweli kumekuwepo na ubadhirifu katika nchi yetu. Tunataka majibu kutoka Serikalini ; majibu yaliyotolewa awali yanaonekana kwamba, kama Serikali inalazimishwa kuchukua hatua juu ya ubadhirifu kwa taarifa zilizotolewa, inaonekana kama Serikali inalazimishwa. Naomba sasa Serikali iwe wazi, itueleze kwa kina, hatua ambazo inazichukua katika suala la ubadhirifu wa fedha.

Katika bajeti, naomba niipongeze Wizara moja, ambayo imeonyesha kuondokana na utegemezi; nayo ni Wizara ya Maji. Katika fedha za nje, fedha nyingi ni za mkopo na

si za kutoka kwa wahisani. Wameamua kukopa kuliko kubembeleza wahisani; huo ni mwelekeo mzuri ambao unatakiwa uigwe na Wizara nyingine. Ni vyema tukope kuliko kutegemea wahisani ambao hawatabiriki. Mimi naipongeza sana Wizara hiyo, kwa jinsi ilivyoamua kufanya hivyo na Wizara nyingine zichukue mkondo huo na ninafikiri tutafika mahali ambapo Watanzania wataona tunafanya kazi nzuri.

Tatizo lilionekana katika Halmashauri; fedha nyingi katika Sekta ya Maji hapa nchini, hazikutumika kutokana na Wataalamu wachache na uwezo mdogo wa Halmashauri. Naiomba sana Serikali, ijenge uwezo kwenye Halmashauri zetu ili ziweze kutumia fedha zinazopangwa na Serikali. Wizara yenyewe ilisema, uwezo ni mdogo kwenye Halmashauri kutumia fedha zinazopangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, nakubaliana na hoja ya bajeti. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mpendazoe na sasa nitamwita Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Umbulla na wakati huo huo Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mbunge wa Chalinze ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu. *(Makofi)*

Awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu na apewe sifa kwa kazi kubwa ambayo ametufanyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sina bajeti nyingine ya kuiunga mkono zaidi ya hii, kwa sababu ni bajeti inayotokana na Serikali tuliyoiweka madarakani. Nina nafasi ya kuichambua ili iweze kupata maboresho na hasa kuweza kupata mtazamo wa siku za usoni kutokana na maisha magumu yanayowakabili Watazania.

Mheshimiwa Spika, suala la umaskini au wananchi kupata maisha mazuri ni suala endelevu na si la siku moja, ndiyo maana kwangu siwezi kusema bajeti hii ni nzuri, kwa sababu haijaweza kukidhi mahitahi ya Watanzania katika kila nafasi yao.

Mheshimiwa Spika, pia nafasi hii niitumie mbali ya kuwapongeza walioiandaa, niwashukuru sana Wahandisi wenzangu walioko katika Sekta mbalimbali na wale *professionals* ambao wamekiri na kutambua nafasi zao katika shughuli mbalimbali, ambazo zinatakiwa zifanyike ili kuleta maendeleo ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Stephen Covey katika kitabu cha *Seven Habits of Highly Effective People* anasema hivi: “Kuna wakati binadamu analiangalia zaidi suala katika sura ya mtazamo fulani na akasahau kutoa *influence* ya kuweza kukabili lile tatizo.” Sasa hapa tumekuja na masuala ambayo ni tatizo la magonjwa yanayotukabili. Kwa nini tumeendelea kuwa na matatizo ya umaskini, hatusongi mbele? Tumefanya tafiti tukagundua wapi mapakacha yetu yanavuja, tumeyaweka mbele. Sasa badala ya ku-*concentrate* na namna ya kutibu tunaanza kufikiria nani, mtu, vitu vidogo badala ya ku-*concentrate* na *issue* ya msingi ambayo ni kuzuia ubadhirifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikirudi vilevile katika kitabu cha *Corporate Entrepreneurship* cha Bwana Paul Burns, katika duara lake la mzunguko wa shughuli au maisha kwa ujumla, anasema kwamba: "Kuna wakati unakuwa na *concept* fulani unai-*test*, baada ya kui-*test* unaangalia imefanya vipi kazi, unagundua ina tatizo ndiyo *reflection* hiyo, baadaye unafanya marekebisho." Sasa nadhani Watanzania tu-*concentrate* katika kufanya marekebisho ya pale ambapo tumeona tumekosea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kusimamia matumizi ya Serikali, halitaweza kuachwa; tutaendelea kufanya hivyo na si hivyo tu, vilevile katika suala hili linalozungumzwa la ufisadi, wale wenzetu ambao walikwenda pale Mahakamani walisema, kuna mambo ya unyatunyatu, yaani ile kuchukua kwa papo kwa papo, hayo lazima tuyafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? Nimefanya ziara Musoma nikiwa Mjumbe wa *NEC*, nimerudi pia katika Jimbo la Mbinga Magharibi na Songea Vijijini, hali ya wananchi siyo nzuri; malalamiko ni makubwa sana, wanatuuliza kila wakati maisha bora kwa kila Mtanzania yakoje? Majibu tunayo lakini hayaonekani vizuri, kwa sababu tunapozungumzia ukuaji wa uchumi, tunauzungumzia katika sura ya ujumla wake, katika uchangiaji wa watu wachache, lakini tukirudi katika *micro level* ya mtu mmoja mmoja chini, hali si nzuri na ndiyo maana lazima tuisemee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika taarifa zilizokusanywa miaka ya 96 na mpaka sasa, nadhani hakuna *data* kamili za hivi sasa. Ukiangalia makundi ambayo yamekuwa yakichangia *GDP* ya nchi hii, wengi wao ni hawa watu wadogo wadogo; wakulima na wafanyabiashara ndogo ndogo, ndiyo wengi wapo hapa chini, ni asilimia thelathini. Hawa wafanyabiashara tunaozungumzia kwamba, wanachangia *GDP* kubwa ni wachache sana na ni wale ambao wengi wao wanatoka nje, *FDIs* lakini ukija hapo katikati wanasema, hawa wajasiriamali wa kati, sana sana Wahindi wachache ambao wapo pale Dar es Salaam. Wengi kabisa Watanzania asilia wapo huku chini, tunawasaidia vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefuatilia pia tumetambua kwamba, katika Kitabu cha Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nisi-*refer* ukurasa la msingi ipo, anazungumzia kwamba; usafirishaji wa bidhaa zetu sisi nje ni mdogo; haukui vizuri, kwa nini? Kwa hiyo, ukifuatilia wajasiriamali wao wanakabiliwa na matatizo katika ngazi kuu nne; namna ya kuanza ile biashara, namna ya kuweza angalau kuihimili, namna ya kukua na kwenda katika ngazi ya Mataifa. Hizi hatua zote wanasaidiwa na nani? Hakuna *link* hapo katikati, tuna sera nzuri zipo huku juu, kuna hawa wanaolalamika wapo huku chini, lakini nani anawasaidia ili waweze kufikia, hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazo *NGOs* nyingi ambazo zingeweza kuwa ni *business development services* zikawasaidia hao, lakini *NGOs* zetu nyingi zimejikita katika masuala ambayo yana pesa ambazo zipo hapo kwa hapo. Ukienda katika suala la UKIMWI, kuna fedha zimetoka Marekani wapo wengi huko, ukienda kwenye mambo ya

haki za kiraia na rushwa wapo wengi huko, lakini sasa ukifuatilia kumwezesha huyu mtu kiuchumi unamsaidia vipi, hapo kuna *missing link*, tunaomba Serikali ifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ianzishe viatamizi vya kuatamia hao wajasiriamali. Kwa nafasi yangu kama Mbunge, nimefanya kama *prototype*; mimi mwenyewe ni kifaranga wa pale Chuo Kikuu nimeona ina-*work*. Sasa kwa sababu mimi sina fedha ya kutosha nimeshindwa nafanya kidogo kidogo, lakini kama hii *model* ingetumika, watu wengi wangeweza kupona kwa kuhamisha *knowledge* ambazo zipo katika *institution*s zetu kama *TIRDO* au maeneo mengine ambayo yanahusika na tafiti, kuwapelekea hawa wananchi ili waweze kutumia, uwezekano wa kuondoa umaskini huu mdogo mdogo upo. Tusizungumzie tu kwamba, bajeti ya kilimo ni ndogo kwa sababu imetengwa *percent* fulani wakati hata matumizi yake pengine hayana *impact* kubwa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo kidogo tu cha uyoga, kitu kidogo sana, nimefundisha kwa muda wa mwaka mmoja tu lakini unaweza kuona hata bibi mzee ameweza kuingiza Sh. 70,000 kwa mwezi. Je, kama tungeweza kuwasaidia wote wangeingiza shilingi ngapi? Kuna haja ya kutoa ruzuku, kama mtu anaweza kununua mfuko wake wa mbolea? Tuwawezeshe wananchi wetu kwa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudi kwenye rasilimali zetu kubwa zinavyotumika. Tuna tatizo kubwa la mafuta; mafuta yanapanda bei kila siku na hali hii ni kikwazo kikubwa kwa uchumi. Pamoja na kwamba ni tatizo mtambuka, lakini sisi tuna neema; juzi tumekwenda Songosongo kuna visima chungu mbovu vya gesi. Visima vile vimepatikana gesi zaidi ya ile ambayo ilikusudiwa na katika ile gesi unakuta kwamba namna ya kuitoa pale kuwafikishia watumiaji haipo, lakini hata hivyo nasema kama utafiti umeshafanyika ikaonekana kwamba kutumia gari la gesi utatumia kwa thamani moja ya nne ya bei ya sasa hivi ya mafuta, tunangoja nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini tusiwawezeshe hao *TPDC* tukasema kwamba, potelea mbali; hebu tusaidie huu mradi magari yaagizwe, kwanza hata wakianza na Wabunge hapa tayari itakuwa ni mfano mmojawapo. *Taxi* zile za mjini, sasa hivi tunakaa kila siku tunaongelea hilo hilo, wengine wanahofia kwamba, kodi hazitakusanywa za kutosha, unakusanya kodi kwa kitu ambacho tayari ni mzigo. Ile *multiplying effect* ya *impact* ya ukuaji wa uchumi iko wapi? *Why are we lazy in thinking*? Tuna matatizo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema na naishauri Serikali kwamba, tuondokane na zile *culture* za kizamani za kufanya kazi kwa kungojea mpaka fulani aseme, ili mradi tu uwe katika misingi ya ukweli, isiwe katika ile staili ya kurukia jambo, hujalifanyia utafiti wa kina mara ndiyo kama hivi inatokea mitambo Alstom kule imefungwa Mwanza, haifanyi kazi, fedha zetu zimekwenda, tukiuliza matatizo, hatutaacha kuuliza! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwamini Mungu na naamini katika yale ninayosimamia. Suala la binadamu au kumtafuta mtu, halitakuwepo maishani mwetu. Tunatakiwa

kujifunza kutokana na matatizo yetu, yawezekana kuna tuliyoyafanya kwa makusudi au tuliyoyafanya kwa bahati mbaya, lakini kimsingi tunataka kuboresha ili twende mbele.

Mheshimiwa Spika, kuna siku nilisoma gazeti, wanasema tusiamini sana magazeti. Kuna mtu mmoja nilikuwa namwamini sana katika *articles* zake, lakini nikakuta amechambua chambua mambo ya *Richmond*, nikaona kama vile sijui imekuwaje lakini sitaki kujibu kwa sababu Serikali inafanyia kazi hilo suala. Endapo kutaonekana kwamba, kuna tatizo kubwa tunalohitaji kujibu, Mungu akitupa uhai tutajibu kwa sababu bado majibu tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi katika hao wenzetu ambao wamewekeza, ni jinsi gani wana-*support* katika hizo *communities*. Ilinihuzunisha sana nilipofika Songosongo, mimi si Mbunge wa Songosongo lakini ni Mbunge wa Watanzania. Wale watu wanakaa katika mazingira magumu; kile kisiwa kimezungukwa na maji marefu, hata maboti hakuna, wana kijishule na zahanati lakini Daktari hakuna. Wale watu mpaka tukaangalia *rate* yao ya kujifungua tukaona ni ndogo, tukajiuliza kwa nini? Nikagundua huenda akinamama wengi wanakufa kiasi kwamba, sasa hata wale wanaoendelea kujifungua, wamekuwa wachache.

Kitu tulichojaribu angalau kutetea pale ilionekana kwamba, wale wawekezaji wapo tayari kumlipa hata yule Daktari ambaye ataweza kwenda kuhudumia ile hospitali; kwa nini tusiwasaidie? Naomba sana kwa sababu tumeambiwa tuongee kichaka chochote kile, basi Waziri wa Afya tunaomba awafikirie.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kuna shule ipo pale. Shule ile wamesema kwamba, wale wawekezaji wamesaidia lakini ndiyo maana tunasisitiza kuwe na mgawo maalum, usaidizi ule hauna sura ya gesi iliyopo Songosongo. Maana yake, tumekuta ile shule mabati yameshapata hata kutu, madirisha yamewekwa vijiwavu mbalimbali vidogo vidogo, halafu tunakwenda kuonyeshwa sisi makampuni matatu yamesaidia shule kama hii; hayo ni matusi jamani, Watanzania ina maana hatuoni?

Tulipouliza zaidi tukaambiwa, tunasaidia na vyoo, tumewapa umeme nyumba mia moja. Kweli kwa mtu ambaye atavuna gesi *in years* amesaidia tu vyoo, sisi tunasema kwamba, tuli-*negotiate; are we serious*? Jamani tufanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa sababu Wabunge tunapoongea maneno kama haya, yanataka nini, kutakuwa na hali ya kutuchonganisha *as if* sisi hatuwataki wawekezaji; si hivyo, tunasema tuongeze nguvu katika kuchambua na kufikia yale ambayo yanastahili kwa faida ya wote; wawekezaji na Watanzania wenye rasilimali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijatenda haki nisipousemea Mkoa wangu wa Ruvuma, Ziwa Nyasa. Waziri wa Uvuvi kweli hatujawahi kuona boti kule, tunasikia tu barabara na vitu gani, lakini nilipokwenda kwenye kikao cha mara ya mwisho nikiwa Tumbi, nilionyeshwa wagonjwa wanne wanaoumwa viuno kwa ajili ya kwenda kuvua kwenye maji marefu. Si hivyo tu, kuna watoto wamezama kwa ajili ya dhoruba. Mbona

kwenye hiyo mikakati, haionekani kwamba *investment* angalau kwenye maboti iko vipi, kwa sababu kama hawa watu unawaambia kila siku wanunue maboti, lakini tunaona kuna *Agency* zinatengeza barabara, zinasimamia umeme; kwa nini kusiwe na *Agency* ya kusimamia uvuvi, zilete maboti ili ziweze kuwafanya watu wavue na wapate matunda kwa ajili ya kuuza ikiwezekana au kuwashirikisha na Ziwa Nyasa lina mawimbi makubwa sana?

Mheshimiwa Waziri, naomba twende mara moja tukampandishe kwenye mtumbwi wa mwembe, tumfikishe mpaka kwenye maji marefu tuone kama ataweza kukaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli leo nisingependa nizungumze sana, lakini ninachoomba maisha ya Watanzania tuyaangalie kwa kina.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia hoja ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Nami naungana na wenzangu, kwa kweli kuwapongeza Wizara, pamoja na Watendaji wake wakuu. Bajeti ni nzuri, makosa madogo madogo ni ya kibinadamu lakini kwa kweli imetupa upeo wa kuelewa masuala mengi ya kiuchumi na mikakati mingi, ambayo itailetea nchi yetu maendeleo jinsi tunavyotazamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja, napenda kutoa mchango wangu katika eneo hili la kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Naunga mkono bajeti hii, kwanza kabisa, kwa sababu hii ni mara ya pili nasikiliza bajeti ya mwaka jana na mwaka huu. Imenipa moyo, kwa sababu nimeona kuna mwelekeo wa kupunguza umaskini kwa jinsi ambavyo imeweza kuainisha changamoto mbalimbali za kupunguza umaskini, kama ilivyo katika ukurasa wa 21 na 22 wa kitabu kile cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, unapoainisha changamoto na hatimaye ukaeleza ni mikakati ipi ya kuweza kukabiliana na changamoto hizi, inakupa moyo kuona kwamba, basi unaweza. Kigezo cha kupima kuona kwamba sasa tumefikia wapi, kwa sababu watu wamepigia kelele sana; kuna mikakati mbalimbali kama vile MKUKUTA, MKURABITA, MKUMBITA na kadhalika. Vitu ambavyo utekelezaji wake na *impact* yake haionekani lakini kwa hotuba hii tunaona mwanga kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Pato la Taifa pia linategemea thamani ya bidhaa tunazozalisha. Kwa hiyo, vigezo vitatu ni muhimu sana katika kuinua Pato la Taifa. Tumeyasikiliza mengi kuhusu ukusanyaji wa mapato ni namba moja, lakini vilevile uzalishaji ambao unaongeza thamani ya bidhaa tunazozalisha vilevile ni kigezo muhimu. Kwa maana hiyo, kilimo kimezungumziwa sana, tutakapozalisha kwa kuongeza thamani katika uzalishaji wetu nadhani tutaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, cha tatu ni matumizi. Inapotokea kwamba, matumizi yetu ni makubwa kuliko mapato, nadhani hatutafika mbali. Kwa hiyo, naipongeza bajeti hii na kuweka matarajio makubwa kwa siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, nina hofu kidogo; tuna vipaumbele vingi sana, kwa mfano, Sekta ya Miundombinu ilikuwa kipaumbele mwaka jana, mwaka huu ni kipaumbele na mwaka kesho huenda kikawa ni kipaumbele. Si hilo tu, tuna vipaumbele katika elimu, afya na kadhalika. Natoa ushauri kwamba ni wakati muafaka sasa, tuweze kuweka vipaumbele vichache kwa kipindi maalum na tuvipe kipaumbele kweli kweli, tuvitekeleze hadi tutakapoona *impact* yake imeweza kuonekana. Kwa mfano, kama ni Sekta ya Miundombinu, tuweze kutenga fedha za kutosha ili tujenge barabara kwa kipindi hicho ili mwaka unaofuata wa bajeti, kipaumbele chetu kiwe tofauti. Hapo tunaweza kupima *impact.* Lakini kama tutakuwa na vipaumbele vingi si rahisi kuona utekelezaji wa jambo moja kikamilifu. Tutakuwa tuna vipaumbele vingi kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni lile la kuwawezesha wananchi kiuchumi. Wakati tunahimiza watu waweze kukopa yale mamilioni ya JK, tumehimiza wananchi na jamii kujiunga na *SACCOS*, ama kwenda kukopa katika vyombo vya fedha, lakini tunasahau kwamba, wananchi wetu wametofautiana katika uelewa. Nadhani ni muhimu Wizara itenge bajeti ya kutosha, kuwapa elimu ya uelewa wananchi, kwa sababu si kila mtu ana uwezo wa kubuni mradi haraka haraka na kuchukua fedha na kurejesha. Nadhani hizi fedha, mpaka sasa hivi zinaishia mikononi mwa wale ambao wanaweza kufanya kazi kwa bidii, haraka haraka na kuweza kurejesha mikopo hii na wale ambao ni walengwa halisi, wanaostahili kupokea mikopo, wanabaki kusubiri kuangalia wenzao wanafanya nini na awamu inawapita.

Mheshimiwa Spika, ili kila mwananchi aweze kunufaika, nafikiri Wizara itenge fedha za kutosha kuwaelimisha ili waweze kuibua miradi na si miradi tu, iwe miradi ambayo inaliletea Taifa letu pato, kwa sababu kuna miradi yenye tija. Kwa mfano, tuhamasishe miradi kama ya ufugaji nyuki. Jana tumesikia miradi ya kulima miwa, ambayo vilevile siyo tu inampatia mwananchi pato, bali pia inaongeza Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia kwa kifupi sana kwa sababu wenzangu wamezungumzia ni la kilimo. Natoka Mkoa wa Manyara na Manyara tunalima sana mahindi katika msimu mzuri. Mkulima mmoja aliniambia ghala langu lina magunia elfu moja, debe moja la mahindi ni Sh. 1,000, kwa hiyo gunia ni Sh. 6,000, akasema hata hainunui mgolole, sisi huko kwetu tunavaa migolole. Akasema tupelekeni basi huko Mtwara kwenye korosho, ambako Serikali ndiyo inaipa kipaumbele sana, kwa sababu hatuoni Serikali ikitupa motisha sisi wakulima wa mahindi. Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri sana, tukaangalia ni maeneo gani na watu wanafanya shughuli ipi ya kuzalisha mazao ya kilimo ili nao tuwape motisha walime kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sasa hivi Serikali imeondoa ushuru wa mahindi, lakini wafanyabiashara hawapati hata mahindi huko kwenye soko la dunia, kwa sababu

wanachozalisha wanakitumia. Sisi hatuna haja ya kuagiza mahindi kutoka nje, tuna uwezo wa kulima na kuzalisha chakula chetu cha kutosha ili tuweze kujitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka kuchangia lakini limeshaongelewa sana ni eneo la madini. Nitakachoweza kusema tu, wenzangu wameeleza kwa takwimu lakini mapato tunayopata kutokana na madini katika nchi yetu, tusingeweza kuwa hata na haja ya kutamka neno MKUKUTA ama MKURABITA na *terms* nyingine zile zote. Pato la Taifa linalotokana na madini ni kubwa, tatizo ni kwamba, nadhani linafuata mkondo mwingine ambao haueleweki. Kama Pato la Taifa litajumuisha madini na sekta nyingine za utalii na kadhalika, hatutakuwa na haja ya kuzungumzia MKUKUTA miaka tunayokwenda. Kwa hiyo, nadhani ni wakati muafaka, kuweka bayana mapato yanayotokana na madini na utalii na mambo mengine ili kwa pamoja, Pato la Taifa linapokuwa kubwa, ndipo maendeleo yatakapoweza ku-*trickle down* kwa wananchi na hatimaye basi umaskini kufutika polepole. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia kidogo upande wa wafugaji na Sekta ya Mifugo. Nasikitishwa sana na jinsi Serikali yetu inavyowaweka pembeni wafugaji na mifugo yao. Sote tunaelewa umuhimu wa mifugo katika nchi yetu, wamezungumzia watu wengi sana na sisi tunaelewa, lakini katika bajeti sijaona kabisa mikakati yoyote ambayo imewekwa ili hatimaye nao wafugaji waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wakati mmoja Rais alitembelea Mkoa wa Manyara akasema, nadhani sasa ni wakati muafaka kuhakikisha mifugo inanenepa na wafugaji wananenepa, haina maana ya kunenepesha mifugo wakati wafugaji wenyewe wanakondeana. Wafugaji wengi wanakuwa *displaced* kwa mfano, kulikuwa na tatizo katika eneo fulani la vilima vitatu, wafugaji kwa mara ya kwanza, waka-*resist* kuhamishwa kwa ajili ya uwekezaji. Lakini baadaye kwa sababu Serikali ime-*resist*, wengine wanakutana na wanaokwenda na mifugo yao huko Handeni, sasa ni lini wafugaji watatulia?

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali haiweki mipango madhubuti ya kuhakikisha kwamba, wafugaji nao wanastahili kutulia katika maeneo yao na wao wakafuga mifugo yao wakanufaika, wakaona kama nchi hii ni ya kwao? Naomba bajeti hii pia iitupie macho Wizara ya Mifugo na zaidi ihakikisha kwamba, wafugaji wananufaika, wanatulia na wanapewa heshima wanayostahili badala ya kila mara kuleta malalamiko kwamba, wamevamia eneo hili wanafukuzwa hapa na pale.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijatenda haki kama sitowazungumzia wanawake ambao wamenileta hapa Bungeni. Hivi sasa sisi tupo asilimia thelathini kwa uwakilishi wa Bungeni hapa na tunapigania iwe asilimi hamsini. Naomba nitoe wito kwa wanawake wenzangu kwamba, sisi na wingi wetu na wingi tunaotaka kuupata, tuangalie tumewafanyia nini Wanawake wa Tanzania na tutafanya nini kwa ajili ya kuleta maendeleo. Kwa kifupi naomba kuachia hapo.

Mheshimiwa Spika, vilevile natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu sisi sote ni Madiwani katika Halmashauri zetu na miradi mingi ambayo inawasaidia wanawake kuwapunguzia adha, inaweza kufadhiliwa na fedha zinazopitishwa kwenye Halmashauri. Sisi Waheshimiwa Wabunge Wanawake, tusipohudhuria kwenye Halmashauri zetu, tukahakikisha tunatenga fedha za kutosha kwa ajili ya miradi ya kuwapunguzia uzito wa shughuli wanawake kama miradi ya maji na kadhalika, basi tutakuwa hatujatenda haki kuwasaidia wanawake wa Tanzania. Naomba tuhudhurie vikao hivyo na hasa vya kupitisha bajeti na tuelewe ni miradi ipi ambayo inawanufaisha wanawake ili tuwapunguzie uzito wa shughuli wanazofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna vifo vingi sana vya wanawake wajawazito nchi nzima na kifo kisicho cha lazima kinasikitisha sana na kwa kweli ni unyanyasaji na ukatili wa aina yake. Utafiti unaonyesha kwamba, mwanamke mmoja anafariki kutokana na tatizo hilo kila baada ya saa moja. Hili linasikitisha na sijui Serikali katika hili limeji-*commit* vipi kupunguza vifo hivi.

Naiomba Serikali iweke bajeti ya kutosha katika maeneo kama hayo, kwa sababu hivyo vifo si vya lazima ni kama kifo kinachotokana na njaa, kile si cha lazima ni cha uzembe; kama hutafanya kazi kwa bidii, basi utakufa kwa njaa; lakini hiki ni kifo ambacho tunaweza kukizuia. Sasa ni wakati muafaka, Serikali iongeze kwa wingi idadi ya wakunga walio na sifa na waliofundishwa, wahudumu wa afya na vifaa vya zahanati katika vijiji vyetu ili kuondokana na tatizo hili katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, kuwe na *free kid delivery*; hili lilikuwepo zamani, suala lipo katika sheria, imekwenda nadhani katika mkondo huo huo wa ufisadi na rushwa likafutika. Sasa tunaomba Serikali ilirudishe, nina hakika kwamba, tatizo hili litaweza kupungua. Serikali pia ihakikishe kwamba, barabara zile zinazopitisha magari ya wagonjwa ziwe zinapitika. Hili ni tatizo kubwa sana, sijui kama wenzangu wataliunga mkono lakini utafiti umeonyesha kabisa ni tatizo la nchi?

Kwa hiyo, sasa ni wakati muafaka, bajeti itengwe ili iweze kushughulikia na kulifutilia mbali tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na haya machache tu ya kuchangia. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti yetu ya mwaka 2008/09.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Waziri na Naibu Mawaziri wake, Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu, Kamishna Mkuu wa *TRA*, Naibu Kamishna wa *TRA*, ndugu yangu Luoga, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kukusanya mapato ya kuleta tija katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisiwasahau pia wafanyakazi wa *TRA*. Kazi wanayoifanya ni kubwa, wanajitahidi lakini pia katika kuwapongeza, kwa sababu wao wakati wote ndio

wanakutana na wafanyabiashara, wao ndio wanaokaa kwenye deski au meza ya kujadiliana na mfanyabiashara ambaye anastahili kulipa kodi kulingana na biashara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa ngazi ya chini kwa upande wa *TRA*, nao pia wanastahili kupewa motisha na vifuta jasho kwa kazi kubwa wanayoifanya, kwani hapa tulipo leo kila Mbunge akisimama anaipongeza *TRA* kwa ukusanyaji mkubwa wa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuondokane na dhana ya wafanyakazi kila mwaka wanafanya vizuri, wanajadiliana ukadiriaji wa kodi, ambapo hatuna utamaduni wa mfanyabiashara kujikadiria mwenyewe. Kazi hiyo inabidi ifanywe na mfanyabiashara, pamoja na mfanyakazi lakini motisha wanayopata hailingani na kazi wanayoifanya. Tuondokane na dhana ya kuwapa shukrani au kuwapa zawadi za kofia au fulana kila mwaka kama ndiyo pongezi kwa kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, mapato yanayokusanywa ni mengi, lakini matumizi nayo ni mengi. Imefikia mahali kinachoingia ni kikubwa lakini kinachotoka ni kikubwa kwa maana hatuna uangalizi mzuri wa matumizi ya mapato tunayoyapata.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la kilimo. Asilimia sita iliyotengwa kwa ajili ya kilimo, haijamkomboa mwananchi. Leo hii, tukitaka ukombozi wa kilimo au mapinduzi ya kilimo tunayoyataja hapa kila kukicha, lazima tukubali kwamba mkombozi wa kilimo anayeitwa jembe la mkono, amekwisha kufa. Wakulima sasa wanastahili kupata matrekta kwa sababu ndiyo yatakayowakoa wananchi kwenye sekta ya kilimo. Jembe la mkono limepitwa na wakati, jembe la mkono linakatisha tamaa, jembe la mkono ndilo lililotufikisha hapa tulipo, kila kukicha nchi inapata uhaba wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa ifikirie kumkomboa mwananchi. Wananchi walio wengi vijijini ni wakulima. Mtazamo wa Serikali kwenye kilimo ni wa kubahatisha. Serikali itazame jambo hili kwani ni hatari na wananchi wanakatishwa tamaa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la Serikali kuondoa ushuru wa asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya kula. Ninapata mashaka sana kuhusu suala hili. Ni kweli kuna punguzo la takriban milioni kama 762 katika pato kwa hiyo ni asilimia 10. Mtazamo wa bajeti hii ni kumkomboa mlaji kwa maana ya mwananchi lakini kwa mtazamo wangu asilimia hizi 10 zilizopunguzwa kwa mafuta ghafi ya kula moja kwa moja atakayefaidika na punguzo hili, ni wafanyabiashara wa viwanda vya mafuta ya kula, hili halina ubishi. Mwananchi ataona kama kafaidika na bei atakayoikuta ambayo ina unafuu wa mafuta ya kula lakini faida kubwa ni ya hao wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mashaka makubwa na imani yangu inaniambia kwamba wafanyabiashara wa viwanda vya mafuta ya kula, wameweka mkono wao kwenye hii *ten percent.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wasipoliangalia suala, hili tutarudi kule kule kwenye migongano ya kila kukicha ya kujadili nani kafanya hivi, huyu kashiriki vipi, hatimaye Taifa letu hili kuliingiza kwenye matatizo kila kukicha kama hapa tulipo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la Madiwani. Madiwani ndiyo wasaidizi wetu kule Majimboni. Madiwani wana hali mbaya sana. Hawana vyanzo vyovyote mifukoni mwao. Mbunge ukifanya ziara ndiyo Diwani akusubiri uongozane naye kufanya ziara kwenye Kata na Vijiji. Madiwani wanapata mtihani wa kuulizwa na wananchi ulikuwa wapi, tulikuwa hatukuoni, kwa nini umekuja kipindi Mbunge naye amekuja lakini majibu ya maswali yale Serikali inayo, tuwasaidie vyombo vya usafiri Madiwani wetu. Tuwakopesha vyombo vya usafiri Madiwani, tunasita nini kuwakopesha vyombo hivyo vya usafiri? Mbona huko wakubwa wanakopeshana na fedha hazirudi? Hali hii ni ya hatari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Madiwani sasa wanakatishwa tamaa. Kuna wengine wanakopeshwa mpaka wanakufa hawajalipa. Kuna wengine wakishakopa kurudisha ni matatizo, wanakiuka mpaka mikataba lakini leo kuwakopesha hao Madiwani wanaoifanya kazi ya Serikali na wanaowatumikia wananchi vijijini, wanaona ugumu kabisa. Waoneeni huruma Madiwani maana na wao wanastahili kama walivyo watumishi wengine au kama wawakilishi wengine wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie wawekezaji. Kwa kweli baadhi ya wawekezaji wanakatisha tamaa. Wawekezaji wengine hawaitakii mema nchi yetu. Nitoe mfano au nataka nieleze jambo moja kwenye Mbuga ya Mikumi. Mikumi *Lodge* ilikuwa inamilikiwa na mfanyabiashara aliyekuwa anaiendesha kwa shughuli za biashara lakini kwa sababu ambazo hatuzijui na ningeiomba Serikali ituambie jambo hili, ikafikia kipindi, yule mfanyabiashara kwa matatizo aliyokuwa ameyafanya pale, Serikali ikasitisha mkataba na yeye lakini katika kusitisha ule mkataba, yule mwekezaji alikwenda Mahakamani. Baada ya kwenda Mahakamani kwamba amesitishiwa mkataba kimakosa, alidai fidia takriban milioni 300 ili aweze kuondoka pale.

Mheshimiwa Spika, Serikali wakati inasita kumlipa zile shilingi milioni 300, katika hali ya kusikitisha, hatumjui ni nani, ni yule mwekezaji, ni watumishi au ni mtu mwingine yeyote, ile Mikumi *Lodge* iliunguzwa kwa hujuma, mpaka dakika hii yamebaki ni magofu pale na Serikali haiwezi kuiendeleza kwa njia yoyote ile na hivi ninavyozungumza, yule mwekezaji anaidai Serikali zaidi ya milioni 900.

Mheshimiwa Spika, sasa nashindwa kuelewa, Serikali inajiandaa kumlipa zaidi ya milioni 900 yule mwekezaji au Serikali inaamua kuitengeneza ile Hoteli ianze kuingiza mapato ya Taifa? Mpaka dakika hii, nashindwa kuelewa, miaka inakwenda, majumba yale ni magofu, Serikali inakosa mapato, mwekezaji huyo yupo. Serikali nataka itueleze

kitu gani kipo pale kati ya Serikali na yule mwekezaji ambaye alifanya jambo lisilokuwa la msingi kwa kuliletea hasara Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali kupitia Shirika la Nyumba la Taifa kwa kujenga maghorofa mawili pale Chalinze. Maghorofa yale na bahati nzuri tumewapa kiwanja kikubwa, naiomba Serikali kupitia Shirika la Nyumba la Taifa, iendelee kuongeza maghorofa mengine ili dhamira yangu ya kutaka Chalinze iwe Wilaya ibaki pale pale. Hata Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo, lakini atakuwa anasikia maombi yangu yabaki pale pale, mji ule sasa unakua.

Mheshimiwa Spika, lakini wapo ambao walikuwa wanaona yale maghorofa hayatapata wapangaji. Ndugu zangu Wasukuma na Wanyamwezi walikuwa wanasema pale atakaa nani?

Mheshimiwa Spika, lakini ninataka nikuhakikishie, yale maghorofa sasa…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, jihadhari, unataja makabila mazito kidogo hapo. *(Kicheko)*

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Lakini ndiyo hao ambao walikuwa wanasema atakaa nani, Wakwere tangu lini wanaweza kukaa kwenye maghorofa, nataka nikuhakikishie, majengo yale sasa yamejaa, wapangaji wengine wamekosa yale. Kwa maana hiyo, bado tunahitaji majengo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, imenitengea milioni 57 kwa ajili ya kununua vifaa vya upasuaji kwenye Kituo cha Afya cha Chalinze. Naishukuru sana kwani nitaondokana na hali ya wale wagonjwa niliyokuwa nikilalamikia wakipata ajali na akinamama na watoto kuwapeleka Tumbi. Hali ile itakuwa imeondoka kwani Serikali ya Japan nayo imetupatia *dollar* 75,000 za kuweza kujenga jengo la upasuaji na vifaa vitakuwa vimepatikana Serikalini baada ya kutoa hizo milioni 57.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, sisi Wabunge ni wawakilishi wa wananchi. Wananchi wanatutegemea sana tunapokuwepo hapa na sisi tunapotoa mawazo yetu na tunapoishauri Serikali, tunaomba nayo Serikali itupe majibu yenye uhakika ili wananchi wetu wapate imani ya uwakilishi wao hapa Bungeni. Kwa sababu wanapopata majibu ya uhakika, ni njia nzuri na sisi ya kuwawakilisha wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya bajeti hii ya Serikali, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ramadhani Maneno, nakushukuru. Namwita sasa Mheshimiwa Mwinchoum Msomi atafuatiwa na Mheshimiwa Maria Hewa, ajiandae Mheshimiwa Bujiku Sakila.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutoa shukrani kwako kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia bajeti yetu ya Serikali ya mwaka 2008/2009. Pia napongeza uongozi wa Wizara ya Fedha kwa jinsi walivyoandaa hotuba hii nzuri na yenye matumaini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, alikuja kwenye ufunguzi wa barabara yetu ya Kilwa. Katika ufunguzi wa barabara ile, alitoa mapendekezo. Aliwaambia watu wa *TANROAD* kwa maana ya Wizara ya Miundombinu kwamba barabara ya kutoka Kilwa inaanzia bandarini hadi Rangitatu lakini aliwaagiza wafanye utaratibu wa kuweza kuunganisha barabara ile kutoka Rangitatu iweze kufika Kongowe kama kilomita moja na nusu au mbili kwa wastani.

Mheshimiwa Spika, ninaomba agizo la Mheshimiwa Rais, lizingatiwe. Nimeangalia kwenye vitabu hivi wala sikuona hilo. Naiomba sana Wizara ya Fedha katika fedha zake ziweze kukaa pembeni ili waweze kuweka heshima ya Mheshimiwa Rais kwa sababu jambo hili amelisema mbele ya halaiki ya watu na inapendeza kama litatekelezwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mradi wa maji ambao mara kwa mara tangu mwaka juzi, mwaka jana umekuwa ukitajwa kwenye Bunge lako Tukufu. Mradi wa kutoka Kimbiji na mradi wa Maji wa Kisarawe *II* ambao ni matarajio na ndiyo njia sahihi ya kuweza kuwakomboa wananchi wa Wilaya ya Temeke lakini mradi huu, nimetazama vitabuni sijauona kama umetengewa fedha au la. Ni mradi mkubwa, kuna wafadhili wameweza kufadhili mambo ya awali huko nyuma, naiomba Serikali iuangalie kwa sababu ni matarajio kwa wana Temeke, si Jimbo la Kigamboni tu bali ni Wilaya nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo la kisera kwenye shule. Kwenye Jimbo langu tumebahatika kujenga hosteli tano. Hosteli hizo zilipata maeneo makubwa na kwa bahati mbaya ziko maeneo ya shamba lakini sera ya Wizara ya Elimu inasema wao hawahusiki na ujenzi wa *fence* kwa maana ya uzio. Sasa kwa mazingira ya hosteli hizi zilivyo, moja ina ekari 20, nyingine ekari 50, nyingine 18 na kadhalika, ni kubwa mno, Halmashauri yetu haiwezi kujenga *fence.* Pili sera inakataa, inaachiwa Kamati ya shule iweze kujenga. Naomba Serikali kwa kupitia Bunge lako Tukufu, itazame sera hizi, ibadilishe kwenye mazingira ambayo ni magumu kama haya niliyoyaeleza, Serikali isaidie na kutoa kibali cha kuweza kujenga angalau uzio kwanza. Tuna matatizo kule hasa siku za mvua nyingi kwa maana ya masika hata wanyama wakali wanafika, ni hatari kwa wanafunzi wetu na matukio mbalimbali ya sasa ya kupotea kwa watoto yamekuwa mengi.

Mheshimiwa Spika, niingie kwenye suala la uvuvi. Nina malalamiko mengi sana kwenye ofisi yangu kutoka kwa wavuvi wa Jimbo la Kigamboni lakini wavuvi wa Tanzania kwa ujumla wana matatizo. Mvuvi mmoja yeye anatakiwa awe na leseni, chombo kiwe na leseni akivua pweza awe na leseni, akivua kamba awe na leseni, akivua samaki wa aina nyingine yoyote awe na leseni, jamani tutafika kweli? Mvuvi huyu kwa nini anafanyiwa hivi wakati mwindaji ana leseni moja. Naomba suala hili liangaliwe kwa

sababu ni hatari na tunamkandamiza Mtanzania. Tunataka mapato lakini tutazame mapato hayo yana tija gani kwa wenzetu Watanzania! Ni hatari na kwa kweli linapigiwa kelele kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, daraja la Kigamboni, nasikitika sana. Mwenzangu Mheshimiwa Shah hapa bajeti ya mwaka jana alisema yeye atagoma kula lakini kama unavyoniona nikigoma kula siku mbili sijui nitakuwaje, watu wataninyooshea vidole, watasema anao huyu, kumbe nimegoma kula. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ndugu zetu wa *NSSF* wamelifanyia kazi hili wakapata mfadhili ambaye ni Serikali ya Uholanzi. Yale aliyozungumza Mheshimiwa Raynald Mrope na Jimbo la Kigamboni yameingia, tumepata mfadhili *NSSF* wamehangaika kila kitu lakini Serikali haikuunga mkono. Naiomba sana Serikali ilitazame daraja la Kigamboni kwa macho mia mia, hii *reverse gear* sasa tuiache.

Mheshimiwa Spika, daraja la Kigamboni ni ukombozi kwanza kwa uchumi wa Serikali yetu. Pili, daraja lenyewe kwa mfano kwenye uchambuzi wa *NSSF* linajilipa. Wamesema baada ya miaka 10 fedha itarudi, sasa kigugumizi kiko wapi ndugu zangu? Baada ya miaka kumi wanasema fedha zote zitarudi, Serikali tunasita nini?

Mheshimiwa Spika, ninaomba mliangalie suala hili na ikiwezekana kwenye majibu ya Mheshimiwa Waziri aje na jibu la uhakika la ukombozi kwa Watanzania na wana Kigamboni kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuweka kwenye bajeti kuisaidia *TIB* lakini naomba kutoa rai, benki hii izame kwenye Mikoa minne ile inayozalisha kwa wingi chakula kwa maana ya Mikoa ya Iringa, Ruvuma, Mbeya na Rukwa. Tujitose kwanza kule kwenye hii Mikoa kwanza ili iwe mfano, wazalishe chakula kwa wingi, hatimaye kiweze kushuka bei badala ya kilimo cha sasa cha kusubiri mvua ya masika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ukiacha Mikoa minne hiyo au wa tano Morogoro pia fedha hizi zijitose kwenye Jeshi letu la Kujenga Taifa JKT. Tuzipeleke fedha huko, vijana wetu walime kwa mfano ili kuwakomboa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *solar power* lilipewa msamaha wa kodi mwaka jana lakini bado bei za *solar power plate,* ni mbaya sana. Hili ni jambo muhimu kwa Watanzania hasa watu wanaoishi vijijini na hali ya umeme ambayo kwa sasa si nzuri, ni jambo la kutegemewa. Naiomba Serikali iangalie bei ya *solar power plate*. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pale feri tuna msongamano. Mara kwa mara, nimekuwa nikisema kuwa msongamano huu unasababishwa na kuwa na *gati* moja upande mmoja na *gati* ya pili upande wa pili. Pantoni ikitoka huku kwenda upande wa pili haiwezi kuegesha, inamsubiri mwenzake aondoke. Naiomba Serikali iongezee fedha Wizara ya Miundombinu ili tujenge *gati* pale angalau ziwe mbili pantoni ikitoka huku iende ikashushe watu na magari moja kwa moja badala ya kungojeana. Hili ni jambo muhimu,

Kigamboni inakua na uchumi pia utakua, wawekezaji wa sekta ya utalii wapo, tuna uhakika fedha hizo zitarudi bila mashaka yoyote. Nyie wenyewe ni mashihidi mnaona mchango wa kivuko cha Kigamboni jinsi unavyotoka. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la barabara ya kutoka Feri hadi Pembamnazi. Barabara hii tukiitengeneza kwa kiwango cha lami, Serikali itakuwa na uhakika wa kupata mapato ya kutosha kwa sababu kuna wawekezaji wengi wa sekta ya utalii, watajenga mahoteli ya kisasa kwenye fukwe ya Kigamboni. Ninaiomba Serikali itoe kipaumbele kwa barabara hii ya Feri – Pembamnazi, imaliziwe kujengwa kwa kiwango cha lami ili tuweze kuongeza mapato ya nchi yetu kutokana na sekta ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna deni kwa Serikali, kuna mradi wa kupitisha umeme wa *grid* ya Taifa ambao unazikumba Kata tano katika Jimbo langu, kata za Vijibweni, Mbagala, Mbagala Kuu, Charambe na kadhalika. Fidia kwa wananchi zimeshalipwa ili kupisha mradi huu wa *grid* ya Taifa shilingi bilioni sita takriban bado bilioni moja Serikali haijawalipa wananchi. Vilio vimekuwa vikubwa, ni kweli ndugu tunazikimbia ofisi zetu, naomba Serikali ijitahidi kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dar es Salaam, tunaiomba Serikali muitengee Wizara ya TAMISEMI fedha ili Mkoa wa Dar es Salaam uweze kupanuka zaidi. Kuna miundo ya Kipolisi sasa hivi imegawiwa kwa Mikoa mitatu ya Kipolisi, iungeni mkono Serikali muweze kuanzisha Mikoa mitatu vile vile ya Mkoa wa Dar es Salaam kwa sababu *population* ya Dar es Salaam imekuwa kubwa sana. Naomba mliangalie suala hilo kwa kuongeza Mikoa kwa misingi hiyo iliyokwishaanza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia mrahaba kutokana na maliasili ya bahari, tunaomba sana Wizara ya Fedha ilifikirie suala hili mara mbili. Wenzetu wanafaidika na madini yao ya dhahabu, almasi na kadhalika, wanapata mrahaba, kwa nini Dar es Salaam rasilimali yetu ya bahari hamtaki kutupa mrahaba? Liangalieni suala hili mzipatie mrahaba Halmashauri zetu tano za Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na ushauri pia wa njia mbadala kwa ajili ya kwenda Kigamboni, tuanzishieni pale *overhead trains* tupite juu twende pale baharini huku daraja kama linasuasua tuweze kupita. *Overhead trains,* tafadhali Serikali naomba hili mlizingatie.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la matatizo kwenye Jeshi la Polisi, wapo wachache sana kuweza kuwahudumia Watanzania. Ninaomba Serikali ichukue hatua tuanzishe *community enforcement*, tuchukue watu kutoka kwenye Halmashauri zetu zote za Tanzania, tuwapeleke Chuo cha Polisi, wasimamie kazi nyingine zinazofanywa na Polisi ili Polisi wakafanye kazi zao muhimu za *traffic* na *community enforcement.* Naomba Serikali iangalie Halmashauri hazina uwezo, wachukueni watu kwenye kila Halmashauri kuweza kufanya kazi zingine za Polisi, nina hakika Jeshi la Polisi litaunga mkono kuwapa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu malipo ya pensheni ya wanasiasa. Kuna baadhi ya wanasiasa wamesahaulika, ninaomba waongozwe kwenye pensheni hizo za wanasiasa nao wafaidike na malipo hayo ili kulinda hadhi zao.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo kubwa sana la Bandari ya Zanzibar. Naiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuisaidia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kujenga *Container Terminal.* Kule kuna matatizo makubwa, makontena kujazana na mahali pa kuyaweka hakuna. Naomba waiangalie Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama Mheshimiwa Rais alivyosema, tuitazame nayo kiuchumi ikiwezekana tuwasaidie wajenge *Container Terminal*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya gesi, naiomba Serikali izidishe kasi, hali ya bei ya mafuta sasa hivi ni mbaya sana imefika mahali sasa wananchi wameanza kuchanganyikiwa. Gesi tunayo, watu tunao na *Alhamdulilah*, tumewahi kuwapeleka China kujifunza. Sasa badala ya kusema maneno mengi, badala ya kutueleza mengineyo, tunaomba wataalam hao waanze kazi, vyombo viletwe ili gesi ianze kutumika kwa ajili ya matumizi ya magari ili kuwakomboa Watanzania kutokana na bei kubwa ya mafuta. Mwenyezi Mungu ametujalia rasilimali hii tunayo, nina hakika kwamba inawezekana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchimbaji wa makaa ya mawe. Naiomba Serikali ijikite huko kupata nishati mbadala. Tuanzie kupeleka miundombinu, tunapochelewa ndugu zangu gharama za maisha zinapanda. Leo badala ya kujenga kwa shilingi 1,000, tukija kujenga miaka mitano ijayo tutajenga kwa shilingi 10,000. Naiomba Serikali iangalie kuanzia kuchimba makaa ya mawe kwa kuanza kupeleka miundombinu katika sehemu zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naona inatosha, kabla sijagongewa kengele ya pili, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hotuba ya bajeti hii kwa asilimia mia, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwinchoum Msomi ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa Maria Hewa atafuatiwa na ninayekadiria kuwa msemaji wa mwisho ambaye atakuwa ni Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila kwa mchana huu.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwanza kwa kunipa nafasi hii niongee mawili/matatu kuhusu bajeti na mwelekeo wetu wa uchumi katika nchi yetu yenye amani na utulivu, Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niendelee kuishukuru Wizara kwa maana ya kumpongeza Waziri na Manaibu wake kwa kuileta bajeti hii ambayo nadhani, siyo kwamba nadhani, ni kweli tu kwamba imeungwa na itaendelea kuungwa mkono nadhani na Watanzania wengi kwa sababu ina mwelekeo wa kumkomboa mwananchi ambaye yuko katika hali ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze moja kwa moja kuongelea suala zima la viwanda. Ninaliongelea hili kwa makusudi mazima lakini nina nia njema ya kuzungumzia suala la ajira ambazo zimo katika kitabu chetu cha Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba tunahitaji kuajiri watumishi wangapi katika miaka yetu mitano.

Mheshimiwa Spika, katika mawazo yangu kati ya moja ya sekta ambazo ninaziwazia ambazo zingeweza kabisa kuwa na ajira lukuku, kuwaweka vijana wetu wanaotangatanga ovyo, akina mama ambao nao wanataka ajira, ni maeneo ya viwanda. Tufike mahali Wizara husika ijue kabisa, Serikali labda nizungumze kwa ujumla hivi tuna viwanda vingapi ambavyo viko hai na viwanda vingapi vinahitaji kufufuliwa na je, tutahitaji viwanda vingapi vipya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kanda ya Ziwa, juzi liliulizwa swali kuhusu Kiwanda cha Sementi na Mabati na Mheshimiwa Limbu. Tukaambiwa tangu mwaka 1973, kitu kama hicho kulikuwa na azma ya kuweka Kiwanda Mwanza kwa maana ya uwakilishi wa Kanda ya Ziwa. Mwaka 1970 mpaka leo 2008, Serikali iko kimya. Hivi kweli tuna nia njema na ukanda huu? Nadhani ni kutokana na upole wetu au na ukimya wetu, sielew,i lakini naogopa kuendelea.

Mheshimiwa Spika, katika hili mmoja amezungumza leo humu anasema wananunua sementi Uganda inafika mahali wanabeba hata na mifuko yetu ya Simba kwa maana ya uthamani wa sementi yetu wanaweka humo, wana *seal*, wanatuuzia, hivi kweli sisi Kanda ya Ziwa hatutaki maendeleo?

Mheshimiwa Spika, tunaomba kabisa, hii kauli kuanzia sasa au katika bajeti kama sio hii lakini nadhani ni hii maana Wabunge wengi wanaongelea vyanzo vipya vya mapato, hebu suala hili lifikiriwe hata kwa kutuwekea msingi tu tujue kwamba sasa kiwanda kinaanza ili tupate vifaa hivi ili tuweze na sisi kutoka mahali tulipo.

Mheshimiwa Spika, ninapoongelea malighafi, eti wanasema ni mbali kutoka huko mpaka Mwanza, hivi mbona barabara tumeboresha, tunasema katika miaka hii mitano Tanzania itakuwa na lami tupu, hivi hamuwezi kuvisafirisha malighafi hizi tu? Viko mbali, umbali gani, mbali ni mbinguni jamani, lakini duniani humu kila kitu kiko karibu.

Mheshimiwa Spika, naomba Kanda ya Ziwa tuungane jamani, tukubaliane kabisa, Serikali itufikirie sasa maana tumevumilia vya kutosha toka mwaka 1970 mpaka leo mwaka 2008. Sasa bajeti kama sio hii kwa bajeti zijazo, hiki Kiwanda kijengwe. Watu wa Kanda ya Ziwa, ni wapenzi wa maendeleo. Kama ni kusafirishwa kwa barabara, kama ni kusafirishwa kwa njia ya maji, sisi bahati nzuri tuna kila kitu, ukitaka kwa meli vinakuja, ukitaka kwa reli vinakuja, ukitaka kwa anga vinakuja, shida ni nini?

Mheshimiwa Spika, katika hili, kwa kweli naomba kabisa Serikali ituwazie kuleta Kiwanda hiki Kanda ya Ziwa. Mbona tuna kiwanda cha bia? Sisi Kanda ya Ziwa tuna malighafi zote zinazotengeneza bia? Huwa haziletwi kweli kwa kusafirishwa? Ninaomba hili lisiwe agenda leteni Kiwanda Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Subiri kidogo. Waheshimiwa Wabunge, kuna mtu mmoja aliyeko kwenye *gallery*, anapiga makofi. Ni marufuku na hairuhusiwi. Ninyi mnaotusikiliza, mnatakiwa kusikiliza tu sio kuchangia. Ahsante, endelea Mheshimiwa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, sikusikia, wanaotoka Mwanza nadhani wamekubaliana na mimi kwa yale matangazo ya asubuhi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninapenda niliongelee katika suala zima la viwanda, ni suala la Kiwanda cha Ngozi ambacho kiko pale Mwanza. Yale majengo ukiyaona yako kwenye *standard* ya msemo wako, ni mazuri na yanakidhi kila kitu lakini Kiwanda kile sasa kiko *dormant*. Hivi pale wangeajiriwa akina mama lishe wangu wangapi kutoka Mkoa wa Mwanza au hata wa kutoka Mikoa mingine? Kiwanda kiko pale, majengo mazuri yana kila kitu ni nini kimetokea?

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara husika au Serikali itembelee huko ili ione suala hili ninalolizungumza jamani, tunabakiza magofu lakini yangefufuka kulingana na vyanzo vya mapato vinavyoongelewa humu Bungeni, tungeweza kufufua Kiwanda hicho na mambo yangeweza kujipa tu kulingana na hali halisi, vitu vipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, niombe kama Wizara haijatembelea, hebu ijaribu kutembelea, itashawishika tu kukifufua Kiwanda hiki cha Mwanza ambacho kina-*deal* na masuala ya ngozi ili kusudi ajira hizi zinazoongelewa, Serikali iweze kuzikidhi na akinamama wangu waweze kupata ajira katika Kiwanda hicho.

Mheshimiwa Spika, *finally* katika suala zima la viwanda, bajeti inapozungumzia suala zima la viwanda, hebu tukubaliane basi kwamba viwanda vidogo vidogo ni muhimu sana, wengi wamezungumzia katika Bunge hili. Tukubaliane viwanda vidogo vidogo na vyenyewe viwekwe katika mlolongo mzima wa kuweza kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania kwa sababu wataweza kutengeneza *juice* za nanasi. Geita kule tunazalisha nanasi za kutosha Tanzania nzima. Watu wa Kanda ya Ziwa wanalima miwa, wanaweza wakatengeneza *juice* ya miwa na ninyi ambao hamlimi miwa ukiacha Morogoro lakini Tabora na kuendelea kote kule mkapata *juice* hiyo. Tunapoongelea suala zima la kumwinua Mtanzania kutokana na bajeti zetu ambazo tunaziweka, tuwazie suala la kufufua viwanda.

Mheshimiwa Spika, niende haraka haraka sana kuzungumzia suala la elimu. Hivi tunaposema, Tanzania Elimu ya Msingi, ni bure maana yake nini? Mbona tunadaiwa madawati, mbona tunadaiwa vitabu, tunadaiwa penseli na tunadaiwa kuchangia hata chaki? Hebu tuitafakari kauli hii, kama kweli Elimu ya Msingi ni bure tusidaiwe dawati, tusidaiwe daftari, tusidaiwe chaki ili iwe kweli ya bure. Neno bure maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la mifugo hasa hasa ng’ombe. Ng’ombe, kwa miezi tisa akizaliwa mtamba ana uwezo wa kubeba mimba na kuzaa lakini wapi wafugaji hawa hatuwaandalii maeneo yao, matokeo yake tunawaweka katika maisha ya kuhamahama tu. Wanakuwa wazururaji badala ya

kukaa na kutulia na kuijenga nchi yao hii. Tunakwenda tu mpaka mwisho tumefika mpaka Njombe nako huko sisi wafugaji tunafukuzwa, hivi ni kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, kila watu wanapokaa kwenye maeneo yao wanapaswa kuwa na utulivu kulingana na mazingira yao, mwishowe mnatulazimisha kujifunza mazingira ambayo si sahihi kwa jinsi tulivyolelewa.

Mheshimiwa Spika, naomba jamani katika hili, Serikali iwafikirie kwa undani zaidi hawa wafugaji, hivi watatulia vipi? Watatulia vipi, malambo wanayo, majosho wanayo na ruzuku katika madawa yao wanafikiriwaje ili waweze kutulia hawa wafugaji?

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu uwanja wa ndege Mwanza. Tumepewa shillingi bilioni moja na Kigoma. Hivi kweli, hivi mnatugawia ngapi na Kigoma mnawagawia ngapi? Hivi mkitupa nusu kwa nusu, Mwanza tunyamaze, si mnatugonganisha ninyi? Tupeni iliyo halali yetu lakini bilioni moja kwa Mwanza na Kigoma sio sawa.

Mheshimiwa Spika, tangu mimi ninakua, naanza kujua kupanda ndege, nakuta *label* juu ya nyumba kwamba sasa unatua uwanja wa Mwanza, hayo majengo yaliyopo ni halali hapo Mwanza? Hiyo bilioni moja ya ku-*share* na Kigoma itajenga na majengo kweli? Naomba fumueni bajeti hapo tupeni bajeti ya kutosha. Naomba mtupe fedha ya kutosha ili tubadilishe majengo yale.

Mheshimiwa Spika, ni aibu, majengo yale kuwepo pale Mwanza na wewe huwa unafika Mheshimiwa Spika, ni aibu, ni aibu, narudia mara mbili, mara tatu. Leteni pesa ya kutosha, fumua bajeti uliyoiweka hiyo, utuongezee na sisi walau zifike bilioni 8 au 10 basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia kuhusu Madiwani. Bila ya Madiwani, Wabunge humu tunatuna tu lakini Madiwani ndio wanaotuwezesha kurudi jamani. Tuwapeni na wenyewe haki yao, wote waliozungumza acha wazungumze na wamezungumza iliyo kweli tu. Madiwani ndio roho zetu, kweli niwaambieni, Wabunge mkubali msikubali, mimi nimetokana na Udiwani, najua. Tukubali kuwaenzi Madiwani na sisi ili watoke mahali walipo walau wapate hata basi kuongezwa posho yao jamani.

Mheshimiwa Spika, mwisho *fifty fifty*. Lisemwalo lipo na kama halipo…? Mbona akinamama hamsemi? Lisemwalo lipo, kama halipo…?

**AKINA MAMA:** Linakuja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Linakuja, si ni lazima lije?

**AKINA MAMA:** Eeeee!

**MHE. MARIA I. HEWA:** *Fifty fifty* lazima ijipe. Kama haitakuwa *fifty fifty* lakini hata mtoto akizaliwa anaanza kukaa, anatambaa, anasimama na baadaye anafanya nini, anatembea, iko siku *fifty fifty* itatembea.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, nipende tu kusisitiza kwa vile kengele haijalia, niombe kumuunga mkono Mheshimiwa Mkulo.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maria Hewa, kutoka Kanda hiyo hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Bujiku Sakila.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii.

Kwanza kabisa, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri na watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa hotuba nzuri waliyoitoa. Nawapongeza sana. Kwanza, ni wageni sana, wengine wametoka Ulinzi, wengine sijui wametoka kule na wengine wametoka Wizara ya Kazi. Wamejitahidi sana na sio kazi ndogo.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi kwa Waziri na wenzake wa Wizara ya Fedha na Uchumi, napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine kwa kuipongeza *TRA*, wale ambao wamefanya tukae hapa kwa sababu bila ya kazi yao ya kukusanya fedha, nadhani hatungekuwa hapa. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja lakini vile vile namuunga mkono Mama Hewa kwa kuomba viwanda Mwanza.

Mheshimiwa Spika, mengi yameshasemwa na sio rahisi kuyarudia yote. Waheshimiwa Madiwani yameshasemwa na mimi naunga mkono lakini mimi naomba nianzie kwenye hoja au bajeti ya maji.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya maji. Tumeambiwa kwamba imepunguzwa na sababu iliyotolewa ni kwamba mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Shinyanga umekamilika, mimi naamini haujakamilika. Kazi ambayo nafahamu imekamilika ni ya kutandazwa mabomba. Lengo la mradi huo sio kutandaza mabomba kutoka Ziwa Victoria kupeleka Shinyanga, lengo ni kuwapatia maji watu wa Shinyanga, Kahama, wa Mwamashimba, ambayo ni sehemu ya Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, kauli hiyo ya Serikali, inashtua kidogo kwa sababu Mwamashimba tulishapata mradi kama huo kutoka sehemu moja inayoitwa Bunere. Mabomba yalitandazwa yakafika mpaka Mnalo miaka ya 1970 kama kilomita 27 hivi, mpaka leo mabomba hayo yapo na watu hawajaona maji yakitoka katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri anaposema kwamba fedha imepunguzwa kwa sababu mradi umekamilika, inashtua kidogo. Naamini sehemu kubwa ya kutandaza mabomba ndio imeisha lakini ule mradi bado haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, nilifikiri kama fedha ya wafadhili iliyokuwa inatandaza mabomba ndiyo iliyokuwa imepunguzwa, ilikuwa ni kazi ya Serikali sasa kutafuta fedha zingine ili kukamilisha sehemu ya kazi iliyobakia. Naona kama mtampa shida kidogo Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa sababu tutakapoanza kudai hii kazi itakamilikaje, atashindwa kujieleza.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile pamoja na kazi ya kukamilisha mradi huu, nafikiri fedha zingine zingetafutwa, nyingi zaidi kwa ajili ya miradi ya *Quick Win*. Miradi ya *Quick Win,* tumeshuhudia katika Wilaya ya Kwimba na imekuwa ya manufaa sana. Tuna mradi kama huo wa Ilumba, Ilula na miradi mingine bado inaendelea. Naamini kama Wizara ya Maji na Umwagiliaji ingepewa fedha nyingi zaidi, miradi kama hiyo ingewanufaisha wananchi wengi zaidi. Ni miradi ambayo inakamilika haraka na matunda yake yanaonekana mapema zaidi. Naomba sana Waziri wa Fedha na Uchumi, wakati anamalizia hotuba yake, ajaribu kurekebisha ule usemi kwamba mradi ule umekamilika maana watu wa Kwimba watashtuka kidogo.

Mheshimiwa Spika, kutoka huko naelekea kwenye miundombinu. Mimi nawapongeza kwa sababu mwaka 2000 nilipokuwa naomba kura katika Jimbo la Kwimba, niliahidi kwamba barabara ya kutoka Mabuki - Malampaka ingetengenezwa kwa mradi wa *PMMR*. Nashukuru mradi huo hatimaye umeanza na watu wanafurahia na wanashukuru sana. Kazi iliyofanyika ni *grading,* ni kuparua kutoka Ngudu, nadhani kazi hiyo imefanyika na nadhani wanaelekea mpaka Magu. Nashukuru sana lakini wananchi wangependa kuona moramu inawekwa. Tungependa kupata taarifa moramu itaanza kuwekwa lini katika barabara hizo ili tuwe na uhakika kwamba barabara zile zitakuwa za kupitika kwa mwaka mzima na kwa muda mrefu zaidi?

Mheshimiwa Spika, nafahamu ni mradi wa miaka mitano lakini kwa sababu ndio unaanza, tungependa kuhakikishiwa utajengwa kwa kiwango gani au kwa namna gani? Hayo ndiyo ambayo ningependa kufahamu kuhusu fedha ambazo zimekwenda kwenye miundombinu.

Mheshimiwa Spika, nakwenda kwenye sehemu ya elimu. Mimi naipongeza Serikali kwa kuuona umuhimu huo wa elimu na kuipa kipaumbele cha kwanza. Mwaka jana nilipokuwa nachangia hoja hii, niliiomba Serikali iipatie elimu kipaumbele cha kwanza, nashukuru sana imefanya hivyo kwa sababu bado tuna kazi nyingi sana katika Wizara hii. Tumemaliza majengo sawa lakini majengo sio shule, wala wanafunzi sio shule, tunachohitaji ni wanafunzi pamoja na Walimu. Kila mahali unapokwenda unaulizwa Walimu. Wananchi wameshatumia nguvu zao nyingi sana, wananchi wanatumia fedha zao nyingi sana. Tunashukuru kwamba kuna juhudi nyingi sana ambazo zinaendelea katika upande wa elimu katika kufundisha Walimu lakini naamini kwamba juhudi zaidi zinatakiwa kuongezwa haswa kwa kuzingatia kwamba baadhi ya Walimu sio lazima waende walikopangiwa lakini vile vile sio lazima waende kwenye Shule za Serikali wanaweza kwenda kwenye shule za watu binafsi na maeneo mengine. Kwa hiyo,

bado kasi ya kufundisha Walimu inahitajika sana na iende haraka zaidi ili shule zetu zipate Walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, shule sio majengo wala sio Walimu, tunahitaji maabara angalau wanafunzi wetu wapate elimu ya msingi kwa ajili ya kuendelea katika teknolojia ya hali ya juu zaidi. Kwa hiyo, naomba fedha ambayo Wizara ya Elimu itapewa sasa hivi izitumie vizuri hasa kwa kuangalia Walimu. Unapowaongelea Walimu, lazima ufikirie na nyumba zao pamoja na maabara.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaondoka kwenye eneo la elimu, nina maombi mawili ambayo nataka kuyaongelea. Nilikuwa nasoma kwenye kitabu cha hotuba, ukurasa wa tano kipengele cha pili pale juu, kinaongea juu ya michango ya mapato yasiyo ya kodi. Nikawa najiuliza hiki ni kitu gani? Likaja wazo katika shule zetu kuna kitu kinaitwa *tuition,* je Serikali imehalalisha *tuition* katika shule zetu?

Mheshimiwa Spika, nafahamu wananchi kwa sababu ndio wanaotoa ile fedha wameshakubali, lakini na Serikali itamke basi kuwa imeshakubali, lakini hata yale makusanyo ya *tuition* yawe na utaratibu mzuri ili zijulikane kama fedha hizo zinaishia kwa Walimu, ijulikane ni kwa ajili ya Walimu, kama ni kwa ajili ya manufaa ya shule, ijulikane ni kwa ajili ya manufaa ya shule. Utaratibu ulivyo sasa hivi hata mzazi inamchanganya, mama Hewa hapa alikuwa anauliza, je, ada ni shilingi ngapi?

*(Hapa kengele ililia)*

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Kengele ya ngapi hiyo?

**MBUNGE FULANI:** Ya kwanza.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Ada ni shilingi ngapi kwa shule za sekondari? Tunaambiwa katika shule za sekondari ni shilingi 40,000/= lakini je, kweli mwananchi anatoa shilingi 40,000/=? Kuna michango kiasi gani na *tuition* kiasi gani? Kwa nini Serikali isiseme kwamba basi katika ada tunaongeza sehemu ya *tuition* ili mzazi aweze kujipanga vizuri?

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine, niende haraka haraka, ambayo inanisumbua kidogo, mwaka huu vijana waliomaliza Kidato cha Sita, wameomba kujiunga na Vyuo Vikuu halafu wakaambiwa unaweza kufanya maombi ya kujiunga Chuo Kikuu hata kabla matokeo hayajatoka. Fomu unachukua kwa fedha. Vigezo vya kuingia Vyuo Vikuu vinajulikana ni *Division One, Two* ukiwa na bahati sana labda *Division Three*. Je, huyu mtu aliyechukua fomu kwa shillingi 10,000/= au 20,000/=, matokeo yanatoka, anatoka na *Division Four,* fedha yake itarudishwa au hiyo fedha inakwenda wapi? Mimi nilikuwa nafikiri tuwe na utaratibu mzuri, wasubiri matokeo yatoke, wenye sifa waombe lakini kumwambia hata mtu ambaye amehisi kwamba amefaulu atoe shilingi 10,000/= ambazo hazitarudishwa sio kumtendea haki.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, napenda kuongelea mambo ya usalama wa raia. Serikali inasema haina dini je, Serikali haijui kama kuna Mungu? Je, Serikali haijui

kama kuna shetani? Serikali hii iko upande gani? Naomba kufahamu, hivi Serikali inaposema kwamba haitambui uchawi, inatafsiri gani ya uchawi, maana yake ni nini? Tukisema kwamba mchawi anatumia nguvu za shetani mtakataa au mtakubali? Watu wanauana kwa kisingizio cha uchawi! Mimi naamini lazima zitakuwepo sheria zinazohusu uchawi, naomba Serikali iseme wazi ni sheria ipi na inasema nini ili wananchi waweze kujua wasiendelee kuuana bure.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hautoshi kuendelea na mchangiaji anayefuata. Kwa hiyo, tutaendelea saa 11.00 jioni.

Sasa niwatamke hao watano wa kwanza kwa jioni. Wa kwanza ni Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, wa pili ni Mheshimiwa Fatma Mikidadi, wa tatu ni Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, wa nne ni Mheshimiwa Suleiman Kumchaya na wa tano ni Mheshimiwa Riziki Lulida. Baada ya hapo, tutaona wapi tutafika.

Kwa hiyo, kama nilivyosema awali, kwa kuwa muda hauturuhusu nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(4), hotuba za bajeti pamoja na randama zake zinahitajiwa kuwasilishwa na kuwekwa Mezani na kuwasilishwa kwa Waheshimiwa Wabunge angalau siku nzima ya kazi kabla ya siku husika ya kutolewa hotuba.

Kwa maana hiyo, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ingebidi igawiwe leo kwa sababu keshoni Ijumaa na Jumamosi na Jumapili ni *weekend*, kwa kuwa inaelekea itasomwa Jumatatu lakini tatizo hili haliko tu upande mmoja. Kanuni hiyo imewakuta Waheshimiwa Mawaziri wengi katika Serikali na haikueleweka vizuri, unajua itachukua muda kuzizoea hizi Kanuni.

Kwa hiyo, ninaona badala ya kusimama kila mara kuomba kwa siku hiyo Kanuni itenguliwe, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, aweze kutoa hoja ya kutengua Kanuni husika ili kwa mwaka huu kwa kipindi chote cha Bajeti, tuendelee na utaratibu wa zamani.

**Hoja ya Kutengua Kanuni**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kwa kutumia Kanuni ya 150, Bunge lako Tukufu likubali kutengua Kanuni ya 99(4), ili katika Mkutano huu wote wa

Bunge la Bajeti ya mwaka 2008/2009, kifungu hicho kidogo cha nne kisitumike kwa vile maandalizi ya randama hizi inachukua siku nyingi na fedha nyingi ambazo hazikuwepo katika bajeti ya mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

***(Hoja ya Kutengua Kanuni ilipitishwa na Bunge)***

**SPIKA:** Hoja iliyotolewa imeamuliwa na kuafikiwa. Kwa hiyo, Kanuni ya 99(4) imetenguliwa kwa muda wote wa Mkutano huu wa Bajeti ya mwaka 2008/2009.

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi niliombwa kutoa mwongozo lakini kulingana na hali ninavyoiona ndani ya ukumbi, nadhani nitoe mwongozo baada ya wengine pia kufika tukiwa tumekaa katika hali ambayo tuko wengi zaidi kuliko hivi sasa. Kwa hiyo nitamwita Katibu kwa shunguli inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2007 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika orodha yangu nilishatangaza kwamba tutaanza na Mheshimiwa Profesa Idris Ali Mtulia, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Mikidadi na wakati huo Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, ajiandae.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie katika hoja iliyombele yetu.

Awali ya yote, naomba kuwapongeza Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji Wakuu wa Wizara, kwa kutuletea bajeti inayotia imani, bajeti inayoonyesha tunakwenda mbele. Inasisitiza juu ya kuongeza pato la Taifa, kudhibiti mfumko wa bei, kuongeza makusanyo ya fedha ya ndani na kwamba sasa asilimia mia moja ya matumizi yetu ya Serikali yanatokana na mapato yetu na mwisho utegemezi umepunguzwa kufikia asilimia 34. Moja kwa moja ninaiunga mkono bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uniruhusu niseme machache kuhusu mfumo wa ugawaji wa rasilimali katika nchi yetu uliojitokeza katika bajeti hii na zile zilizotangulia. Nchi yetu ni

kubwa, ina Mikoa mingi, tunatofautiana katika maendeleo Mkoa kwa Mkoa. Ingekuwa Wataalamu wa Wizara ya Uchumi na Fedha wangetaka kutufurahisha sisi, wangechora ramani ya Tanzania wakatuambia kwa uchache Mikoa gani imeendelea sana kwa maana ya kuwa na barabara nyingi, nzuri, nyumba nzuri za kuishi, sekondari nyingi na hali nzuri ya maisha na Mikoa iliyonyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, hiyo katika dhana ya Udaktari, unapokuwa na wagonjwa wengi, wote unawapima kwanza, ukishawapima, unajua huyu na yule wanaumwa sana kwa hiyo unatoa wakati mkubwa na nyenzo nyingi na rasilimali kufanya juhudi ya kuokoa maisha ya yule au ya wale wanaoumwa sana kuliko wale wengine. Mimi napenda kuona mfumo wa kugawanya rasilimali zetu unafuata kwamba wale ambao wako nyuma kimaendeleo wangepata zaidi kuliko wale ambao wanaahueni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kuleta ubishi, ninaomba watu kuwa wakweli kwamba mwingine akipata na mwingine akikosa, kuna kijicho na urafiki huisha na ukitaka kutengeneza urafiki jaribu sana kuweka mambo sawa. Mimi naona mgawanyo wetu huu unahitaji kuboreshwa kidogo ili mambo yawe sawa.

Mheshimiwa Spika, ukitazama vitabu hivi vitatu, *Volume III, Regional Votes* na *Public Expenditure Estimates* na hiki kitabu cha takwimu ya *population* ya Tanzania, halafu ukatazama mgao huu umekwenda vipi, mimi nilichukua muda kidogo. Naomba uniruhusu kidogo ninukuu majibu niliyoyapata, nimepata kama ifuatavyo na nimechukua Mikoa michache tu:-

*"Dodoma ina wananchi 1,900,000 lakini ukifanya per capita, pesa aliyopewa kila mwana Dodoma ni shilingi 22,000/-. Ukienda kwa watani wangu wale wa Mwanza wako 3,200,000 lakini ukitazama per capita waliyopata kila mmoja ni shilingi 23,000/-. Ukitazama Mkoa wa Kilimanjaro una watu 1,500,000 lakini per capita wamepata 39,000/-"*

Mheshimiwa Spika, sasa nenda katika maendeleo, nimeona kwamba:-

*"Mwanza pamoja na watu 3,200,000/- wamepata per capita ya 8,700/- kila mmoja lakini Kilimanjaro wao wapo 1,500,000/- per capita wamepata 10,700/-."*

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi hapa, tunachohitaji sasa ni kukubali kwamba yaliyopita si ndwele tugange yajayo.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kuomba kuwe na fikra ya mabadiliko kwa upande wa watendaji na siasa nzima ya nchi kwamba kwa kuwa nchi hii ina matatizo ya maendeleo tofauti basi kuwepo na *flat per capita* kwanza ya kila Mtanzania halafu kwa nia nzuri itafutwe ziada, iongezwe na wale watu wa mahesabu ya uchumi wanajua itachukua miaka mingapi kuwanyanyua watu walio chini angalau uwiano ukawa mzuri labda ziada hiyo itolewe kwa Mikoa hiyo kwa miaka mitano au sita ili baadaye yale maendeleo yalingane. Lakini tusipofanya hivyo, tunajidanganya kwa sababu chuki itazidi na hakuna atakayepata faida na mtu asijidai kwamba yeye kaendelea sana kwa ajili yeye ana akili nyingi, hapana. Ni mwelekeo wa fedha za Taifa zimeelekezwa sehemu fulani

ndiyo maendeleo yakawa makubwa lakini akili hatupitani jamani, akili hatupitani hata kidogo, mkubali hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali sasa ikubali kuelekeza rasilimali kwanza kila mtu apate *per capita* inayofanana kwa kuwa yeye ni Mtanzania, ana haki ya maendeleo. Lakini hawa watu ambao hawajaendelea, Serikali naomba ifunge mkanda na kukubali tuwaongezee kwa muda ili na wao wapate nafasi ya kuwa karibu karibu na wale walioendelea. Hiyo ni hoja ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, nizungumzie juu ya janga la UKIMWI. UKIMWI upo, sasa hivi hatuna haja tena ya kusomeshana kila mtu anajua upo na unaua, kila mtu anajua nyenzo za kujikinga. Kila mtu anajua unaweza ukaokoka ukawa na nafuu nzuri, hilo si wengi wanaliweza. Tumeona katika *studies* kwamba ukifanya *circumcision* utanusuru asilimia 60 ya wanaume wasiambukizwe, tumefika pale.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho nataka kulieleza Bunge lako, ni jinsi Waziri wa Afya alivyopigiwa makofi mengi pale *UN High Level Meeting for HIV/AIDS*, New York juzi. Kwa sababu hakuna nchi kwa mwaka mmoja imepima kwa hiari wananchi wake milioni 4.2 na ikaonekana kwamba Rais wetu mpendwa ndiyo alianzisha hiyo na tukafanya hivyo, dunia nzima hakuna. Akapata makofi mengi sana, naona tujipongeze wenyewe jamani.

Mheshimiwa Spika, katika *study* ile ya kupima kwa hiari, UKIMWI umeonekana kupungua kuwa asilimia 4.6 lakini uchunguzi wa nchi nzima uliotangazwa hivi karibuni bado UKIMWI umeonekana umekwenda chini, maambukizi yameshuka kutoka asilimia saba mpaka asilimia 5.8.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huo nilioshiriki pale *New York, UN,* hoja sasa sio kuwaambia sasa UKIMWI unaua, UKIMWI unaweza kujikinga, sio hiyo, hoja imebadilika sasa hoja ni kwamba utawafikiaje na kuwatibu wagonjwa wa UKIMWI wote. Ndiyo pale inakuja *the concept of universal access to HIV treatment*, sasa hiyo ndiyo hoja.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano ule nilikuwepo, tuliona tupo katika makundi mawili. Makundi ya wafadhili, wao wanasema hawawezi kutoa fedha kwa sababu sisi wenye ugonjwa wenyewe hatutoi fedha za kutosha kwa kundi letu sisi. Tuliamua Azimio la Abuja ili sasa hivi tuweze kuchangia afya kutoka kwenye pato la Taifa kwa asilimia 15 bahati mbaya sana mwaka huu tupo asilimia 11 lakini hata hivyo ninashukuru sana bajeti inapanda.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa hivi tuna hoja ya kutibu, lazima kuwe na mabadiliko katika fikra zetu katika *TACAIDS. TACAIDS* sasa mfumo wake ubadilike uwe mfumo wa kutibu wagonjwa wengi na kununua dawa nyingi Tanzania. Sasa hivi tuna wagonjwa 440,000 ambao tulitaka tuwatibu lakini tumeshindwa na tunawatibu wagonjwa 150,000 na bajeti hii inatoa shilingi bilioni 150, haitoshi. Hata hivyo, tunashukuru ila jambo kubwa ni kuwa wafadhili wanasema huu UKIMWI nchi yenu haitoi fedha badala

yake wafadhili ndiyo wanatoa. Sasa hii ni aibu, tunashindwa kuzungumza mbele ya wenzetu.

Mheshimiwa Spika, ninaloomba Serikali sasa ikubali kubeba mzigo wa UKIMWI yenyewe. Sasa hivi fedha zinazotumika hazifiki asilimia 30, naomba tungejivuta hata kufika asilimia 50 kwa sababu Botswana sasa hivi imejivuta na wanatumia 90 *percent,* wanatibu wenyewe wagonjwa wao wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka, naomba sasa nitoe hoja kwamba *TACAIDS* kwa kuwa sasa hivi uwezo wake wa kuzungumza kisiasa umeshapitwa na wakati sasa ijielekeze katika kutibu na itoke kwenye Ofisi ya *Prime Minister* iende katika Wizara ya Afya ambako wanajua namna ya ku-*monitor* matibabu na wanajua dawa zinapatikana wapi. Sasa ile siasa wakati wake umeshapita. Kwa hiyo, ninaomba kwa dhati yote kwamba tuihamishe *TACAIDS* kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu tuipeleke Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, *point* ya tatu ni suala la kilimo. Kwa kweli hali ya chakula duniani na hapa nyumbani ni mbaya sana. Nchi nyingine wamekataa kutuuzia chakula, kwa hiyo, ni sisi wenyewe tutajikomboa.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri, Bonde la Rufiji, *arable land* ni 25 *percent* ya nchi nzima, linaweza kulimwa na linaweza kutumika kwa kilimo cha umwagiliwa na linaweza kutoa chakula kwa Tanzania nzima na kupeleka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sasa tupate matrekta. Serikali ijikite katika matrekta. Nakubali kabisa suala la mbegu bora, mbolea, upandaji wa mistari, huduma za ugani, hizi zote zinafanya kazi za kuboresha kilimo lakini kupanua kilimo hakuna mbadala lazima tununue matrekta. Kule Rufiji tunahitaji matrekta sana.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mkuu wa Mkoa wangu, Dr. C. Ishengoma, hakai pale Kibaha lakini kila siku yupo Rufiji kuhimiza kilimo lakini jembe la mkono, hatuendi mbele, tunaomba tupate matrekta Rufiji.

Mheshimiwa Spika, naomba tutazame sasa suala la nishati. Kwa bahati nzuri kule Rufiji, ule Mto una maporomoko ya Stiggler Gorge na umeme unaoweza kupatikana pale ni *megawatt* 900 mpaka 2500 na wawekezaji wapo na tumeshapeleka hoja hiyo Wizara ya Nishati. Kwa kweli, tukiupata umeme pale utakuwa bei rahisi kwa watumiaji na bidhaa zetu zitashindana katika masoko na vilevile tutaweza kuuza umeme nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, suala la gesi ya Mkuranga, hatuoni kwa nini Serikali inakigugumizi kuitumia haraka haraka. Kule Rufiji katika kijiji cha Nambunju kuna tetesi na mafuta yapo, tunaomba Serikali isimame kidete itumie nafasi hizi tuondokane na umaskini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza nami kuchangia katika masuala mazima ya bajeti ya Serikali.

Kwanza kabisa, ninapenda kutoa pongezi na hongera kubwa kwa Wizara kwa kuweza kutengeneza bajeti ambayo inagusa watu wa hali zote kwa unafuu wa maisha, moja ikiwa mikopo ya ujenzi, kwa sababu tumeshaona kwamba ujenzi wa nyumba ni shida sana kwa wananchi.

Tumemsikia Mheshimiwa Zungu anasema kwamba yeye amekaa miaka kadhaa hajajenga nyumba na hii si yeye tu ni watu wengi hata sisi tuliopo hapa, nyumba kwa kweli ni mgogoro kujenga. Kwa hiyo, unafuu kidogo hapo upo.

Mheshimiwa Spika, si hilo tu, unafuu wa maisha umekuja katika suala la kupunguza ushuru wa forodha wa magari ya kuzolea takataka, *switch* za umeme, vilevile kwa *transformer*. Hii inaonyesha moja kwa moja kwamba umeme kwa namna moja au nyingine utakuwa umepungua bei. Kwa kweli, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa niingie kwenye masuala ya bajeti. Kwa miaka mingi, tumekuwa tunazungumza suala la sisi Tanzania kuwa na uchumi mdogo au fedha hazitoshi lakini nafikiri hatujajipanga tu. Sasa lazima twende na wakati na tusingoje wakati utubadilishe. Kwenda na wakati sasa hivi ni kwenda na sayansi na teknolojia. Kama Rais Bush, anaweza kuja Tanzania, lazima na sisi twende na wakati tuongeze uchumi wetu, ni lazima mambo makubwa yatakuja nchini Tanzania, ni lazima tuangalie upya. Kutegemea kilimo kila siku kama nyenzo kuu ya uchumi, kwa kweli ni kupitwa na wakati kwa sababu kilimo peke yake hakitoshi, lazima tuangalie nyenzo nyingine za uchumi.

Mheshimiwa Spika, nina mawazo mengi lakini hapa nitayataja mawili ambayo tungeweze kutumia hayo, yangeweza kuwa nyenzo mbadala ya kuongeza uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni utalii. Utalii ungeweza kutuletea faida kubwa sana nchini mwetu kwa sababu sasa hivi wamebadili kibao badala ya kuangalia mambo yale makubwa makubwa ambayo yapo maeneo mengine, sasa hivi wanataka mambo madogo madogo na mambo madogo madogo, Tanzania yapo.

Kwa mfano, mambo ya jamii, utamaduni, mavazi, sisi tunayo. Hawa watu wa nje wanakuja kututazama sisi tukoje na wanajaa kuangalia mambo kama hayo. Sasa watu kutoka nchi nyingine wanakuja kutuangalia, watu wengine wanasema usanii tu yaani utalii wanaona kitu kama cha usanii tu kumbe wao wanakuja na pesa zao wanaongeza uchumi wa Tanzania. Sasa kama tungejipanga upya katika utalii, kwa kweli utalii ungetuletea pesa nyingi sana Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Tanga kuna masuala ya utalii, Mbeya kuna utalii wa milima mikubwa mikubwa, Iringa nao kuna maeneo ya utalii wa mambo madogo madogo hayo. Nitolee mfano Mkoa wa Lindi wanakuja kuangalia masuala ya jamii na vizazi vyao, wanakuja kuangalia mambo madogo madogo tu. Kwa mfano wanakuja kuangalia eneo la vita vya majimaji, vizazi vyao na wajukuu wao walivyo. Kila siku watu 50 wanakuja Kilwa na hata ukizuia namna gani wanajaa. Sasa hivi Kilwa kwa nwezi unaweza ukakuta watalii 1000 na zaidi hata kama hakuna pa kulala wanajenga *tent* wanalala siku mbili, tatu wanaondoka lakini hatujajipanga kwa suala la utalii. Hawaangalii tena masuala ya fisi, twiga, mbuni au Mlima Kilimanjaro, wanataka jamii inafanya nini. Wanakuja Kilwa kuangalia Kinjeketile yuko wapi na vizazi vyake.

Mheshimiwa Spika, si hilo tu, wanakuja kuangalia magofu ya Waarabu na Wareno. Kilwa kuna mapango 22; wanasikia huko na wanakuja kuingia na kutoka. Lakini kuna pango moja kubwa wanasema ni pango kubwa kuliko yote katika Afrika wanakuja kuangalia likoje, lakini hatujajipanga. Wanakuja bure na kutoka bure, Serikali haijajipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si hilo tu Zanzibar hapa hapa utalii umeshamiri sasa hivi. Hakuna kitu kikubwa zaidi lakini watalii wengi wanakwenda wanaacha Kilimanjaro kwenda kuangalia Mlima na wameacha kuangalia fisi lakini wanaenda Zanzibar, wanakwenda kuangalia nini? Wanakwenda kuangalia magofu ya Waarabu walivyotawala zamani na vizazi vyao, kuangalia mtu amevaa kanzu na kofia, kuangalia mtu amevaa buibui, ni utalii huo, si usanii. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninachozungumzia...

**SPIKA:** Wanavaa baibui sio buibui. *(Kicheko)*

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Wanakuja kuangalia shilingi aliyokuwa anatumia Sultan Balaghash, hii hapa na ninazo nyingi, aliyokuwa anatumia Sultan zamani ambayo ina nembo ya bendera ya CUF, hii hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, upande mmoja imeandikwa Zanzibar Sultan Balaghash 1300 sijui na ngapi, anayeweza kusoma Kiarabu aje kusoma Kiarabu hapa. Huku kuna mizani miwili sawa sawa na bendera hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wanakuja kuona vitu kama hivyo…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hebu mkabidhi Mhudumu ili Spika aweze kuona, maana sioni hapo. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ninachosema ni kwamba utalii sasa hivi tunaangalia *interest* za watu kwamba wanakuja kuangalia jamii na vizazi

vyao vinafanya nini. Wareno wanakuja Kilwa kuangalia mambo waliyoacha wazazi wao ni yepi.

**SPIKA:** Hiyo sarafu, naiomba hiyo sarafu!

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, sawa! Muda unapita! *(Kicheko)*

**SPIKA:** Muda unalindwa! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nitakupa mbili, ziko tano!

Mheshimiwa Spika, naendelea!

**SPIKA:** Endelea mama!

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, Kilwa kuna viboko 500 wanaoongea na watu. Hiyo ni utalii, wanakwenda watalii pale wanaongea na viboko. Haijapata kutokea, eehe!

Mheshimiwa Spika, kuna uwindaji, watalii wanakuja kuwinda wenyewe, wanasema hivi kweli naweza nikapiga bunduki nikawinda, anatazama shabaha yake iko wapi, huo ni utalii!

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba lazima tubadilike, tutafute vyanzo vingine vya utalii na inaweza kutuletea faida zaidi katika utalii.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo lingeweza kutusaidia katika masuala ya uchumi ni nishati au madini. Kwa kweli, madini ni kitu ambacho kingeweza kutuletea uchumi mkubwa sana hapa nchini. Madini haya haya kwa sababu sasa hivi wanachojua ni madini ya Mererani, Geita na Kiwira, basi lakini hawajafanya utafiti mzuri nchini, madini yako ya aina gani na yako wapi, kuna sehemu nyingi tu zenye madini.

Mheshimiwa Spika, ukichukua mfano sehemu za Kusini; mimi napenda kutolea mfano maeneo yangu kwa sababu nina uhakika, sehemu zingine naweza nikakosea. Ukichukua Kusini, kwa mfano, ukija Mkoa wa Lindi, utakuta Kilwa kuna *Gypsum* ambayo inaitwa Jasi kwa ajili ya mbolea na kwa ajili ya kutengenezea *cement. Cement* huwezi kutengeneza bila kutumia Jasi ambapo ile ya Kilwa ni asilimia 90 lakini watu wanakwenda kutafuta Jasi yenye asilimia 60 ambayo haifai, tena iko mbali, chini kabisa, ipo Arusha lakini Kilwa unaparuza tu na mkono, unaikuta ipo nyingi tu. Wanakwenda kutafuta India kwa bei kubwa, mabilioni ya *dollars* wakati Tanzania Jasi ipo nyingi hawataki kuitumia.

Mheshimiwa Spika, siyo hiyo tu, kuna chokaa, kuna gesi ya Songosongo, madini hayo niliyosema, kuna gesi ya Mnazi *Bay* ambayo miaka 600 ipo, Rwangwa kuna dhahabu, kuna kitu kinaitwa *Green Tourmaline, Green Garnet* ipo Rwangwa, lakini

haijaangaliwa. Wachimbaji wadogo wadogo wanachezeachezea tu lakini hawa tungewaunga mkono wakapata nyenzo za kufanyia kazi, tungepata uchumi wa kutosha kwa kweli. *Green Tourmaline*, *Green Garnet* ni mali kubwa kabisa. Kuna *Sapphire* Rwangwa huko huko, kitu kinaitwa *Sapphire*. Kuna rangi rangi za aina mbali mbali kumi na mbili ambazo unaweza kupaka katika nyumba, zipo Rwangwa lakini watu wanachezea tu, wanafanya usanii tu basi, hatujajipanga!

Mheshimiwa Spika, si hilo tu, Nachingwea kuna dhahabu. Halafu kuna kitu huko Ludewa, Liganga. Hii Liganga, tunaambiwa kuna chuma cha Liganga, kuna mkaa wa mawe. Sasa chuma cha Liganga, kuna kitu ndani yake kinaitwa *Titanium* na *Vanadium*. Haya ni madini ambayo yanapatikana nchi tatu duniani. Yanapatikana Marekani, Afrika Kusini na Tanzania. Kazi yake ni kutengeneza nyuklia, kazi yake ni kutengeneza mbawa za ndege na bodi za ndege. Sasa sisi kwa nini tulalamike kwamba hatuna uchumi, hatujafanya kazi na hatujajipanga. Kama mambo haya yangefanyiwa kazi, kwa kweli sisi tusingekuwa maskini. Kwa hiyo, vitu kama hivi vingekuwa vimefanyiwa kazi, sisi tusingekuwa na umaskini wowote.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa lazima mazingira yatengenezwe. Mazingira ya eneo husika kama mnataka kusaidia vitu hivi, lazima yatengenezwe. Yatengenezwe vipi? Kama mngeweza Mkoa wa Lindi, kutusaidia maji hasa Lindi Mjini, Nachingwea, Rwangwa vile vile kutusaidia umeme, ingesaidia. Sasa hivi Nachingwea, Rwangwa, Liwale kwa miezi mitatu hakuna umeme. Sasa utalii bila umeme hauwezi kuja, watalii wale wanakimbia sasa. Wale waliokuwa wanakuja 50 kwa siku wanakimbia kwa sababu hakuna umeme. Sasa hilo jamani mtusaidie. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, *MCC* imekuja kwa malengo ya kufanya mambo matano ambayo ni barabara, umeme, *airport* na maji. Sasa kwa nini tusimegewe kidogo ikapelekwa Kusini kama msaada?

Mheshimiwa Spika, vilevile, tungesaidiwa *airport*, *airport* ya Lindi imetengenezwa mwaka 1939 wakati wa vita ya pili na mpaka leo inatumika, zinaweza kuingia ndege nne kwa pamoja, *yes*!

*(Hapa kengele ililia)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili hiyo!

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia, ahsante sana! *(Makofi)*

**SPIKA:** Sina budi nikiri Mheshimiwa Fatma Mikidadi, usemaji wako, ndani yake una vitu vingi vinaburudisha. Nilitamani uendelee, lakini kanuni haziniruhusu.

Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, halafu Mheshimiwa Suleiman Kumchaya ajiandae. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi leo kuniona kwa macho mawili. Naona asubuhi kidogo ulielekezwa na mtu kwamba mimi nipo, ulikuwa hunioni sijui, lakini kumbe mimi ndio sikuoni wewe! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, awali ya yote, nataka kusema kwamba naunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wetu kwa aslimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, halafu kwa kuwa vile vitabu vimeandikwa na mimi lazima niwe na vitu vyangu kadhaa ambavyo vilitakiwa viwepo, lakini havikuwepo, ninapenda sana vingeongezwa ili niweze kuona kwamba mambo yametimia kinamna yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, nitaanza kuchangia kuhusu suala la hawa jamaa zetu wanaopinga hii hoja. Wanasema kwamba hoja yetu mbovu, sijui nini, mimi nasema kwamba, Mheshimiwa Mkulo, usiache kulala, lala, kwa sababu hawa watu ni lazima wawepo na wasipokuwepo, labda sisi ndio tutalala, sasa hivi, tuwaachie tu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ukija kwangu Kilwa, mimi ninao kibao wala siwaogopi. Sina macho lakini siwaogopi na waje tu na wala siwaogopi lakini nasema hivi, waje kwa ajili ya nini, kwa ajili ya wananchi wetu, kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Ndugu yangu Mheshimiwa Mkulo, usiwaogope, lala usingizi, tengeneza watoto, wewe fanya utakalo, wala usiwe na wasiwasi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpanda, akilala usingizi, hawezi kutengeneza watoto! *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninalotaka kuzungumzia ni kuhusu suala la kilimo. Suala la kilimo kusema kweli, limezungumzwa na wenzangu wengi na sisi Lindi kusema kweli, tulikuwa na Halmashauri, lakini tukazifanya mbili kwa sababu gani, kwa sababu ya kwanza, tukaifanya ya kisiasa, ya pili tukasema ya kufuata kilimo. Tukaunda kikosi kazi, kikosi kazi cha kulima na tulikuwa tunasema kwamba watoto wanazaliwa kama kompyuta, lakini, kilimo tunakizembea. Sasa hii aibu, aibu kubwa na mimi sitakubali kuacha kuzungumzia suala hilo kwa kuwa naona dunia inavyokwenda. Watu sasa hivi dunia nzima wanasema mafuta na uhaba wa chakula, sasa kwa nini mimi nisizungumzie kilimo leo? Lakini, nashangaa kusikia kwamba Lindi au Kilwa au Kilwa Kaskazini kwa jina, hususan, hata trekta moja ndugu zangu, hata hamnipi! Mimi mnataka nilime kilimo kile cha kijembe cha mkono? Jamani. Kikosi changu cha kilimo kitafanya kazi kweli? Kwa hiyo, naomba hilo ulitilie mkazo.

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumza kuhusu suala la hawa ndugu zangu wanaopinga kidogo kuhusu bajeti yako au hoja yako. Mimi nataka kuzungumzia kisomi kidogo kwamba kila kitu lazima kiwe kina *opposition* na kwamba hata ukisoma ile *Newton's Law of Motion,* inasema:-

*"Lazima kitu kiwepo na kitu kinachokizuia ili kitu kisimame"*.

Kwa hiyo, hawa watu hawa lengo lao sisi tusimame ili wao wakae kwenye maeneo yetu na sisi tunasema hatuwaruhusu, tunaenda mbele na hatuwaogopi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ninalotaka kuzungumza ni suala la maji. Maji ndugu zangu, ni kwamba tunatilia kipaunyuma, sielewi kwa nini tunapoona mambo yanayohusiana na maji, tunaweka nyuma sana, nyuma sana, *percent* tatu, inakuwa vipi?

Mheshimiwa Spika, angalia kila swali linaloulizwa hapa, utamkuta Waziri wa Maji anajibu, wapi visima, wapi mabwawa, wapi nini, matatizo ya maji. Kwetu kule Kilwa maji, ni matatizo kweli. Mnawapa *percent* tatu, mnafikiria nini?

Mheshimiwa Spika, kuna *DDCA*, wakala hii imeanzishwa na mimi pale nikiwepo wakati huo, zamani za kale, mwaka 1999 na mimi nilikuwepo. Lakini mpaka sasa hivi bado inadorora mpaka naona uchungu, kwa nini vinatokea vitu kama hivi? Ituibue, tuwainue hawa watu ili masuala ya maji yaweze kupamba moto.

Mheshimiwa Spika, hili tatizo ni *very initial*, vitu vya msingi kabisa ambavyo binadamu wa kawaida ni lazima apate chakula na apate maji na maji hatuyapi kipaumbele, kwa nini lakini?

Mheshimiwa Spika, namalizia na suala la nne. Nataka kumkumbuka Mahatma Ghandi na namchukua Mahatma Ghandi kwa sababu namjua yule Max ana ma-*volume* makubwa, wengine labda pengine itakuwa tabu kuyasoma. Lakini, mchukulieni Mahatma Ghandi, alisema kwamba:-

*"Ili nchi iendelee, lazima kuwepo na vitu vitatu. Aliweka mafiga matatu, human resources, natural resources na industrial"*.

Mheshimiwa Spika, ndio maana akapata na *Nobel* enzi hizo. Sasa leo tunaanza kurudisha nyuma tena, elimu, *human resources,* watu tunaanza tena kugombanagombana.

Mheshimiwa Spika, shule zangu mimi, mwalimu mmoja, maktaba ndiyo usiseme, hakuna. Sasa tunakwenda wapi? Tunaposema *natural resources*, mama Mikidadi hapa naona ameni-*pre-empty* kweli lakini nilitaka nayo kuyasema yote hayo lakini na mambo ya viwanda nayo sitayaacha nyuma, maana mama Hewa kazungumza kweli mimi sitaki kurudia tena maneno hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa mara ya mwanzo, ulinitamka kwamba ningechangia, lakini baadaye ukaniruka kwa namna unavyojua mwenyewe, lakini bahati nzuri sijui nani amekukumbusha lakini nasema hivi, mimi natumia ile *theory* aliyotoa mwenzangu Eichetein yule Mjerumani, *thesis* yake ya *PhD* ilikuwa na kurasa 24. Kutokana na kitabu hicho, watu wanatoa *volume* na ma-*volume* na ma-*volume* na ma-*volume* ya *PhD* pamoja na mimi mwenyewe nimetumia kitabu hicho hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema hivi, bora nikatishe kwa kuangalia kwamba Eichetein kama aliweza kumaliza *PhD* yake kwa kurasa 24, je, kwa nini mimi nisiweze kumaliza kwa dakika tano?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hawa Ndugu zangu wa Kusini hawa, basi ngoja tuendelee na mwingine. Mheshimiwa Suleiman Kumchaya! Ajabu! Atafuatia Mheshimiwa Riziki Lulida, sijui wamepangaje hawa? Halafu ndio tunahamia Kanda ya Ziwa, Mheshimiwa Magale Shibuda. *(Kicheko)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika bajeti hii.

Pili, ningependa kuchukua nafasi hii kuwapongeza ndugu zetu, Mheshimiwa Waziri Mkulo na Manaibu wote wawili, Katibu Mkuu na Manaibu wake na watendaji wote wa Wizara hii ya Fedha na Uchumi kwa jinsi walivyoiandaa hii bajeti ambayo leo tunaichangia katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, si rahisi hata kidogo kwamba wanaweza wakayafanya mambo yote kwa wakati mmoja na hasa tukizingatia kwamba bado nchi yetu ni maskini na ndio maana ninawapa pongezi hizi kwa sababu wamejitahidi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Lulindi katika Wilaya ya Masasi, Mkoa wa Mtwara, nina mambo ya kuzungumza, yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, naanza na miundombinu. Katika bajeti hii ambayo tumeizungumza leo hii, miundombinu imetengewa bilioni 9.733. Ni hatua kubwa sana! Ninawapa pongezi hizi lakini nafikiri tumefika mahali tuanze kubadilika kidogo na kubadilika huko ni kwa sababu ya kutaka kujenga mazingira ya uchumi wetu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni kwa muda mrefu sasa, barabara zetu za vijijini ambako ndiko tunakolima mazao mengi, ni mbaya sana. Mbaya kiasi ambacho wakati mkulima anapotaka kusafirisha bidhaa zake, anapata matatizo makubwa na matokeo yake anachelewa kufika sokoni. Hata kama anachukua nyanya, basi kuna uwezekano mkubwa nyanya hizo zikaoza.

Mheshimiwa Spika, katika msimu uliopita wa korosho, mimi mwenyewe nimeona jinsi gani malori yalivyokuwa yanakwama vijijini kwenda kukusanya korosho kupeleka

katika maghala. Korosho ambazo zinachukua nafasi kubwa ya fedha za kigeni katika nchi yetu kwa sababu tu barabara ni mbovu.

Mheshimiwa Spika, naomba basi niiombe Serikali pamoja na wengine wote wanaohusika, kwamba sasa imefika wakati tuzitazame barabara za vijijini ambako ndiko chimbuko la uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nilikwenda katika kata moja kule kwetu Mnavira. Mnavira ni sehemu ambayo inazalisha korosho katika nchi hii nyingi sana, nimekuta malori yamekwama, hayaendi kwa sababu barabara ni mchanga mtupu na hii imekuwa kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, tukisema kwamba tunazo Serikali za Mitaa, Halmashauri zetu zinaweza zikajenga barabara hizi, si kweli hata kidogo. Uwezo wa Halmashauri zetu ni mdogo sana, hawawezi wakaifanya hii kazi hata kidogo. Kwa hiyo, kuna haja ya Serikali Kuu ya kuongeza nguvu ili barabara hizi za vijijini zijengwe, magari yapite, bidhaa zifike kwa urahisi katika masoko na uchumi ujengeke.

Mheshimiwa Spika, kupanga ni kuchagua, sasa kama tunachagua, basi moja kati ya mambo ambayo tutachagua ni barabara vijijini.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji ni kubwa sana katika nchi yetu lakini ni kubwa sana katika Jimbo langu. Katika kipindi kilichopita, Serikali ilitoa ahadi ya kuboresha na kutengeneza vyanzo vya maji katika Jimbo langu. Katika Jimbo langu, kuna chanzo cha maji kinaitwa Chiwambo. Ni chanzo kikubwa na ni rahisi kupatikana kwa maji, kinachokosekana ni mitambo tu ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, katika swali langu kipindi kilichopita, Serikali iliahidi kutoa shilingi 168,290,000 ili mradi huu wa maji utengenezeke. Katika chanzo cha maji cha Lupaso, shilingi 19,500,000. Nashukuru pale tayari visima vimeishajengwa lakini bado hali si nzuri kiasi hicho. Chanzo cha maji cha Mkululu kilitengewa shilingi 120,703,000.

Mheshimiwa Spika, mpaka ninapokuja leo hii kuzungumza hapa, ahadi hii ya vyanzo hivi viwili haijatekelezwa hata kidogo. Wale wapiga kura wangu wataniona muongo pamoja na kwamba wamesikia redioni na nilijitahidi kumchukua Mheshimiwa Waziri wa zamani wa Maji, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, ameviona vyanzo hivi. Nainaomba sana tufike mahali ahadi hii itimizwe.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie kuhusu kilimo. Ni muda mrefu sasa tumezungumza kwamba kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wa maisha yetu. Kwa kipindi cha miaka 20, wataalamu wanasema sekta ya kilimo imekua kwa wastani usiozidi asilimia nne tu. Sasa hivi Watanzania tunafika milioni 40, kukua kwa kilimo ndio huku? Wanatuambia wataalamu hao kwamba kama kilimo hakitakua haraka kiasi hicho, itachukua karne moja na zaidi ili Mtanzania aweze kuwa na maisha bora.

Mheshimiwa Spika, kuna haja sasa ya Serikali kuweka utaratibu wa kupata zana za kisasa kwa mfano, matrekta na zana nyingine. Mimi nasema pamoja na kuagiza kutoka nje, lakini tunaweza tukaweka mipango ya kutengeneza vifaa vya kilimo hapa hapa ndani pamoja na matrekta haya, tunaweza. Vijana wetu wengi tu wamesoma sasa hivi ili tuweze kubadilisha kilimo chetu. Haya mambo kila siku tunakuja hapa, tunazungumza kilimo, sijui vitu gani na nini, uwezo upo ndani yetu sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ifanye maamuzi ya makusudi kabisa ili kilimo chetu kiweze kubadilika. Tujitahidi kuondoa kodi hizi ambazo siyo za lazima katika vifaa vyote, mazao yote na maeneo yote ya kilimo ili kilimo kiweze kuongezeka katika nchi yetu, watu wetu wawe na maisha bora na uchumi wetu uweze kukua.

Mheshimiwa Spika, katika kilimo hapo hapo, mwaka jana tulipitisha sheria hapa, tuseme tulirekebisha, ili sisi watu wa Kusini tunaolima korosho, tufaidike na *Export Levy*.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba nisome, lakini katika lugha ya kiingereza: "*The Principal Act is amended by adding immediately after section 10 the following not with standing section eight a person who exports raw cashew nut shall pay and export levy to be computed and collected by the Tanzania Revenue Authority at the rate of 10 percentum of FOB value, the rate of 10 percentum collected under sub section one should be divided as follows; 6.5 shall be divided among District Councils which are cashew nut producers*" na nyingine.

Mheshimiwa Spika, lakini mpaka ninapozungumza hela hizo hatujazipata bado. Naomba Serikali ituambie wanatumia sheria gani? Ni hii ama nyingine? Ili tuzipate hizi pesa tuboreshe kilimo chetu cha korosho.

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Mkulo atakapokuja hapa atueleze hizi pesa zimekwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa kutusaidia suala la bandari na itafanya kazi sasa hivi na *Artumas* itafanya kazi sasa hivi. Lakini sio vibaya nikisema

lingine, kwamba kuna haja ya kubadilisha uwanja wa ndege wa Mtwara kuwa uwanja wa Kimataifa. Uwanja ule umekaa mahali pazuri, ni mpakani viwanda vinakwenda na umeme upo, kuna Mozambiq, Zambia na Malawi. Tusichelewe hata kidogo, kwani wakati ni huu.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni kwamba tulipokuwa tunapitisha bajeti hii katika eneo la kodi, tulielezwa kwamba kutakuwa na asilimia 10 ya ushuru wa simu za mkononi. Sina kipingamizi na hilo hata kidogo na nia ni ile ile ya kutaka ku-*harmonize* kodi katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, lakini ukitazama, utakuta wenzetu Kenya na Uganda kodi zao zipo chini na kodi zetu zipo juu. Leo unasema tuchukue asilimia 10, ni sawa. Lakini ni kweli itatusaidia, itafikia mahali Watanzania watashindwa kumiliki simu za mikononi na kufanya hivyo kuyafanya haya makampuni yasiweze kutoa kodi ya mapato Serikalini kwa sababu tu inakosa watu wengi.

Mheshimiwa Spika, naomba tutazame tena eneo hili ingawa nia yetu ni nzuri ya kutaka kurekebisha kodi katika Afrika Mashariki, lakini leo hii tukiona wenzetu bado kodi iko chini na sisi iko juu na kodi zenyewe ni nyingi, naomba tutazame kidogo, twende mbele lakini pia turudi nyuma kidogo.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kabisa ni *empowerment*, kwa Kiswahili ni uwezeshaji. Tuna sera nzuri sana. Kuna *MKUKUTA*, *MKURABITA*, *MKUMBITA*, sera nzuri sana, lakini mimi nasema tufike mahali tufanye maamuzi ya makusudi kabisa kuwasaidia watu wetu.

Mheshimiwa Spika, leo ukizungumzia uchumi katika nchi yetu, watu ambao wanazungusha uchumi katika nchi hii ni wachache sana, wengi ni watazamaji. Hii inachangia katika kukua kwa uchumi wa nchi yetu kwa sababu sio wengi ambao wapo katika mzunguko wa uchumi. Leo hii huwezi kunilinganisha mimi na mtu mwingine aende katika mabenki makubwa akachukue mkopo aupate kwa urahisi kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, atakayekwenda kule ni wale matajiri wakubwa ndiyo watakaopata mkopo. Kwa kufanya hivi, tunachelewa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, hata kama sio leo, lakini tutazame uwezekano wa kuweka mazingira ya makusudi kabisa ya kuwawezesha watu wetu huu *MKURABITA* ufanye kazi vizuri, *MKUKUTA* ufanye kazi vizuri na mengineyo yafanye kazi vizuri ili washiriki katika kujenga uchumi wa nchi yetu na hii itasaidia katika hivyo vipaumbele vitakavyoleta uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, nimezungumzia masuala ya Bandari, leo ukizungumza kuhusu wawekezaji, unazungumza habari za nje. Hakuna mwekezaji kutoka Tanzania hata kidogo ambaye anaweza kuwekeza katika bandari, reli, mashamba makubwa makubwa!

Mheshimiwa Spika, tunategemea watu kutoka nje, sasa tufike mahali tutafute utaratibu mzuri ambapo wananchi wa kawaida watashiriki. Wenzetu nchi nyingine wameyafanya haya! Malyasia waliamua kwa makusudi kabisa wakafanya haya kwamba hapa ni kwa Suleiman Kumchaya, hapa ni kwako wewe. Kwa kufanya hivyo, wakajenga uchumi wao haraka haraka! Leo Malyasia ni moja kati ya nchi ambazo zimekua kiuchumi katika Asia ya Mashariki. Kwa nini sisi hapa hatuwezi?

Mheshimiwa Spika, tufike mahali hizi nyimbo za kipaumbele tuanze kuzipunguza kidogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Suleiman Kumchaya kwa mchango wako. Namwita sasa Mheshimiwa Riziki Lulida, ajiandaye Mheshimiwa Magale Shibuda halafu atafuatia Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi.

**MHE. RIZIKI SAID LULIDA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kuchangia siku hii ya leo katika hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Manaibu wake, Katibu Mkuu na bila kukosa fadhila napenda nimshukuru Mwenyekiti wa Bodi ya *TRA* - Mama Marcelina Chijoliga, kwa ushirikiano aliounyesha kutuletea bajeti ambayo sasa hivi tunayo mezani.

Mheshimiwa Spika, ni lazima nishukuru kuwa Mwenyezi Mungu ametupenda wananchi wa Kusini. Sasa hivi tuna matarajio makubwa ya miundombinu ya barabara ya kutoka Dar es Salaam mpaka Lindi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mikoa ya Kusini waliteseka kwa muda mrefu sana kwa kukaa barabarani siku tano hadi sita, lakini sasa hivi ni lazima tuseme ahsante sana na Mwenyezi Mungu awajalie sana.

Mheshimiwa Spika, kwa nini ninazungumza hivyo, tumepata wakandarasi watatu kutujengea barabara ya Lindi mpaka sasa hivi, Mkandarasi wa kwanza ni *M/S* Kalafu, Mkandarasi wa pili ni *SICO* na wa tatu kutoka Kibiti tumewapata Watanzania wenzetu wa *TANROAD* kutujengea barabara.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tukubali kwamba *M/S* Kalafu amefanya kazi nzuri! Ile barabara ni ya mfano na ni ya kuigwa na zionyeshwe wakandarasi wengine kuwa kweli wanaweza kujenga barabara ikaonekana katika macho ya watu kwamba ile ni barabara.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba kipande kilichobakia kutoka Malendegu mpaka Ndundu kama kweli mnaitakia mema nchi hii mpeni *M/S* Kalafu kile kipande akimalizie ili tuweze kufaidika na ile barabara.

Mheshimiwa Spika, ile barabara tuna imani tutakaa miaka 22 bila kuigusa. Lakini sasa hivi ni lazima tusikitike kwa sababu kipande cha kutoka Mbwemkulu kwenda Nangurukulu sasa hivi hatujakabidhiwa, viraka vimeanza kuwekwa. Sasa mimi sielewi ni kwa sababu ya wasimamizi kuwa wabovu au ni kitu gani. Hatupendi turudie tena watu kama hao watakaoturudisha nyuma katika maendeleo ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, sio barabara hiyo tu ambayo mimi naona kuna utata mkubwa ambao unajitokeza. Serikali inatoa pesa nyingi sana ili angalau Watanzania wawe na barabara nzuri, lakini baadhi ya makandarasi wakishirikiana na wasimamizi, hawako tayari kuisaidia nchi hii.

Mheshimiwa Spika, leo tunategemea kupata barabara nzuri kupunguza foleni Dar es Salaam, kama barabara ya Sam Nujoma, lakini ninavyoona sasa hivi tunakokwenda tunarudia kule kule katika barabara ambazo haziko katika viwango. Tuisaidie nchi hii tupate barabara yenye viwango ili tuondokane na usumbufu wa barabara.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wangu wa Lindi tunahangaika sasa hivi na barabara za Mikoa, leo Mwananchi kwenda Liwale anatoka Dar es Salaam anakuja mpaka Lindi wakati wa masika anakwenda mpaka Masasi ndipo afike Liwale. Lindi hatuna barabara za Mkoa wakati wenzetu wanahangaika na barabara za lami Vijijini. Imefikia mahali ambapo na sisi tunajiuliza kulikoni wengine Vijijini wanapiga lami lakini Mkoa wa Lindi hata kutoka Nachingwea kwenda Liwale inachukua siku mbili watu wako katika baiskeli na *Land Rover?* Kweli inakatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, ifikie mahali kuwa uwiano huu waache sehemu fulani waangalie sehemu ambayo ni korofi waweze kuwasaidia ili wananchi nao waondokane kukaa katika visiwa wakati wa masika, miezi mitatu hajakanyaga Dar es Salaam hata Nachingwea kutokana na barabara mbovu. Kwa hiyo, hili ni lazima tuliangalie sana.

Mheshimiwa Spika, sitakuwa mchoyo wa fadhila bila kuipongeza sekta ya utalii. Sekta hii imejitahidi sana sasa hivi kuleta pato kubwa sana la nchi, lakini tusijivunie hilo pato ambalo limepatikana, inabidi iwe utalii endelevu ili angalau pato liweze kukua zaidi. Kwa mfano, leo Mkoa wa Lindi tunamiliki asilimia T! ya *selous,* lakini hiyo *selous* sasa hivi haina faida yoyote kwa mwananchi wa Lindi hata wenzetu wa Morogoro naona ni hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, ningependekeza selous sasa hivi iwe *agency* kama mashirika mengine ama *TANAPA* ili zile *agency* ziweze kuleta mafanikio na kipato kwa Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii inabidi iendelezwe na Serikali itoe pesa ya kutosha kusaidia utalii ili uwe utalii endelevu. Kwa mfano, Mashirika ya *TANAPA*, Ngorongoro ambayo yanajitahidi kuboresha sekta ya utalii na kuleta utalii endelevu na kuingiza kipato Tanzania, lakini unakuta pato kubwa ni la kuchangia katika michango ya maendeleo ya ujenzi wa shule ni wao Ngorongoro, *TANAPA* kwa ujenzi wa madarasa na

ujenzi mahospitali. Wanatoa pesa nyingi sana kwa ajili ya huduma ya jamii kwa Watanzania. Hivyo, ni lazima na wao wapewe nafasi wapate pesa kiasi cha kufanya maendeleo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano sasa hivi tumeongeza hifadhi 10 ndani ya *TANAPA*, kuna Katavi, Ruaha, Gombe, Mahale, Mkomazi ambapo panahitaji kuendelezwa. Hivyo hizi Taasisi wakinyang'anywa pesa zao ziingie katika mfuko tutapata wapi pesa za kuboresha hizo hifadhi nyingine ambazo zimeingia katika hifadhi ya mbuga za wanyama?

Mheshimiwa Spika, katika jambo hili Serikali iliangalie kwa huruma, waangalie *sources* nyingine kama madini ambazo mpaka sasa hivi hawajatoa pato lolote katika nchi hii ili nao waweze kutumia zile pesa kwa maendeleo endelevu ndani ya sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, hakuna cha kuficha. Sasa hivi Tanzania utalii unakua! Katika Mkoa wa Lindi tuna vivutio vingi ambavyo inabidi vitumike! Kwa mfano, leo Wilaya ya Kilwa, yenyewe ina urithi wa dunia namba 21. Lakini mpaka sasa hivi ule urithi haujatumiwa kikamilifu, watalii wanakuja kama hawana wenyewe, nilihoji katika Halmashauri mpaka sasa hivi hawa watalii wanaokuja Kilwa mnapata nini? Wananchi wananiambia hatupati hata senti tano.

Mheshimiwa Spika, hii yote inaonekana maendeleo yanaangaliwa sehemu moja. Inaangaliwa Kaskazini tu, lakini Kusini kuna utalii mkubwa sana ambao inabidi Serikali ikae iangalie tutafanya nini na Katavi. Katavi wana Twiga weupe ambao hakuna sehemu nyingine yooyote duniani. Watalii wanataka kwenda kule, lakini inabidi kuboreshwe, kwa kutumia miundombinu, barabara, mazingira mazuri ya wafanyakazi ili angalau utalii endelevu uweze kwenda sehemu nyingine ili na kipato kiweze kupatikana na kusaidia wananchi wa sehemu hizo ambako wanatoka.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi na Mtwara, leo Mikindani tuna magofu yetu ambayo inabidi yaendelezwe, yatunzwe ili watalii waweze kwenda kule na uwekezaji wa mahoteli upelekwe kule ili uweze kusaidia.

Mheshimiwa Spika, bila kificho, leo kuna watu wanachukua *beach* kienyeji bila uwekezaji endelevu. Inabidi Watanzania wagangamale ili wale watu wanaokuja kuchukua hizi *beach* wawekeze na Watanzania wenyewe, pajengwe hoteli endelevu ili angalau watu watakapokuja kule wapate mahali pa kufikia penye mazingira bora.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda nilipe kipaumbele ni kilimo. Mwenyezi Mungu ametujalia Tanzania, tuna ardhi kubwa na yenye mazingira mazuri ya kijiografia, tunapata mvua za kutosha, tuna mabonde mazuri, kwa mfano, Mkoa wa Lindi tuna mabonde ya Mavuji. Leo ukiona mavuji utajiuliza, hili bonde kwa nini limeachwa hapa? Lakini matokeo yake ardhi inapewa watu kuwekeza katika jatrofa. Hivi jamani jatrofa inapewa kipaumbele kuliko chakula?

Mheshimiwa Spika, leo tunazungumzia mabaa ya njaa ambayo yanatukumba Tanzania, tunataka tuendeleze kilimo cha mpunga, kilimo cha mahindi cha kiangazi na wakati wa masika. Lakini kwenda kuwekeza jatrofa ni kudidimiza na kuweka hali hii izidi kuwa ngumu.

Mheshimiwa Spika, mimi siamini kama kweli wale watu wanataka kuwekeza kwenye jatrofa. Yale maeneo yana madini vilevile, hivyo tutakapozigawa ardhi zetu tuwe na vigezo vizuri vya kuangalia: Je, tunampa huyu ardhi, kweli anataka kulima hii jatrofa? Je, lipo soko kubwa la jatrofa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, tujiandae katika sekta ya kilimo, yale mabonde yawekezwe, tupeleke matrekta, watu walime na watu tupate chakula kitusaidie isiwe kila mwaka tunaomba chakula kutoka Thailand wakati tunao uwezo wa kupata chakula hapa hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, leo ninapozungumza na wewe katika Bunge lako Tukufu, wajanja wapo mashambani wanachukua chakula wanakwenda kukiuza nje, mahindi tunayotegemea kuwa tunaweza tukaweka hapa tukayatunza sasa hivi yanachukuliwa kiholela kupelekwa nje kwa ajili ya kuuza.

Mheshimiwa Spika, mchele wetu mzuri wa Kyela wajanja wapo maporini, sisi wenyewe tupo wapi? Ni wakati muafaka tuanzishe bodi za mazao mchanganyiko, *Grain Marketing Board* ili angalau chakula cha wananchi kiweze kununuliwa na kiweze kuhifadhiwa kitusaidie katika msimu wa njaa. Tunaambiwa kuwa mwaka huu hatutegemei kupata chakula kutoka nje: Je, mtindo wa kupeleka chakula nje, sisi wenyewe tutabakiwa na nini humu ndani?

Mheshimiwa Spika, tuwe waangalifu katika hili, Kamati za ulinzi ziangalie, *Custom* waangalie hiki chakula kisipelekwe nje wakitegemea baada ya muda mfupi Tanzania tutakuwa katika hali ngumu sana ya njaa, kweli ni masikitiko makubwa lakini tuyarekebishe yanawezekana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni la vijana. Sasa hivi Tanzania tunahangaika na vijana ili angalau wapate ajira, lakini wanasumbuliwa sana na wamachinga, kumeingia wamachinga wa Kichina katika nchi hii, lakini tunawaona na kuwaacha. Je, baada ya muda mfupi tutasema nini kuhusu hili suala? Wachina wanakuja hapa wanawekeza kuuza karanga Kariakoo, Wachina wanauza Mamantilie Kariakoo. Je, huu ndiyo uwekezaji? Tutafute mazingira mazuri ili vijana wetu watafutiwe kazi za kufanya, isiwe kutegemea watu wa nje wanakuja kuchukua nafasi za wafanyabiashara wadogo wadogo ituweke katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, hili pia linawezekana watu wa uhamiaji waangalie: Je, hawa wamekuja katika njia gani? Tusije tukawafukuza Wazaire tu na tukawaacha Wachina wamejazana Mjini hapa na makabila mengine kutoka Asia yanachukua nafasi za vijana wetu ambao tungeweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kutoa duku duku kidogo. Nilikuwa nachangia Muswada wa Nishati na Madini wakati tupo Dar es Salaam, nilieleza jinsi watu wanavyotumia vibaya *areas* zetu kwa ajili ya ubadilishaji wa mafuta ya *petrol*, wanachanganya na mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Kurasini kuna mfanyabiashara anayefanya biashara ya kubadilisha mafuta. Mimi nilizungumza kama hoja katika Bunge, lakini alinitishia mpaka kupitia katika vyombo vya habari na kusema atanichafua. Lakini kwa bahati nzuri watu wa vyombo vya habari, wakaniambia Mama tunakuona upo *very innocent* kwa hili, hatuwezi tukakuchafua. Kwa nini hawa wafanyabiashara wanafanya hivi? Wakiharibu vitu vyao tukihoji wanasema watatumia vyombo vya habari kutuvuruga!

Mheshimiwa Spika, tusikubali hili suala kwa sababu ni suala la hatari sana kuvurugiana maisha katika kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie machache katika mjadala huu wa Mapato na Matumizi kwa ajili ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa juhudi zake za kuhalalisha na kutengeneza Bajeti inayokidhi ustawi na maendeleo ya nchi na inayoendana na matakwa ya Katiba ya kutekeleza Serikali ya Ujamaa na Kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile nimpongeze Rais wetu - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa juhudi zake za utawala bora na kusimamia diplomasia ya uchumi ambayo inasaidia kuwezesha nchi yetu kupata misaada kutoka nchi mbalimbali na pia kupata wahisani ama wafadhili na wawekezaji katika nchi yetu. Mungu amjalie heri ili aweze kuendeleza hayo katika Serikali yetu na wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda pamoja na Wajumbe wa Kamati yote kwa juhudi walizofanya za kuchambua kwa maslahi ya nchi na kuhakikisha kwamba bajeti yetu inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, hapa tupo katika majadiliano, bado haijapitishwa kuwa bajeti ya Serikali. Mipango yote iliyoelezwa ni mizuri sana, lakini naomba kusema machache yafuatayo ili yaweze kuzingatiwa katika bajeti ya Taifa kwa sababu bado tupo katika majadiliano.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri wa Fedha akumbuke kwamba toka mwaka 2006 niliwasilisha maombi kwa Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Mramba wakati akiwa Waziri wa Miundombinu. Tulizungumzia masuala ya matengenezo ya barabara na vilevile niliwasilisha maombi ya kuboresha masuala ya maji na yote haya yakapitia kwa Mawaziri na kuhakikisha kwamba tunaweza kupata misaada inayostahili.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atusaidie kuelewa wananchi wa Wilaya wa Maswa kwamba atatusadia vipi kukamilisha miradi ya maji kama alivyosema katika hotuba zake na mwongozo wa maelezo aliyotoa kwamba bajeti hii itakamilisha mahitaji ya miradi ambayo iko tayari inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kiasi cha shilingi bilioni 1.2 katika kukamilisha mradi wa maji wa bwawa la Maswa ili tuweze kuwa na chujio, madawa na tuweze kufanya ununuzi wa vifaa vya kiufundi ambavyo vitasaidia kusambaza maji katika mfumo wa maji ambao tayari umekuwa ni chakavu kwa muda wa miaka mingi. Kwa hiyo, naomba Waziri wa Fedha atusaidie kuelewa ni jinsi gani tutakamilisha mahitaji ya shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya mradi wa maji.

Mheshimiwa Spika, vilevile namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atueleze atatusaidia vipi kukamilisha mradi ambao una nguvu kazi za wananchi na umeshachangiwa visima, ambao tunahitaji shilingi milioni 700. Ninaomba ushauri wake kwa sababu dhamira ya bajeti hii ni kuhakikisha kwamba tunakamilisha miradi iliyoanza.

Mheshimiwa Spika, nauliza haya kwa sababu Wizara ya Fedha ndiyo fungamano na kufaulishwa kwa Wizara zote kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile kukumbushia kwamba, katika hotuba ya Waziri wa Fedha, alisema Mikoa iweze kubuni fursa mbalimbali za kuchochea ustawi na maendeleo ya jamii. Ninamwomba Waziri wa Fedha kwa kuzingatia kwamba toka mwaka 2006 niliwasilisha ombi la pesa kwa ajili ya viraka kwa ajili ya kutengeneza barabara ili barabara zipitike, kilometa 291.7. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha anisaidie kuwaambia wananchi wa Maswa kwamba mradi huu ataukamilisha vipi? Kwa sababu malimbikizo yanapozidi, gharama zinakuwa kubwa. Hivi sasa tunahitaji kiasi cha shilingi bilioni 1.8. Kwa hiyo, naomba Waziri wa Fedha atusaidie kutufahamisha hili.

Mheshimiwa Spika, hizi ni gharama ambazo zilifanyiwa mchanganuo chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Mramba wakati akiwa Waziri wa Miundombinu. Ninaomba, kwa kuwa Serikali haijabadilika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atusaidie kuelewa kwamba ufungamano wa kauli zinazotolewa na Mawaziri pamoja na mabadiliko yanayotokea zinatekelezwa vipi?

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile kuthibitisha kuwa barua ya kukumbushia Serikali iliwasilishwa tarehe 27 Desemba, 2007 Serikalini kupitia kwa Mheshimiwa Dr. Shukuru ambaye alikuwa ni Waziri wa Maji na sasa ni Waziri wa Miundombinu, ikikumbushia matatizo ambayo yanasababishwa na mvua nyingi hatimaye barabara zinakuwa hazipitiki.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atusaidie kuelewa udharura ambao unaweza kukamilika hivi sasa katika bajeti hii ambayo bado haijafungwa

kuzingatia na kuunganishwa, inakuwa na kitungo cha kuchochea ukamilifu na utimilifu wa mahitaji ya kutengeneza barabara za Maswa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababu ni mtu hodari na mbunifu na historia yake inathibitisha uzalendo toka akiwa Mkurugenzi Mkuu wa *NSSF*. Alifanya maajabu na sifa zote za *NSSF* hadi leo tunaziona. Ninamwomba Waziri wa Fedha huyu huyu, sasa anisaidie kuunganisha fungamano la ujuzi wake na maarifa yake pamoja na mamlaka yake na ninaiomba Serikali itusaidie wananchi wa Maswa ili na sisi tujue kucheka. Anayejua kulia anajua na kucheka. Aaomba sasa mtusaidie watu wa Maswa tuanze kucheka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile kutumia fursa hii kutoa rai kwa Waziri wa Fedha kwamba wakati umefika tuhamishe michango inayotolewa na viongozi wetu wa Kitaifa. Humu ndani tuna Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ni Mbunge mwenzetu ambaye nina uhakika hawezi akasimama hapa akazungumzia matatizo ya barabara, matatizo ya visima vya maji na tunaye Mheshimiwa Spika ambaye vilevile hawezi akajisemea. Tunaye Mheshimiwa Naibu Spika! Nadhani wakati umefika tujaribu kuwa wabunifu. Sio lazima tusubiri kuambiwa kwamba Waziri Mkuu ndiye tunamtegemea kutembelea Majimbo yetu, kutuona huko na kutusaidia mahitaji ya Majimbo yetu.

Mheshimiwa Spika, anahangaika Kitaifa na Kimataifa kuboresha majukumu ya Wabunge na uwezeshaji wa Wabunge. Nadhani tusiwe na choyo, tukubali kwamba mcheza kwao hutunzwa. Basi Waziri wa Fedha pamoja na Mawaziri wenzako mtazame kwa jicho la huruma mahitaji ya Wabunge wenzetu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba vilevile kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wakati nampongeza kwa dhamira zake nzuri, atusaidie kufaulisha kupata msako wa maisha bora Maswa na hasa tunapozungumzia bajeti hii, kwamba wakati umefika itusaidie angalau *ambulance* tatu. Nasema hivyo kwa sababu mraba wa Jimbo la Maswa ni kilometa 3,400 ni sawa na Majimbo matatu kwa viwango vya Taifa vya kutenga Majimbo.

Mheshimiwa Spika, kweli pana kilio cha kila siku kwenye magazeti kwamba kuna vifo vya imani potofu. Lakini: Je, Serikali ina juhudi gani za kupambana na vifo vinavyotangazwa kwamba ni vya imani za uchawi, ikiwa kijijini tunategemea mkokoteni wa ng’ombe kilometa 60, unatoka Ipililo kwenda Maswa Mjini, Hospitali kumpeleka mzazi, mtoto kazidiwa hana damu, atafika salama ? Ninaomba Serikali ithubutu kutuondolea tatizo hili. Nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha uwe na huruma ambayo ndiyo stahiki yako na ndiyo uungwana utusaidie katika *initial* ya bajeti hii kutuondolea adha ya mauaji ama vifo vinavyosemwa vinatokana na imani potofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo matatizo ya kijamii, lakini hayo yanaweza yakaondolewa ikiwa vile vile miundombinu itakuwa inaboresha mustakabali wa ustaarabu na maendeleo. Hotuba ya Waziri wa Fedha ina changamoto nyingi sana. Ina changamoto, kwa mfano imetoa mwongozo wa jinsi gani bajeti hii inatarajia kuibua msako wa maisha bora. Sasa msako wa maisha bora kwa Maswa sijui tutawapata vipi?

Wizara inazungumzia kuimarisha huduma zilizoanzishwa katika vipindi vilivyopita. Naomba kukumbusha ya kwamba tarehe 5 Oktoba, 2007 Maswa tulikuwa na ugeni wa Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, tulikuwa na ugeni wa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na tulikabidhi kuhusu mahitaji yetu ya maji, wakati huo ilikuwa ni shilingi milioni 700. Naomba Waziri wa Fedha atusaidie hilo. Je, tunapeleka jibu gani?

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuimarisha zao la pamba. Zao la pamba kwa kweli linakuwa kama ni zao la yatima. Bodi ya pamba imeomba iweze kufaulisha usimamizi wa zao la pamba, lakini mahitaji yake hayajakamilika. Sasa hivi kule kuna mfereji wa kudhulumu wakulima wa pamba. Naomba Bodi ya Pamba ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mchango wa pamba ni mkubwa sana katika nchi hii. Naomba Serikali ilitazame kwa jicho la huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo vile vile la kuimarisha huduma za jamii linalosababisha kutokupatikana kwa walimu. Hatuna maji safi na umeme. Shida hii sasa inasababisha walimu hawaji Maswa, wanakimbia! Ningeomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha apate muda ili niweze kuja kukukabidhi takwimu na mahitaji stahiki hasa kwa sababu muda hapa hautatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nawapongeza ndugu zangu wa Kusini. Mimi nimezaliwa Masasi, ninaomba sasa gesi itakayopatikana iwe kwa maslahi ya nchi. Muangalie kwamba wasizuke vizuka ambao watakuja kusadikisha uongo kwa uongo wa kusadikisha pafumuke miradi ya ajabu. Tuna matatizo Buzwagi, ninaomba mtuunge mkono na ninaiomba Serikali, tulitafuta uhuru ili tukomboe wananchi wetu. Sasa fidia zinazotolewa haziendani na dhamira ya kutafuta uhuru na kwamba sheria ni zile zile za mkoloni. Jamani, naomba mfute wananchi wapate stahiki za fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pana matatizo ya hizi simu za mkononi. Kodi ziangaliwe upya ili ziendane na ushindani na kuvutia wawekezaji. Hivi kwa nini Kenya wana asilimia tano katika pato la Taifa linalotokana na simu? Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha ayatazame hayo kwa makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuelezea takwimu za vifo vya watoto. Watoto wanakufa sana Maswa kwa ugonjwa wa Malaria, *mortality rate* iko 221 kwa watu 100,000, kitaifa ni 529. Kwa hiyo, naomba kabisa Mheshimiwa Waziri wa Fedha aelewe kilio cha kurekebisha na kuimarisha huduma ya afya. Naomba kwa sababu yeye ndiye fungamano na mgao kwa Wizara zote pamoja na kwamba nitazungumza katika Wizara husika. Ningeomba sana takwimu hizi utusaidie kuimarisha na kuboresha uhai na ustawi na maisha ya wananchi wa kijijini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba muelewe kanda ya Ziwa Mkoa wa Shinyanga, hivi vilio vya kuambiwa kila siku kwenye magazeti pana vifo vya imani potofu, ninaomba muelewe tuna kiu ya ustawi na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kuna nchi masikini na kuna nchi tajiri. Kwa hiyo, nchi tajiri hubeba nchi maskini sana. Wilaya duni kwa ustaraabu na maendeleo naomba zibebe kwa upendeleo na naomba Wizara zinazobeba majukumu hayo zifikiriwe upya katika unganisho la mgao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kwa kusema ya kwamba nawaomba Mawaziri wote pamoja na Waziri wa Fedha na namwomba Waziri Mkuu, nawaomba sana waelewe sana sisi tuna kiu ya maendeleo Maswa. Lakini bajeti ndiyo mbolea ya kuchochea ustawi na maendeleo ya jamii. Kwa hiyo, ninaomba viongozi wa Serikali wasije wakawa kama mawe ambayo yako baharini, hayajui kiu ya mtende ulioko jangwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MWANAWETU S. ZARAF:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia siku hii ya leo. Kwanza ningependa kutoa pongezi kwa bajeti mbadala ya kambi ya Upinzani ambayo imesomwa hapa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Pamoja na yale yote ambayo wamechangia wengine kuhusu hali halisi ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kuelezea tatizo nililokuwa nalo. Mimi kama mimi au Mbunge wa Mkoa wa Lindi, katika kipindi kilichopita katika Bunge hili hili ilielezwa kwamba vikao vya *RCC* na vile muhimu vyenye uamuzi kuhusu mambo yanayotendeka katika Mkoa vifanyike wakati Wabunge wakiwa kule, yaani ina maana kwamba Wabunge tushiriki katika hivyo vikao. Lakini vikao hivi vimekuwa ni tofauti kwa Mkoa wa Lindi.

Huu ni mwaka wa pili sasa, sisi Wabunge wa Mkoa wa Lindi tunashindwa kushiriki kwa sababu vikao hivyo vinakwenda sambamba na vikao vya Bunge.

Kwa mfano, sasa hivi Mkoa wa Lindi ndiyo wafanya juzi juzi wakati sisi tuko hapa Bungeni. Kwa kweli tunashindwa kutoa maamuzi haya. Lakini nini sababu, mimi nafikiri Mkuu wa Mkoa anafikiria kwamba tukiwepo sisi tutakuwa tunatoa maamuzi ambayo anataka ayatoe yeye kwa sababu ana kawaida ya ku-*monopolize* maamuzi, anataka yeye maamuzi yake ndiyo yawe. Kwa hiyo, wakiwemo Wabunge wa Mkoa wa Lindi katika mkutano huo anajua yale maamuzi ambayo siyo sahihi sisi tutapinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri Mkuu atueleze au awafahamishe Wakuu wa Mikoa na sisi tunahitaji kushiriki kwa sababu maendeleo ya Mikoa yetu ni muhimu kusikiliza na kuweza kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina suala lingine kuhusu ufuta. Katika Mkoa wa Lindi mwaka huu ufuta umekuwa ni mwingi na bei imepanda zaidi ya asilimia 100. Lakini mwaka 2007 ufuta ulikuwa ni Sh. 650/=, mwaka huu ufuta unauzwa Sh. 1,300/= kwa bei ambayo amepanga Mkuu wa Mkoa kwa Chama cha Ushirika. Mimi nilifikiria biashara ni

huria katika kununua mazao ya wakulima, lakini mwaka huu naona kwa Mkoa wa Lindi imekuwa ni tatizo, hasa Wilaya ya Kilwa. Siwezi kuelewa maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kama ni ufuta umepanda asilimia hiyo na yupo mfanyabiashara ambaye yupo tayari kununua kwa Sh.2,000/= au Sh. 1,800/= au Sh.1,400/= Mkoa kwa nini ukataze wafanyabiashara wasinunue huo ufuta, badala yake kinunue Chama cha Ushirika tu cha Mkoa wa Lindi cha Ilulu na hawa wafanyabiashara wasinunue kwa bei ambayo iko juu ya ile ambayo imepangwa na Mkoa? Bei ya Mkoa ni Sh. 1,300/= lakini wapo watu ambao wananunua huo ufuta kwa Sh. 1,400/=, Sh. 1,500/= hadi Sh. 2,000/= na ambaye amefikia bei ya Sh. 2,000/= ni *Mohamed Enterprise*.

Lakini hili limekuwa ni tatizo! Wafanyabiashara wakinunua, hawapewi vibali vya kusafirisha mazao yao. Mkulima anapotaka yeye mwenyewe akauze, pia anazuiwa. Hivi leo kuna magari ya wakulima ambayo yamekwamishwa Kilwa kwamba hayawezi kusafirisha huo ufuta na kibali wamewapa, wamewaeleza kwamba kibali wakirudishe Halmashauri watawalipa fedha zao. Je, usafiri waliochukua hawa wakulima ambao wameshalipia watawarudishia? Mimi naona hatutendewi haki katika Mkoa wa Lindi na hili ndiyo maana Mkuu wa Mkoa hapendi sisi tukae kwenye maamuzi ya hivyo vikao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina suala lingine kuhusu huo huo ufuta. Hapa Dodoma ufuta sasa hivi unauzwa shilingi 1800 mkulima anayeshika mkononi. Kwa nini mkulima wa Kilwa asiweze kuipata shilingi 1800 au 2000 ambayo wengine wamepanga bei yeye mwenyewe? Mimi naona haya yote ni maonevu.

Kuna tatizo lingine ambalo pia wenzangu wa Mkoa wa Lindi wametangulia la kuhusu mibono, kweli wawekezaji tunawataka, tunapenda waje. Kuna mwekezaji amewekwa Mkoa wa Lindi katika kijiji cha Mavuju, ni eneo kubwa la karibu hekta 14,000 amepewa lakini kabla hatujaona matokeo ya mibono hii kwamba imeleta tija gani kwa wananchi wa Kilwa, amepewa maeneo mengine ya vijiji; Kijiji cha Migelegele, Liwiki na Kijiji cha Nainoke. Amepewa tena hayo maeneo, mimi naona huu ni ubadhirifu kwa sababu kabla hatujaona matokeo ya hii mibono ambayo amepewa hekta 14,000, kwa nini apewe hizo hekta zote ambazo zinafikia karibu 45, 46 wakati hatujaelewa nini matokeo/tija ya wananchi wa Kilwa?

Mheshimiwa Spika, mimi naona hii itakuwa kama *TICS* ya kupewa mkataba wa miaka mitano, kumi akaongezea mpaka ikafika miaka 25. Kwa nini usisubiri mpaka pale utakapoona tija ilipo? Naomba Serikali iliangalie hili suala. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna wengine ambao wamewekeza sasa hivi, ardhi imekuwa ni mtaji na ni mali lakini hawa wawekezaji naona wanataka waihodhi ardhi tu na siyo kwa sababu ya kufanya shughuli ambazo zitaleta maendeleo kwa wananchi. Nikichukulia mfano, Chibuku ilichukua hekari 5,000 katika Wilaya tangu mwaka 1984, lakini mpaka leo hawajaendeleza kitu chochote. Ni kwa nini? Hawa kweli wana nia, baadaye watu wanalalamika kwamba kodi ya ardhi imepanda kutoka 200 irudi chini. Wataonaje

kwamba hii bei ni ndogo au ni kubwa? Kwa sababu wao hawawekezi pale, kwa hiyo, haileti faida, lazima waone kodi ni kubwa. Hili pia liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, hili limekuwa tatizo kwa Kilwa kwa sababu Kilwa kuna ardhi ni kubwa, nzuri na watu wote sasa wamekuja kuhodhi ardhi katika Wilaya ya Kilwa. Naomba hili liangaliwe kwa sababu Rais alipofika Kilwa alituambia tuangalie kutoa ardhi ovyo. Lakini sio wananchi wanaotoa ardhi ovyo. Hii mikataba na vitu vyote vinaanzia huko juu. Wananchi wanakuja kupewa tu maelezo kama hayo. Naomba hili liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu kuna tatizo lingine la fukwe. Mheshimiwa Mbunge pale amelizungumzia. Kilwa kumezungukwa na fukwe, wananchi wana mashamba yao ya asili. Kwa muda mrefu mashamba haya, Halmashauri sasa hivi wanawaambia wananchi tunapima mji, tunafanya nini, lakini wale hawashauriwi. Ina maana wanawapa watu wengine wamiliki yale maeneo wakati wenyewe wenye maeneo yao ya asili ambayo ni halali hawapewi ushauri isipokuwa wanaambiwa kwamba Halmashauri imeamua kwamba inapima Mji. Mimi naona hawawatendei haki.

Mimi nilifikiria wananchi watashauriwa jinsi ya kumiliki ardhi wamiliki kihalali na kama kuna mwekezaji ambaye anahitaji kuwekeza pale, wapeane ubia. Nadhani Serikali ingefanya hivyo, lakini badala yake hiyo haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado naona kuna utata. Nilifikiria kwamba sisi wananchi wa Kusini tulikuwa katika mstari wa mbele ili kusaidiwa kwa sababu tuko nyuma kimaendeleo. Lakini badala yake naona wajanja ambao wamekuja Mikoa ya Kusini wamekuja kutudidimiza zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina suala lingine kuhusu Jeshi la Polisi pamoja na Magereza. Nimepata malalamiko na nimetumwa kuja kueleza hapa kwamba likizo ya miezi mitatu, yaani baada ya miaka mitatu kwa wao sasa hivi wamechoka nayo na wanashindwa jinsi ya kuizungumzia. Kwa sababu nini maana ya likizo? Ni kupumzisha akili baada ya kazi ngumu na ndio maana wanachukua kila baada ya mwezi mmoja. Lakini likizo ya Polisi, Jeshi la Magereza ni miaka mitatu. Ina maana miaka mitatu bado akili yake haijachoka.

Kwa hiyo, wanaomba hii sheria ibadilishwe ili wao waende likizo kama wanavyokwenda watumishi wengine ya mwaka mmoja na unakwenda likizo mwezi mmoja. Wanashindwa kufanya mambo yao ya kimaendeleo kwa sababu wanakwenda likizo ya miezi mitatu, hata nauli ya kurudia kwao wanashindwa. Fedha wanazopewa muda mwingine hazitimii za ule muda ambao wanatakiwa wawe likizo. Kwa hiyo, wanaomba sana hii sheria ya likizo ya miezi mitatu na baada ya miaka mitatu ibadilishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado narudi tena Mkoa wa Lindi. Tulipoambiwa kwamba tuhamasishe kujenga shule za sekondari, lilikuwa ni suala zuri sana na wananchi walijitolea wenye kuku, waliuza na walitoa Polisi kwa sababu walishindwa kuchangia

michango yao. Kuna shule ya Sekondari inaitwa Nanyanje - Mkoa wa Lindi, imejengwa yapata miaka miwili. Ilikuwa na *Form One* na *Form Two*.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, ameibadilisha ile shule na kuipeleka Chikonji. Usajili unaotumika Shule ile ya Chikonji aliyoipeleka ni wa jina la Nanyanje. Fedha ya *TASAF* ambayo inatolewa ili iende kwenye Shule ya Nanyanje inapelekwa Chikonji. Usajiri wa shule hii mpya haina usajili, inatumia usajili wa Shule ya Nanyanje. Wananchi wa pale wamegoma na wanafunzi walishafikia kidato cha pili, wamepelekwa Shule ya Chikonje ambayo haijasajiliwa, lakini wanatumia jina la Nanyanje. Wananchi wa pale hawataki hii habari na kuna ugomvi mkubwa, wananchi hawana raha, mtendaji hawezi kufika katika Kijiji cha Nanyanje kwa sababu anaogopa.

Mkuu wa Mkoa ameshawahi kwenda pale, lakini kwa Ulinzi. Diwani na yeye pia anashindwa kufika katika ile shule kwa sababu wananchi wamechachamaa.

Mheshimiwa Spika, naomba hili liangaliwe kwa sababu ni kweli wamekwenda kuchukua mabenchi, wananchi wamegomea mabenchi yao, lakini shule imehamishiwa kwingine. Madai ya Mkuu wa Mkoa anasema kwamba shule ile iko porini walimu watakaa wapi? Kwa hiyo, anaibadilisha ili iwe Zahanati. Sasa mimi nauliza, hawa wafanyakazi wa Zahanati watakaa wapi na kule ni porini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo maamuzi ambayo yanamfanya na Mkuu wa Mkoa sisi Wabunge tusiwepo kwenye vikao vyake vya *RCC* vya Mkoa. Naomba Serikali iende kule ikaangalie kwa sababu ni ugomvi mkubwa wa watendaji kutokwenda kule pamoja na mimi kwenda na kuwaambia kwamba watendaji waacheni waende na wamekubali, lakini bado kuna utata, wanaogopa kwenda. Sijui hapa nyuma yangu kama wameshawahi kwenda pale.

Mheshimiwa Spika, hizi ni hitilafu kubwa kwa sababu wao wanadai wamefanya kazi kubwa na wamejenga pale na vijiji vitatu vilikubaliana kwa sababu sasa hivi sekondari zinatakiwa zijengwe sehemu yenye nafasi. Sehemu yenye nafasi ilikuwa ni pale, vijiji vyote vilikubaliana. Sio kosa kuwa na shule mbili katika Kata moja au tatu, kwa nini uifunge hii ambayo imeshakuwa tayari ukawapa wengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuzungumza kuhusu adha tunayoipata sisi wananchi wa Kilwa Mkoa wa Lindi kwa ujumla kuhusu ndovu. Ndovu imekuwa adha kubwa! Mkulima hapati chochote kutokana na hii. Halmashauri inapoomba ma-*game*, wanatakiwa ma-*game* ambao wana *degree*.

Nataka kuuliza, shabaha inahitaji *degree*? Naomba turuhusiwe wale ma-*game* ambao tunao, maana tuna ma-*game* ambao tulikuwa tunawatumia, lakini hawajapata *degree* na hawataki kuajiriwa. Tunaomba waturuhusu waajiriwe kwa sababu upigaji wa tembo hauhitaji kuwa na *degree*.

Ili kuepusha wanyama hawa wasiendelee kutumaliza wananchi wa Kilwa, tunaomba mtoe ruhusu ya kuwaruhusu hawa watu waajiriwe hata kama hawana *degree*.

Huyo mtu mwenye *degree* atakayekwenda kukaa msitu wa Kilwa, nani? Wao wawe washauri tu, lakini mpigaji ndovu wao awe mtu wa kawaida. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuongezea kwenye hii bajeti kwamba punguzo la huduma za simu kwa sababu kukiwa na punguzo la huduma za simu, idadi kubwa ya wananchi watapata ajira.  Halafu vile vile watumiaji watakuwa wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pato la Taifa litaongezeka. Lakini kitendo cha kuongeza kodi ya huduma za simu kinasababisha pia kuwa kukosa hivyo vyote ambavyo vingesaidia Taifa kupata pato kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa leo naomba niishie hapo. Naomba izingatiwe kwamba wananchi wa Kilwa wanahitaji huduma kama wengine na vile vile vitega uchumi vyetu tushauriwe na wananchi wapewe nafasi pia ya kuchangia kile ambacho kinatakiwa wachangie. Isiwe tu kwamba mtu mmoja anachukua maamuzi. Mkuu wa Wilaya amewekwa pale kwa ajili asaidie shughuli za Wilaya na Mkurugenzi ndiyo kazi yake.

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Mkoa yeye ni mkubwa kwa hawa watu. Kwa hiyo, awape nafasi hawa pia watoe ushauri, siyo yeye tu ang'ang'anie kila kitu, awe anatoa ushauri yeye. Mtu anashindwa kusema kwa sababu yuko juu yake hata kama analiona kama hili halifai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuachia hapa nikitegemea haya yatafanyiwa kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sijui kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha ataweza kweli kujibu matatizo kati ya Mbunge na Mkuu wa Mkoa. Lakini, haya! Tunaendelea. *(Kicheko)*

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa leo nimefarijika sana kwa kuona kwamba umekabidhiwa Kadi ya *CUF* ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nafikiri umekabidhiwa kadi tatu, ni bora moja ukamkabidhi Mheshimiwa John Chiligati na moja ukamkabidhi Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ni mwanzo mwema.   *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kadi ya *CUF*…!

**SPIKA:** Bahati  mbaya kadi siyo mpya, zina majina ya wenyewe. *(Kicheko)*

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Spika, *Okay* inaonekana kwamba ni Chama kikongwe hata kuliko CCM basi.  Kuonekana kwamba kuna nembo ya mizani isiwe tatizo kwamba ni nembo ya Kijemshid au Ike-Baragash kwa sababu hata Mahakama Kuu ya Tanzania nembo yao ni mizani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, twende kwenye mada.  Kwa kweli watanzania tuna tabia ya kutafuta vyanzo vya mapato bila  ya kuviendeleza vilivyopo mikononi mwetu.  Ni kosa

kubwa sana! Chukulia mtandao wa simu. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi isikieni.

Mheshimiwa Spika, napenda ninukuu Ilani ya mwaka 2005 ukurasa wa 58 mpaka 59 imeahidi miongoni mwa mambo mengine kwamba katika kipindi cha mwaka 2005/2010 Chama cha Mapinduzi kitaihimiza Serikali kutekeleza mambo yafuatavyo: Kuboresha mtandao wa huduma za simu nchini.

Mheshimiwa Spika, nasoma kwa sababu sio Chama changu, ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, endelea.

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA: "**Kuboresha mtandao wa huduma za simu nchini, kuendelea kupanua huduma za simu za mezani na mikononi hadi ngazi ya vijiji. Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi utategemea sana uwezo wa Serikali kuvutia wawekezaji katika Sekta na watumia huduma kutumia huduma hizo kikamilifu." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, leo simu ni muhimu kama ilivyo reli, kama ilivyo ndege au usafiri mwingine wowote wa binadamu na inarahisisha hata biashara baina ya mtu na mtu, Shirika na Shirika, nchi na nchi kwa sababu ni nyenzo nyepesi ya mawasiliano katika ulimwengu wa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa leo tunaweka *excise duty from seven percent to ten percent*, nani anaumia? Mtumiaji, akiumia atakwenda kwenye *MSG,* akienda kwenye *MSG* mapato yanashuka. Serikali inakosa vyanzo vizuri vya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *twenty percent* ya *VAT* ni kubwa ukilinganisha na nchi za jirani. Kenya wana asilimia 16, Uganda wana asilimia 17, sisi ni asilimia 20, *excise duty* Kenya wana asilimia 10, Uganda wana asilimia 12 na sisi tuna asilimia saba, tunataka tuipandishe mpaka asilimia 10, nani anaumia? Tunaumia wenyewe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tutapunguza matumizi ya simu, tutaongeza idadi ya vibaka wanaonyakua simu kwa sababu watu watakaokuwa wanamiliki simu watakuwa ni wachache. Tunataka Watanzania wote kutokana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi wawe na simu za mikononi. *Excise duty* iondolewe kabisa na *VAT* iteremshwe kutoka kwenye asilimia 20 mpaka kwenye asilimia 15 au asilimia 10 au hata kuondolewa kabisa.

Mheshimiwa Spika, nini faida yake? Zipo nimeziorodhesha hapa, kama mnataka niwambieni, itaongeza ajira katika kipindi cha miaka kumi inayokuja, matumizi yataongezeka kwa asilimia saba na Serikali itapata mapato kwa asilimia kama nane baada ya miaka 10 na mtandao utapanuka kwa asilimia tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki ndicho kitu cha kufanya. Tusitafute jetrofa**,** tukataka kukamua mafuta. Ya nini? Tumejitosheleza kwa mahindi na mpunga. Ulichokuwanacho kihodhi hicho, ukilee, ukipanue kikupe mapato bora.

Mheshimiwa Spika, ninaendelea. Nafikiri leo ungetengua kanuni ungenipa nusu saa. Baba wa Taifa - Marehemu Julius Nyerere, alisema, katika nchi hii, tofauti ya mwenye kuwa nacho na aliyekuwa hana itakapokuwa kubwa ni sawasawa na kuacha petroli kudondoka katika nyumba na mwisho wake ni kulipuka. Tanzania tumefikia hapo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, *gap* baina ya mtu masikini na tajiri ni kubwa sana. Bajeti lazima ilenge maslahi ya wananchi waliotutuma hapa. Sisi tunakuja hapa katika Bunge, kazi yetu kubwa ni kugawanyika katika makundi, kusengenyana, kujenga hoja ambazo hazileti maslahi kwa nchi na hapa tumeletwa kwa gharama kubwa, watu wamekufa, watu wametuchagua walalahoi ambao toka wamezaliwa mpaka leo miaka 50 mpaka miaka 60 hawajui kuvaa viatu katika miguu yao. Leo tunawasaliti! Tunakuja hapa tunazungumza mambo ambayo hayana maslahi na nchi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umasikini ulivyoshamiri siyo tu vijijini, hata mijini kuna umasikini. Lakini tumeandaa mikakati gani ya kuondoa umaskini? Chukua mfano, tumeondoa kodi kwenye Moto Poa, *already* tumekwishaambiwa kwamba ule ni Moto Poa hauna nguvu, umepoa. Hauwasaidii wanavijiji, hauchemshi maji ya sufulia kubwa la *extended family* katika vijiji vyetu na ukaweza kupika ugali wa mhogo au ugali wa sembe. Ule ni moto ambao unamsaidia mtu wa *standard* ya kati na kati, kukaanga mayai, kuchemsha maji ya chai, kuchemsha maziwa, kumtengeneza lakitojeni ya mtoto mdogo. Unakwenda kumpa mtu wa kijijini, jamani hatutoki vijijini, mimi ninatoka katika kijiji cha Kajengo Makunduchi. Ninajua namna tulivyokuwa tukiishi, hatukuishi kwa kutumia majiko ya namna ile. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, jiko lenyewe ni Sh. 38,000/=, gesi ya lita moja ni Sh. 10,000/= ataitumia kwa siku ngapi na atamfikishia nani kijijini? Kiberiti chenyewe cha kuwashia gesi ukazima kila mara ni Sh.50/=, hakimiliki vijijini wanagawiana moto. Huko vijijini ndivyo wanavyoishi. *This is reality*, kwa nini tufichane? Hili siyo suala la CCM wala la Upinzani ni suala la Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unachukua gesi unaiondolea ushuru, mtungi wa gesi ule mdogo kama mtu yupo Masasi unavyomalizika inabidi akaifuate gesi Mtwara kilomita 120 kwenye ku-*refill* mtungi wake. Kama ni Maswa aifuate gesi Mwanza kilomita zaidi ya 100, kama ni Turiani aifuate Morogoro zaidi ya kilomita 50 au 60, kama ni Makunduchi mpaka aje Mji Mkongwe ndiyo apate gesi. Sasa tunafanya nini?

Mheshimiwa Spika, ili kulinda mazingira, *solution* siyo gesi hiyo, wala siyo *jeli* wala siyo Moto Poa. Kuna Wizara lazima tuilazimishe Serikali ku-*subsidy* tuoteshe miti. Kulikuwa na operesheni huko nyuma ya kata mti panda mti; siyo panda mti, panda miti. Panda miwili, mitatu. Mmoja ukifa miwili ina-*replace*. *(Makofi/Kicheko)*

Tumefanya *research* katika Jiji la Dar es Salaam, lina wakazi milioni nne, wanatumia tani ngapi kwa mwaka? Tumeondoa kodi ya Moto Poa na gesi na tufanye *research* mwaka huu halafu twende mwaka wa pili tukafanye *research* ya pili, kama tutaona kuna punguzo la matumizi ya mkaa, hakuna! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hayo kidogo niliyokuwanayo naweza nikaelezea yakawa ni matumaini kwa Watanzania. Kuna tatizo moja kubwa sana, kwamba tuna *concept* kwamba Wapinzani ni maadui. Wapinzani wanataka nafasi za CCM, hapana! Sisi sote tumekula kiapo kimoja kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka *Senegal West Africa*, Abdul Waye Wade alipomshinda Abdioup, kabla ya kutunga Baraza lake ikawa kuna Mkutano Paris Ufaransa wa nchi zinazozungumza Kifaransa, akamwambia Abdioup, niwakilishe, na ni mpinzani wake na amemshinda na Abdioup akatoka akaenda Ufaransa. Ule ndiyo utamaduni wa siasa za Kiafrika. Unyonge wetu, tufanyeni kazi pamoja. Kaeni na sisi tukupeni vitu, tuokoe jahazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna ubaya. Mimi ni Mtanzania kama wewe. *The only difference* na ambayo iko hata ndani ya *Quran* ni ngozi tu hii, ngozi tu basi. Mimi ni *fare complex*, mwingine ni mweusi, mwingine ni *brawn*, lakini *we are all Tanzanians. We have to work together for the benefit of this nation. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna vyanzo ambavyo tumeviacha. Kuna Mgololo *Mufindi Paper Mill* kule tumeiacha. Mufindi Njombe kuna *growth* ya miti mikubwa kuliko hata Europe. Nenda Norway ambao wanatengeneza mbao nyingi, wanatoa karatasi nyingi, lakini sisi tunawashinda kwa *growth* ya miti. Miti kwao inachukua mpaka *fifty years* kuweza kupata *maturity* ya kutoa mbao na kutoa karatasi. Sisi *only five to ten years.* Kwa nini? Jiulize. Kwa sababu Europe wana-*practice winter all times, spring.* Sisi tuna-*practice only two weathers.* Utaona kwamba na miti yetu inapata *sun light* kwa muda wa miezi sita mpaka saba, *growth* yake inakuwa kubwa. Kwa nini tusikiendeleze kile kiwanda? Tumekibinafsisha, sijui anafanya nini?

Mheshimiwa Spika, kiwanda kile kilikuwa *one of the greatest industry in the Southern Part of Sahara.* Kilikuwa kitosheleze karatasi za Tanzania nzima na ku-*supply* nyingine za Kiafrika. Hii kengele ilikuwa inizuie kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, leo gazeti halimfikii mwanakijiji. Tuondoleeni kodi kwenye redio na mawe ya redio ili wananchi vijijini watusikie, nani walanguzi, nani wala rushwa, nani mafisadi, watusikie kule! Leo gazeti Sh. 300/=, twende kwa hawa wanaochapisha magazeti, wanachapisha magazeti mangapi kwa siku? Yanatosheleza hata Dar es Salaam! Yanatosheleza hata Dodoma? Lakini kutokana na bei, tunashindwa kununua gazeti, tukapata *information* na ni kitu muhimu katika nchi kuweza kujua nchi yako inaandaa nini, iko vipi, mnaweza kunyanyua uchumi namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kuhusu misamaha ya kodi. Inasikitisha kweli kweli! Kwanza nani aliye-*authorize,* wale ndugu zetu wa *TRA?* Wanatukusanyia pesa nyingi tu! Sisi namna ya kuzitumia tunazitumia hovyo hovyo. Wale ndugu zetu wanasamehe watu sio kwa amri zao. Inaonekana kuna amri za wakubwa wanapeleka vi-*note* ili watu wasamehe kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano mmoja mzuri, kama kusamehe kodi, tusamehe viwanda vya ndani, kuna *General Tyre*, mipira inatoka Korea, Malaysia, India, Uingereza. Wale ndio wa kupunguziwa kodi tukavilinda viwanda vya ndani ili ajira ipatikane, *production* iwe ya ndani, mipira tutumie yetu. Sasa kina maana gani kuwepo pale? *(Makofi)*

Kuna *TANALEC* inatengeneza mpaka *transformers* ambazo tunaweza tukauza Msumbiji, tukauza Zambia, Malawi, *the only place is Tanzania in South Africa,* kwa nini tusiwape *subsidy* wale? Kwa nini tusiwapunguzie kodi wale? Leo kodi iliyosamehewa Zanzibar ni shilingi bilioni 19.6. Ni dola 16,333,333.30, kwa *rate* 1,200 ya leo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha zile tungeweza kununua *generator* za *standby* Zanzibar ambazo zinatoa *megawatts* 35 wakati matumizi yetu sisi Zanzibar ni *megawatts 40,,* isingekuwepo hali ile iliyojitokeza. Matokeo yake tumekaa mwezi nzima, nchi ime-*freeze.* Vijana hawana kazi, umeme hamna, *security* mbovu, watalii wamekimbia, pesa zile shilingi bilioni 20 tungeweza kununua hii na tuna uwezo wa kununua. Tungeweza kununua *generator tatu* au mbili, kwa sababu ukileta moja ni *7.5* kwa mbili inakuwa 15 na zile dola milioni 16. Nani anatoa vibali vya kusamehe kodi, ukasema kwamba mchele unatolewa msamaha wa kodi ili ushuke chini, mchele haushuki chini! Mnajua athari yake nini? Kwa sababu anayesamehewa kodi inaonekana anaambiwa tunakusamehe, lakini kuna 10%, 20% na 30%. *(Makofi)*

Yule anayesamehewa anasema, mimi nataka kurejesha. Utakuta msamaha umetoka, kodi iko pale pale! Tusamehe viwanda vya ndani. *CocaCola coverage* yake ya *business* katika Tanzania ni asilimia 80, *just imagine 80%* ya *population* ya *40 million* wanauza chupa za *CocaCola* ngapi kwa kutumia maji yetu? Wale sio wa kusamehewa kodi! Wale wa kuonyesha maendeleo katika nchi na hawa simu ndiyo wa kusamehewa kodi. Hawa siyo wa kusamehewa kodi. Kwa sababu kodi zao wanapokuwa wanasamehewa wanazichukua wanakwenda ku-*invest* nje, wananunua hisa nchi za nje. Lazima tuwe makini kuwatumikia Watanzania, *other wise* 2010 haiko mbali. *(Makofi)*

Sio mimi, sio wewe tutapoteza *six* na si hasha mwaka 2010 mkatoka huko mkaja huku sisi tukaja kule. *Yes, definitely*. Kwa nini kisiwezekane, hawa wanaoondoka wameondoka vipi? Mimi nakwambia sentensi yangu ya mwisho iwapo kuanzia leo kwa muda wa siku 90 kama utaitishwa uchaguzi bila ya kupiga kampeni, basi tutachukua Serikali. *(Kicheko/Makofi)*

Hamna mwelekeo, mmeshagawika, hamfanyi kazi kwa maslahi ya nchi, mnafanya kazi kwa maslahi binafsi na hakuna kitu kibaya kama hicho. *Too big enemies*

katika mwili wa binadamu ni *fats and sugar* na *too big enemies* katika *governance* yake ni *corruption.* Mtajiju!

Mheshimiwa Spika, ahsante sana *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanya, neno utajiju siyo sahihi katika Bunge. Namwita Mheshimiwa Chacha Wangwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Lyima na kwa jioni hii nadhani tutamalizia na Mheshimiwa Anna Abdallah. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuzungumza katika Bunge lako Tukufu na inavyoelekea kuna mengi ya kuzungumza. Lakini ningependa tu kuzungumzia katika suala la bajeti tuliyonayo. Hii bajeti tuliyonayo imeshaonekana ina dosari nyingi na nisingependa kuzirudia kwa sababu wenzangu wengi wa upinzani na hata wa Chama kinachotawala wamezungumza. Ila ningependa tu kuwakumbusha kwamba inafedhehesha sana kuona Wabunge tunasimama hapa na kuzungumzia kuhusu dosari zilizopo kwa dakika 15 halafu baadaye unasema kwamba unaunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo jambo wananchi hawalielewi kabisa. Hiyo ni falsafa ya Chama cha Mapinduzi ambayo ni mpya kabisa katika *tradition* ya Mabunge. Kama unapinga, unapinga, kama unakosoa, unakosoa. Sasa hii ya kusema kwamba dosari ni hizo nyingi sana, lakini ninaunga mkono mia kwa mia, inamahanisha nini? Ina maana hawa waliokuwa wanasikiliza wao hawana namna ya kuweza kuelewa. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, ninavyoamini ni kwamba hili Bunge lingekuwa ni Bunge moja la nguvu la kuleta mabadiliko katika nchi yetu. Kwa sababu Wabunge wengi humu ni wa Chama cha Mapinduzi. Kama kweli wangekuwa na nia ya dhati ya kutaka kuleta *changes* katika nchi yetu na kupinga vitu kama ufisadi kwa moyo mmoja kama ambavyo sasa hivi wanaelekea kufanya baadhi, akina Mama Malecela wanazungumza. Wanaapa kwamba wao wako tayari hata kufa. Lakini mimi *I don't believe!* Mimi sidhani kwamba Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wako *serious.* Kwa sababu mambo kama haya ambayo sasa hivi yanakabili Taifa letu, kitu kama *corruption* ni kitu ambacho kinapingwa ulimwengu mzima. Lakini kuchukulia hatua wananchi wakaona ya kwamba kweli kuna dhamira ya dhati imeshindikana. Basi hapo mimi ndio ninaposema, ni kwamba hii Bajeti kwanza imekiuka misingi yote ya uchumi.

Nasema hivyo kwa sababu katika sayansi ya uchumi, kuna kitu kinaitwa *land, capital, labour*. Hiyo ndiyo misingi ya uchumi, ardhi, mtaji na nguvu kazi. Hakuna kitu ambacho unaweza kugundua zaidi hata baada ya miaka 1,000, hizo ndiyo *factors.* Ndiyo vitu vinavyotumika kutengeneza uchumi. Sasa ukiangalia sisi tumeshindwa kuelewa kama tuko katika mfumo gani wa uzalishaji *model of production.* Kwa sababu kuna *model of production* ambayo tulikuwanayo na ambayo katiba inaongea kwamba tunayo. Inasema ya kwamba tuna mfumo wa ujamaa. Katiba inasema kwamba tuna mfumo wa ujamaa na kujitegemea. Katika ibara ya tatu, Jamhuri ya Muungano ni nchi ya kidemokrasia na ya kijamaa isiyokuwa na dini, yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Sasa kama tunafuata *socialist model of production*, wapi *state planning?* Lakini sasa kwa sababu ya mabadiliko ambayo yanaonekana wazi ni kwamba tunaelekea kwenye mfumo wa ubepari. Lakini pia hata katika mfumo wa ubepari tunahitaji kuwa na *production. Production* yenyewe ni kwamba ardhi ndiyo msingi. Vitu vyote vinatoka kwenye ardhi. Halafu *capital* ikishawekwa ule mtaji, basi tunakuwa na uzalishaji na katika uzalishaji tukishindana na nchi nyingine sasa tunauza vitu vinavyotokana na ardhi na viwanda vyetu. Lakini sisi ardhi tumeiachia, tumewatupa wakulima na sasa hivi ardhi yetu inagawiwa kwa watu hovyo. Hii ndiyo nchi ambayo inatoa ardhi bure. Kwa hiyo, tunatengeneza Zimbabwe nyingine hapa.

Kwa sababu kama tuko mahali ambapo mwananchi wa Tanzania hana ardhi na hana haki ya kumiliki ardhi, halafu wageni wana uwezo wa kuja na kuchukua ardhi wanavyopenda, walime mibono, wanachukua maeneo yenye viwanja vya madini. Mbuga za wanyama zinachukuliwa wanavyopenda. Hayo yote yamekuja kukutana katika Mkoa wa Mara. Leo watu wanakufa katika Mkoa wa Mara kutokana na fujo, zilizotokana na makosa yaliyotokana na *policy* za Serikali. Serikali inawaangalia inasema hawa wako hivyo, hawa wana mila ya kupigana. Kuna watu wenye mila ya kupigana duniani kweli! *(Kicheko)*

Wanadamu watapigana wanapokuwa na sababu ndiyo maana ukienda kule Mashariki ya Kati, Wapalestina wanapigana na Israel kuhusu ardhi na hata Wapalestina wenyewe kwa wenyewe, sasa hivi wanapigana kwa sababu zao. Juzi Afrika Kusini sio Waafrika pale wamepiga Waafrika wenzao, wale walikuwa ni Wakurya! Wanapigania maslahi, wanapigania *space.*

Mheshimiwa Spika, pale Dar es Salaam kuna makabila mawili, sijui ni makabila sijui ni koo mbili zinapigana kila siku zinatoana damu, ndani ya mji wa Dar es Salaam. Upande mmoja kuna Wamachinga, upande mmoja kuna Mgambo. Wanapigania *space. (Makofi/Kicheko)*

Unataka kuniambia wale ni Wakurya wamehamia Dar es Salaam kupigana wenyewe kwa wenyewe? Watu wenye shida kubwa sana ya ardhi sasa hivi katika Tanzania ni wachungaji, wafugaji. Wao ndio wamekuwa *uprooted completely* wanarandaranda nchi nzima unawakuta wamelala kwenye vivuli vya miti ndani ya miji kama Dar es Salaam, Arusha, Kampala na kila mahali. Hivi hamuwezi kuona kwamba ile ni *disaster!* Watu wametolewa katika mazingira yao ya asili ya uzalishaji wao wanarandaranda na ni Watanzania. Wakiingia huko Kilosa wakijitafutia maeneo wanapigana na wakulima. Lakini kule angalau Serikali inachukua hatua inakwenda mpaka hata inamwondoa *DC,* inamwondoa *OCD.*

Lakini Tarime ukikutana na *DC* au ukikutana na Mkuu wa Mkoa, yeye anasema kwamba hawa wako hivyo na lazima waachwe wapigane kwa sababu ni wapinzani. Kwa hiyo, Tarime inateseka kwa sababu ya upinzani. Sasa hivi tumewekewa *blockage.* Umewekwa mpaka, mpaka ule ambao ungekuwa ndiyo wa Kenya umehamia kilomita 100 ndani ya Tanzania.

Kwa hiyo, kuna mpaka uko pale Kirumi, karibu na Musoma na mpaka mwingine uko Serengeti ili mali kama nafaka, mchele, mahindi, maharage yasiingie Tarime. Wakati Tarime sasa hivi kuna hali hiy
o ya vita, watu hawalimi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu, Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu, Kanuni ya 64 Kanuni ndogo 1(a) ambayo inasema kwamba Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Mbunge hapa anaongea juu ya kuhamishwa kwa mpaka kutoka mpaka wa Tanzania na Kenya mpaka Mto Mara. Hizi taarifa siyo za kweli. Naomba akanushe na afute.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Kwa Kiswahili mpaka ni kitu tofauti kabisa. Sijui huyu Mheshimiwa alikuwa na maana ya *road block.* Kama ni mpaka, basi sio kweli kabisa, kwa sababu nchi yetu wala haijapungua kwa kiwango hicho. Kwa hiyo, nadhani sio sahihi na ni lazima urekebishe na kufuta usemi huu.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ni bora nirekebishe kwa kusema ya kwamba Katiba yetu katika sehemu ya kwanza inasema kwamba kusiwe na ubaguzi wa aina yoyote. Ninazungumza hivyo kwa sababu Katiba inaposema katika ibara ya 12 kwamba ni marufuku kwa mtu yeyote kubaguliwa na mtu au mamlaka yoyote inayotekeleza madaraka yake chini ya sheria yoyote na au katika utekelezaji wa kazi au shughuli yoyote ya mamlaka ya nchi nili-*base* hapo nilipokuwa namaanisha kwamba unapofunga barabara na kuzuia chakula kisiende katika eneo moja la nchi, hakiendi...

**SPIKA:** Wewe umesema mpaka Mheshimiwa...

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kwa sababu, sababu anayoitoa Mheshimiwa ni kusema kwamba chakula kinakwenda Kenya. Kwa hiyo, *road block* badala ya kuiweka Sirari mpakani anaiweka kilomita 100 ndani na kuzuia chakula kisiingie kwenye Jimbo langu. Sasa hicho kizuizi cha kuzuia chakula kisiende Kenya, kwa nini kisiende?

**SPIKA:** Mheshimiwa Chacha unafuta ama hutaki? Kwa sababu suala la mpaka wa nchi ni suala la mamlaka ya nchi yenyewe *sovereignty.* Tangu lini mpaka umehama? Hilo ndilo wenzio wanakushangaa kwa sababu sio kweli kwamba mpaka umehama. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Basi nafuta neno mpaka. Nasema kizuizi. Hapo sawa. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Endelea!

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kwa kuzingatia kwamba katika Mkutano wa Tisa, Mheshimiwa Marmo mwenyewe alisimama hapa na kusema Tarime inatawaliwa kwa sheria ambazo siyo zile tulizokubaliana katika Katiba ila inatawaliwa kwa sheria za kimila. Nadhani anafahamu vizuri sana mambo ya Tarime na yeye ni mhusika mkuu.

Sasa katika suala la Tarime, kuzuiwa kupelekewa chakula, watu wafe na njaa. Pale walipo wanahitaji *relief aid.* Kwa sababu tatizo halitokani na kabila la Wakurya kwamba wana koo, kila Waafrika wana koo zao, lakini ukilifuata lile suala *scientifically* utagundua kwamba kulikuwa na *colonial land policies* ambazo zilipitishwa mwaka 47 na kutenganisha zile koo na kuziwekea mipaka na *DC* mmoja anaitwa Inglam ambaye aliziwekea mipaka na akaziita *Chief Tenses* akaziwekea ma-*chief.* Leo hiyo mipaka ndiyo inaleta migogoro baada ya kuwa Serikali kuwa ilihamisha watu kutoka pale na kuwapeleka vijijini. Wakati zile sera za vijijini ziliposhindwa, Serikali ikawaambia watu warudi kwenye mahame yao, wakati wameongezeka idadi na mipaka haieleweki. Hicho ndiyo kilikuwa chanzo cha mgogoro mwaka 92 hadi leo.

Sasa cha kushangaza, Serikali yetu ina nguvu na ina *influence*, Serikali yetu imetatua migogoro ya Burundi. Juzi juzi Serikali ilikuwa inatatua mgogoro wa Comoro. Huku haisiti kuwapeleka akina Chacha, ndiyo wanaongoza vikosi huko kutafuta amani. Kenya tumetatua, lakini inashindwaje kutatua tatizo la koo. Kwa hiyo, kwa kufikiria kwangu ni kwamba Serikali ina sababu yake maalum ya kuacha watu waendelee kupigana. Wameuana hadi wamefika 30. Lakini watu wakiuawa wachache tu wa Afrika Kusini ni *International issue,* watu wanatangaza. Wakiuawana kumi na kitu huko Darfur inatangazwa mpaka mataifa yote yanayohusika. Lakini sasa kwa kusoma hii kwamba kuna kitu kinaitwa ubaguzi, basi inaonekana kwamba wale Wakurya siyo watu, maana wanakufa, hakuna *announcement* yoyote inayotolewa na Serikali wala kueleza ya kwamba wanataka kutatua huo mgogoro vipi.

Kwa hiyo, nilichokuwa nasema ni kwamba, kama Serikali yetu inatawala mpaka Tarime kwa nini isiwaangalie wale wananchi na kusitisha yale mapigano? Kwa sababu wale wananchi wako chini ya Serikali ya Muungano wa Tanzania. Hawako chini ya tawala za mila na koo. Kuna *OCD* na *DC* kuna Mahakama na kuna Kamati moja inaitwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ambayo ndiyo inapanga majeshi kule yanaitwa majeshi ya jadi ambayo hayapo kikatiba.

Kwa hiyo, moja kwa moja Serikali inahusika na mpaka sasa hicho kizuizi ambacho nimeambiwa nisikiite *blockade,* mimi ninaona kile kizuizi kimetuletea madhara makubwa, kwa sababu watoto 3,000 wanasoma Kenya. Mchele, mahindi, maharagwe, karanga ndiyo chakula chetu.

Waziri Mkuu aliyepita alikuja pale tarehe 26/11/2007 na akakaa na viongozi wote wa vijiji mpaka vitongoji na tukakubaliana wote pamoja kwamba atarekebisha ile mipaka kwa kuangalia zile *beacons* zilizowekwa kwa sababu ndiyo ramani inayotambulika

halafu atatengeneza *rules*. Sasa hata kama ameacha, si alikuwa anawakilisha Serikali! Kwa hiyo, namwomba Waziri Mkuu wa sasa ambaye ni mtu wa pale pia, shemeji yetu, aone kwamba wapya zake sasa pale wanakufa wakati yeye yuko madarakani. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Wangwe, mchango wako hauendani kabisa na hoja ya Waziri wa Fedha. *(Kicheko)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ninachosema ni kwamba, sisi tunalipa kodi na ni sehemu ya uchangiaji kwa sababu, Serikali inapata mapato makubwa sana kutoka Tarime. Wawekezaji pale wakiguswa kidogo kwamba wananchi wameokota mawe, inaleta askari 1,000. J

uzi tu mwezi wa nne, inaleta mpaka helikopta na magari. Kwa nini watu wanapokuwa wanauawa na majambazi Serikali inashindwa kuchukua hatua? Kwa hiyo, hii nazungumzia kuhusu ubaguzi wa kiserikali kwamba sasa tumewekewa *blocked* na hiyo ni bajeti. Kwa mfano wale watu sasa hawa-*produce* mazao yao, yanafyekwa, nyumba zao zimechomwa moto, hakuna *relief aid* inayokwenda. Hiyo ni *budget per se.* *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mkulo naomba uangalie kwamba pale masuala yako ya kukusanya kodi hayataenda vizuri pale mpakani Sirari, kwa sababu sasa mpaka umefungwa, Wakenya hawatakiwi kuja Tanzania, Watanzania hawaendi Kenya, kwa sababu Mkuu wa Mkoa anatekeleza Ilani ya kupambana na Wapinzani. Lakini nimhakikishie kwamba sasa ndiyo anawathibitishia wananchi wa Tarime ya kwamba upinzani ndiyo unaowawakilisha hapa. Sasa upinzani uta-*spread* nchi nzima nikiwa kama Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, turudi katika sheria na kusema kwamba tuna haki ya kuweza kupata chakula halafu ndiyo tuweze kuchangia bajeti ya Mheshimiwa Mkulo vizuri tukiwa tumeshiba na watoto wetu wanakwenda shuleni. Lile suala la mapigano, Serikali ikubali kwamba ndiyo iliyoanzisha kwa kuhamisha wananchi kutoka katika maeneo yao na kuwapeleka katika vijiji na hilo litawakuta Watanzania wote kwa sababu hii migogoro itakuwa nchi nzima kwamba Serikali mpaka sasa inamiliki ardhi yote kwa kitu kinachoitwa *radical tittle* kwamba mtu mmoja, Rais anamiliki ardhi yote. Kwa hiyo, nusu ya Mkoa wa Mara umechukuliwa na *TANAPA* mpaka Bunda. Mheshimiwa Wasira yuko hapa, ni Waziri lakini anaelewa wananchi wake sasa hivi wanataka kuandamana kwa mapanga.

Mheshimiwa Wanyancha wananchi wake hawana *space* hata ya kuweza kuwinda, maeneo yamechukuliwa na Kampuni inaitwa *VIP* ambayo inafukuza Wabunge wakienda kutembelea. Ina-*run* Serikali yake yenyewe, ina majeshi yake yenyewe. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, hapa kuna *situation* ya *state structure* ndiyo maana siamini ya kwamba Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wana uwezo wa kusimamia Serikali yao. Kwa sababu Serikali hii inaonekana inaendeshwa kwa nguvu nyingine siyo zao. Wao ni walalamishi tu hapa Bungeni kama sisi. Hawawezi waka-*decide* kitu humu ndani na

kikafanyika.  Kwa hiyo, naona suala la Wabunge kushindwa kusimamia Serikali ni matokeo ya Chama cha Mapinduzi na Wabunge wao.  *(Makofi)*

Kwa hayo machache, nafikiri *message sent,* tunaendelea. Ahsante sana.  *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:**   Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu!

**SPIKA:**  Samahani, kuhusu utaratibu!

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:**  Kuhusu utaratibu, Kanuni ya 68 fasili ya 7 naomba mwongozo wako Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:**   Naam!

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:**   Mheshimiwa Naibu Spika, alituambia kwamba kipindi hiki cha bajeti na baada ya hotuba ya Waziri Mkuu tunaruhusiwa kuongea kitu chochote, yaani tunaweza tukaongelea na akawa anatu-*convince* kwamba tunaweza tukaomba kuongea hata kipindi hiki ambacho tunasubiri kwa Waziri Mkuu kwa sababu anasema watu ni wengi sana.  Kwa hiyo, naomba mwongozo wako kwamba tunatakiwa tuchangie vipi?  Maana tunaambiwa kwamba tunaruhusiwa kuongea chochote.  Ahsante.

**SPIKA:**  Kanuni ndiyo zinatuongoza hapa. Nadhani ulivyomnukuu Mheshimiwa Naibu Spika, ule upeo ambao unakubalika una mipaka yake.  Ukichukua Wizara ya Fedha maana yake hoja iliyo mbele yetu ni hoja Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka huo wa fedha.  Ndiyo hoja iliyoko mbele yetu.

Sasa ukileta suala la ubaguzi na mipaka imehama ya nchi na kadhalika kidogo umekwenda mbali. Ni *sense* ya Spika kwamba mtu anayeweza kukuwekea mipaka, kwa sababu kanuni kwa ujumla zinasema kwamba tukiwa na mada mbele yetu tuongee kuhusu hiyo.  Mimi nilimwandikia kabla Mheshimiwa Chacha Wangwe.  Sasa niseme, tulisema ninahisi wewe panapokufaa ni kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, akakataa.

Sasa ameyatumbukiza yote hayo kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha ambaye masikini sidhani kama ataweza kujibu mambo ya mipaka, ubaguzi na *sociology* ya Wakurya na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, hiyo ndiyo mipaka ambayo lazima tuiweke. Tunaendelea Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:**  Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu ya Waziri wa Fedha kuhusu bajeti ya Serikali.  Awali ya yote, nimpongeze na kumshukuru sana Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake nzuri mbadala na ndiyo sababu baadhi ya Wabunge wamesema kwenye vyombo vya habari wanaandika sana kuhusu bajeti ya Upinzani. Nadhani wameridhika nayo na ndiyo sababu wanaandika.  *(Makofi)*

Lakini pia niipongeze sana, pia na Waziri wa Fedha, Manaibu wake na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa waliofanya ya kuleta bajeti hii pamoja na mapungufu, lakini kwa kweli wamefanya kazi. Kwa hiyo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi yameshasemwa, lakini na mimi nijikite kwenye mambo machache hasa nikianzia na suala zima la hali ya uchumi. Katika kitabu cha Hali ya Uchumi aliyowasilisha Mheshimiwa Waziri wa Fedha, anasema kwamba pato la Taifa limekuwa kwa asilimia 7.1 na zaidi ya hapo anasema kwa wastani wa Mtanzania anapata Sh. 548,588/= kwa mwaka. Ukipeleka kwa mwezi ni Sh. 45,000/= na kwa siku ni Sh.1,500/= kwa mwezi wa siku 30.

Mheshimiwa Spika, huu ni wastani ikiwa inamaanisha kwamba wale wenye vijisenti vyao pia wako *inclucive*. Kwa hiyo, ina maana wale wasiokuwa na hela kuna watu ambao wanaweza wakawa wanakosa hata dola moja kwa siku. Kwa hiyo, nadhani bado hatujafika mbali na hii ni kwa sababu ya kutokuwa na sehemu nyingine za kupata kodi. Lakini zaidi ya hapo labda kwanza niwapongeze sana *TRA* kwa kazi kubwa wanayoifanya kukusanya kodi na nimpongeze sana Mwenyekiti wa Bodi, Dada yangu Macelina Jijoriga kwa kazi kubwa anayofanya. Naamini wanawake tunaweza na ndiyo sababu *TRA* imefikia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende zaidi kwenye suala la kilimo. Kilimo ni uhai na kumekuwa na matamko mbalimbali kuhusu kilimo bora, kilimo ni uti wa mgongo na kweli kilimo ni uti wa mgongo kwa nchi kama Tanzania.

Mheshimiwa Spika, inajulikana kwamba zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima wadogo wadogo na kwa maana hiyo ajira kubwa ziko kwenye kilimo. Lakini kilimo kimetupwa kabisa, bajeti ya mwaka huu ni 3% ndio imetengwa kwa kilimo na sisi tunajua katika vipaumbele vyetu kilimo ni mojawapo lakini imepata 6% tu ya bajeti, kwa njia hii au kwa *style* hii hatuoni kwamba kilimo kitaendelea. Zaidi ya hapo tunajua kwamba udongo mwingi wa Tanzania tayari umechoka na hivyo unahitaji mbolea.

Mbolea bei zake bado ni za juu sana na hivyo kufanya wakulima wengi kushindwa kuinunua, lakini baada ya kushindwa kuinunua unakuta kwamba mavuno yao ni finyu sana. Kwa hiyo, tulikuwa tunafikiri kwamba ni muhimu Serikali ikaangalia ni jinsi gani inaweza ikawasaidia wakulima hasa kuwapatia pembejeo za kilimo pamoja na mbolea ili waweze kuvuna au tuwe na kilimo kizuri zaidi hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, labda nitoe tu ufafanuzi kuhusu suala la kilimo. Kumekuwa na wataalamu wengi na wamekuwa wameelezea hali ya kilimo na wakasema kwamba umasikini wa Watanzania au wa Afrika Mashariki, unatokana na kilimo chetu ambacho tunakifanya kama ni *business as usual* na sio kile ambacho ni *productive agriculture*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nategemea kwamba Serikali kupitia wataalamu wa kilimo waone ni jinsi gani wanaweza wakafanya kilimo cha sasa hivi kiwe

*more productive* na sio *business as usual.* Lakini pamoja na hilo nilikuwa nafikria pia kwenye suala zima la Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Huko nyuma kilimo cha umwagiliaji kilikuwa kimepewa kipaumbele na ndio sababu tukawa na ekari zaidi ya 450,000 hapa Tanzania za umwagiliaji, lakini sasa hivi ekari hizo zimepungua na zimebaki karibu mia mbili tisini na kitu. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kwa bajeti ya umwagiliaji na maji kupungua ina maana kilimo cha umwagiliaji bado kitaendelea kwenda chini.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nadhani kwamba kilimo cha kutegemea mvua hapa Tanzania na tukizingatia kwamba hali ya hewa huwa inabadilika sana inakuwa ni hatari sana kwa mkulima kwa sababu fedha zake zote anaingiza kwenye mbegu na pembejeo, lakini bado mkulima huyo hawezi kupata chochote kwa sababu ya ukame. Kwa hiyo, ifikie mahali kwamba kilimo tukipe kipaumbele hasa cha umwagiliaji ikizingatiwa kwamba mazingira na hali halisi ya kijiografia ya Tanzania mara nyingi haina mvua wakati wote.

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo labda niende kwenye suala zima la maisha bora kwa kila Mtanzania. Hii ni kauli mbiu ya *CCM* ambayo kwa kweli mimi nadhani kila Mtanzania angependa kuwa na maisha bora. Lakini maisha bora hayo bado kabisa hayajamfikia Mtanzania na ndio sababu kuna Watanzania wengi wanaoishi kwa mlo mmoja.

Sasa hivi kwa mfano nichukulie suala ambalo linanikera sana, ni suala la kuruhusu Wamachinga wa kichina kufanya biashara Kariakoo. Wachina wale wameua kabisa ile dhana ya kumwezesha Mtanzania kuwa mjasiriamali au kufanya au kufanya biashara ndogo ndogo. Wachina wale wanaleta bidhaa zao moja kwa moja kutoka kwenye viwanda vyao China na wanakuja kuuza, kwa hiyo, unakuta lile soko la ndani la Watanzania wetu ambao ndio ajira zao walizokuwa wanafanya limepungua sana na wengi wanakata tama kabisa ya kufanya biashara.

Kwa hiyo, nilikuwa nadhani ni bora Serikali ione ni jinsi gani inaweza kuwasaidia Watanzania wetu waliokuwa wanafanya biashara waendelee na biashara zao ndogo ndogo na sio kuwakumbatia Wachina ambao kwa kweli mimi nadhani wale wanaweza kufanya biashara kubwa zaidi ya hizi za nguo au za vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la *UKIMWI*. Kwanza, nashukuru kwamba niliweza kwenda kwenye *delegation* ya Marekani kwenye Mkutano wa *UKIMWI* na pale Rais wa kwanza wa Zambia, Keneth Kaunda, alitoa ripoti ya *UKIMWI*, kwa kweli hali ya *Sub-Sahara Africa* inatisha. Labda tu naomba ninukuu, ni kwa Kiingereza, lakini naweza nikasema kwa Kiswahili, baadhi ya nchi za Afrika chini ya Sahara, nchi sita, sasa hivi *life expectance* ni chini ya miaka 40 hii ikiwemo Zambia, *Central Africa Republic*, Lesotho, Swaziland, Zimbabwe na Botswana.

Lakini kama Tanzania hatutaweza kudhibiti hali hii na sisi tunaweza tukaelekea huko maana yake bado sisi nadhani tuko kwenye miaka 48.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, Wizara ya Fedha ione ni jinsi gani inaweza kuwapatia Wizara ya Afya, kwa sababu Wizara ya Afya kutokana na lile azimio la Abuja ilikuwa inatakiwa ipewe, kila Wizara ya Afya katika nchi za *Sub-Sahara* wapate asilimia 15 ya bajeti, lakini sasa hivi iko karibu asilimia 10. Kwa hiyo, nilikuwa ndhani kwa kweli suala la *UKIMWI* tulipe kipaumbele kwa sababu wengi wanaoathirika ni vijana na vijana ndio nguvu kazi ya Taifa hili. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri tuone ni jinsi gani tunaweza kusaidia hasa wale ambao wameathirika kupata dawa.

Mheshimiwa Spika, taarifa nilizonazo ni kwamba sasa hivi wale ambao wana *CD 4* chini ya 200 ambao wanapaswa kupewa dawa Tanzania wako zaidi ya 400,000 ambao wamepimwa lakini kwa sasa hivi ni 150,000 tu ndio wanapata dawa. Kwa hiyo hili ni tatizo kubwa sana kwa sababu zile dawa mtu ukishaanza inabidi uendelee.

Kwa hiyo, nilikuwa nadhani ni vyema wagonjwa wote ambao wameshajulikana wana *CD 4* chini ya 200 waweze kupata hizo dawa. Kwa hiyo, iwe na ile *universal access to ARVs,* bila hivyo tutakuwa tunapoteza nguvukazi ambayo kwa kweli itafanya Taifa letu liendelee kuwa masikini sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilitaka kuliongelea ni suala zima la elimu. Baba wa Taifa aliwahi kusema kwamba tuna maadui wakubwa watatu hapa Tanzania ambao ni ujinga, maradhi na umasikini. Lakini *on top of that* ni kwamba mimi naamini kabisa tukiweza kuondoa ujinga, haya mengine yanaweza yakaisha.

Lakini pamoja na kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, bajeti yake ni nzuri ni kubwa lakini bado. Niko katika Kamati ya Huduma za Jamii na Wizara ya Elimu iko chini ya Kamati hii tunaikagua. Elimu ni kitu cha msingi sana katika maendeleo ya nchi yoyote ile, lakini suala la ukarabati au ujenzi wa vyuo pamoja na shule hapa nchini bado ni tatizo. Kwa mfano shule zimetengewa fedha nyingi *MES* kwa ajili ya ujenzi, lakini vinavyojengwa ni *sub-standard* kiasi kwamba fedha zinakuwa ile *value for money* haionekani, lakini kikubwa nilichotaka kuongelea kuhusu elimu ni suala zima la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinachukua takribani wanafunzi 20,000, ukilinganisha na vyuo vya binafsi vyote nchini ukiviweka kwa ujumla wake haviwezi kufikia hiyo namba. Lakini ni jambo la kusikitisha kuona kwamba miundombinu ya chuo kile ni mibovu sana na tulipoongea na uongozi wa Chuo Kikuu ulisema wangehitaji kama Sh. 100,000,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa chuo kile. Lakini katika bajeti Chuo kile kimetengewa Sh. 2,000,000,000/= tu za ukarabati. Kwa hiyo, tulikuwa tunafikiri ni vyema Wizara ya Fedha iangaliwe ni jinsi gani inaweza kutatua tatizo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hii ikiwa ni pamoja na vyuo vingine lakini hicho kwa kweli ndio kimetia fora katika uchakavu wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, sasa labda niende kwenye suala la mawasiliano. Suala la mawasiliano sio anasa, mawasiliano ni muhimu sana hasa vijijini na Mheshimiwa Sanya, ameshaongelea kwamba ilani ya *CCM* inasema hivyo na mimi nakubaliana nayo ni muhimu sana. Lakini sasa nashangaa, Serikali hiyo hiyo ya *CCM* inajikana yenyewe

kwamba sasa wanataka wapandishe kodi, ukiangalia nchi zote za Afrika Mashariki, jumla ya kodi kwa Tanzania ni asilimia 81 ya simu ukilinganisha na Kenya ambayo ni asilimia 43 na Uganda asilimia 53. Hili ni tatizo kubwa sana! Sasa hivi tuko 5% bado wengi hawawezi ku-*access* simu.

Mheshimiwa Spika, mimi siamini kama kuna Mbunge hata mmoja hapa ambaye ha-bipiwi na wapigakura wake, kwamba wanaku-*beep* wewe sasa ndio uwe wa kupiga. Kama katika hii 5% watu ambao tuna uwezo kidogo wa simu tunapata matatizo hayo: Je, tukiongeza ikafika asilimia 10 itakuwa vipi? Kwa hiyo, mimi nilikuwa nadhani suala la mawasiliano sio suala la anasa, ni suala la muhimu sana katika maendeleo ya nchi yoyote ile.

Kwa hiyo, suala la kupandisha kodi mimi napingana nalo na nilikuwa naomba Wizara ilione hilo isije ikawa sasa tunaongeza yale matabaka kwamba wanaokuwa na simu ni Wabunge na viongozi wa Serikali tu kwamba wale wapigakura wetu wote tuwaache hawawezi ku-*access communication.* Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana hili liangaliwe upya na kodi ama ibaki pale pale au ishuke ili wananchi wa vijijini ambao ilani yenyewe ya *CCM* ambacho ndio Chama tawala imesema, basi itekelezwe isije tukaona kwamba huu ni usanii *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, suala lingine nililotaka kuzungumzia ni suala zima la *Finance Bill.* Tukiangalia kwenye *Finance Bill,* Mheshimiwa Waziri, anaomba kwa mfano ukurasa ule wa 12, naomba kunukuu kuhusu suala la Mamlaka ya Mawasiliano. Wakati Mheshimiwa Waziri anaomba apatiwe kibali na Bunge, tunaomba Mheshimiwa waziri, atuambie siku za nyuma kwa mfano mwaka 2006, Ofisi ya Waziri Mkuu, iliiomba *TCRA* kutoa Sh. 10,000,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Bagamoyo – Msata na hizi hela zilitoka. Je, Waziri huyo alipata kibali wapi na sasa anataka Bunge hili liidhinishe hii sheria? Lakini lingine pia waliiomba hiyo hiyo *TCRA* kukarabati uwanja wa ndege wa Mwanza. Sasa tulikuwa tunaomba kujua hivi Waziri anapoleta hii *Bill* sasa hivi na tayari alishavunja hii Sheria anataka sisi sasa hivi tufanye nini?

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nilitaka kuongelea kidogo suala zima la miundombinu. Maendeleo yote ya nchi huletwa na barabara pamoja na reli na viwanja vya ndege. Ni ukweli ulio wazi kwamba barabara zetu ni mbovu sana na hasa za Mikoa ya pembezoni ikiwemo Rukwa, Kigoma na huku Kusini. Ukiangalia miaka hiyo ndio wazalishaji wakubwa sana na wanaoingiza pato la nchi hii kwa kiasi kikubwa.

Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba, ukiangalia hata mwaka 2008 kwa mfano, walikarabati barabara kwa kiasi cha kilometa 8,611 wakati mwaka huu wameweza kukarabati 5,062. Kwa hiyo, ukiangalia unaona kwamba pamoja na kwamba fedha zimeongezwa bado ukarabati wa barabara umekuwa mdogo, nilikuwa nadhani tatizo kubwa labda liko katika Halmashauri. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali Kuu, ione ni jinsi gani inaweza kupeleka wataalamu ili barabara ziweze kujengwa. Fedha zipo kwenye Halmashauri, lakini nadhani tuna tatizo la wataalamu kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri Wizara ione ni jinsi gani inaweza kusaidia ili barabara zetu ziweze

kutengenezwa na ziweze kupitika ili mkulima aweze kufaidika na yale mazao ambayo ameweza kuyalima yaweze kufika sokoni na apate kile ambacho anastahili, nashukuru.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimepanga kwamba tuwe na mzungumzaji mwingine, lakini hesabu zangu hazikukaa vizuri. Inaonekana sasa haitawezekana. Lakini nitoe tu taarifa nzuri kwamba wachangiaji wanne ambao ninao bado kwenye orodha ili tukamilishe na kumaliza kabisa shughuli hii, nitawapa nafasi kesho asubuhi. Nao ni kwanza, Mheshimiwa Anna Abdalah; wa pili, Mheshimiwa Maulida Komu; wa tatu, Mheshimiwa Devotha Likokola na nitamalizia na Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, saa 4:00 mpaka saa 5:00 halafu tutaendelea sasa na utaratibu wa kuweza kusikia hoja zikipata majibu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa muda uliosalia haumtoshi mtu yeyote kuchangia na hatuwezi kuendelea kwa mujibu wa kanuni, kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi kesho saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 01:50 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 20 Juni, 2008 saa 03:00 Asubuhi)*